MWANANCHI WA KAWAIDA KAMA MDHULUMU WA MASLAHI YAKE KATIKA TAMTHILIA ZA *KILIO CHA HAKI*, *AMEZIDI* NA *MSTAHIKI MEYA*.

NA

RONIC GADDAFI OMOGA

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta

MACHI, 2018

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine.

_____ _____

RONIC GADDAFI OMOGA **TAREHE**

Tasnifu hii imetolewa kwa chuo kikuu kwa idhini yetu kama wasimamizi.

_____ _____

DKT. R. M WAFULA **TAREHE**

_____ _____

MWALIMU P. M. MUGAMBI **TAREHE**

TABARUKU

Ningependa kuitabaruku kazi hii kwa mke wangu mpendwa Bi. Deborah Nyaboke na Binti zetu Stacey Ronic na Natasha Ronic. Sitawasahau kamwe kwa kunihimiza katika kazi hii. Aidha naitabaruku pia tasnifu hii kwa wananchi wa kawaida ambao wametambua umuhimu na nafasi zao katika kuzuia dhuluma.

SHUKRANI

Kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na baraka zake hadi mwisho wa kazi hii. Shukrani zangu za dhati pia ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Richard Wafula na Mwalimu Peter Mugambi kwa kunieleza na kunielekeza katika kila hatua ya kazi hii. Msaada wenu wa maoni, fikra, maarifa, mwongozo, mapendekezo na motisha ulinifaa sana. Ahsante sana kwa uvumilivu wenu na Mungu awabariki kwa kila hali na kwa kila njia aushini mwenu.

Aidha, shukrani ziwaendee wahadhiri wote katika Idara ya Kiswahili ambao walinifaa kwa maarifa mengi. Ahsanteni sana. Pia shukrani za dhati zimwendee mke wangu Deborah Nyaboke na binti zetu Stacey na Natasha kwa kunipatia nafasi na motisha ya kuendelea na kazi hii japo walikosa muda wa kutosha kujumuika nami. Ninawashukuru kwa uvumilivu wenu na Mungu awabariki sana.

Shukrani zingine za kipekee ziwaendee Charles Sereti, Lameck Matara, Don Oiriga, Job Juma, Julia Ali na Yournina Oguba kwa upendo na kunitia motisha katika kipindi chote cha masomo. Sitawasahau wazazi wangu Bwana Sylvester Omoga na Bi. Mary Gesare kwa kunitia ari ya kuendeleza masomo yangu. Nawashukuru ndugu zangu Josephat Omonyi, Timothy Ombasa, Jesnah Nyambeki na Dolphine Mokeira kwa kunipa moyo na usaidizi wao wa hali na mali hadi kukamilika kwa kazi hii.

Mwisho ninawashukuru rafiki zangu chuoni walionifaa kwa njia mbalimbali tukiwa katika makundi ya mijadala mbalimbali. Ni wengi mno lakini nitawataja wachache kama vile Vincent Makini, Hellen Ngure, Sarah Mose, Vincent Misigo, Moses Owino miongoni mwa wengine. Kwa wale ambao sikuweza kuwataja, usaidizi wenu umenakiliwa katika mtima wangu na kwenu nyote ninasema Mungu awabariki sana.

IKISIRI

Utafiti huu ulichanganua kazi za Al- Amin Mazrui, Timothy Arege na Said Ahmed Mohamed ambazo ni tamthilia za *Kilio cha Haki (1981)*, *Mstahiki Meya (2009)* na *Amezidi (1995)* mtawalia. Kazi hizi zililenga kumsawiri mwananchi wa kawaida kama chanzo cha dhuluma dhidi yake. Kwa kutumia sifa mbalimbali za wahusika, kazi hizi zinaangazia maisha ya wananchi katika nchi zinazoendelea hasa katika kipindi cha ukoloni na baada ya ukoloni. Utafiti huu unapania kuonyesha kuwa shida wanazokumbana nazo wananchi katika mataifa yanayoendelea zinatokana na wananchi wenyewe. Kwa hivyo, utafiti umebainisha baadhi ya matendo wanayoshiriki wananchi ambayo yanawafanya wajidhulumu. Nadharia ambazo ziliongoza utafiti huu ni nadharia ya uhalisia wa kijamaa ya Friedrich Hegel na nadharia ya udenguzi ya Jacques Derrida . Nadharia ya udenguzi imeasaidia katika kubainisha jinsi maoni ya waandishi wengi kuhusu chanzo cha dhuluma kwa mwananchi si ya hakika. Waandishi wengi wanahusisha kuteseka kwa mwananchi na umaskini, uongozi mbaya, mila zilizopitwa na wakati miongoni mwa sababu nyingine. Utafiti unalenga kuonyesha kuwa kwa kiwango kikubwa, ni mwananchi aliye chanzo cha dhuluma anazokumbana nazo. Nadharia ya uhalisia wa kijamaa imemwezesha mtafiti kuhakiki na kuchambua hali na maisha halisi ambamo wananchi wa kawaida hujidhulumu. Utafiti huu ulifanywa maktabani na tamthilia teule zilichaguliwa kwa njia makusudi ikilenga tamthilia za *Mstahiki Meya*, *Kilio cha Haki* na *Amezidi*. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa maelezo kwa kufuata utaratibu huu: sura ya kwanza ya utafiti imetanguliza mada, maswali yanayoongoza utafiti, malengo ya utafiti, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, sababu za kuchagua mada na misingi ya nadharia. Sura ya pili ilihusu chanzo cha dhuluma kwa mwananchi wa kawaida. Sura ya tatu ilishughulikia athari zinazotokana na dhuluma kwa mwananchi kwa kuangazia tamthilia teule. Sura ya nne ilishughulikia mikakati ya mwananchi katika kuzuia dhuluma nayo sura ya tano ilishughulikia matokeo ya utafiti pamoja na mapendekezo ya mtafiti. Inatarajiwa kuwa utafiti huu umekuwa wa manufaa katika kuonyesha nafasi aliyonayo mwananchi katika kujikomboa au kujidhulumu. Aidha, utafiti huu utakuwa wa muhimu kwa wananchi kufahamu nafasi zao katika kubainisha uongozi bora.

ABSTRACT

This research analysed the works of Al- Amin Mazrui, Timothy Arege and Said Ahmed Mohamed, *Kilio Cha Haki (1981), Mstahiki Meya (2009)* and *Amezidi (1995)* respectively. These works intend to show how the common man is portrayed as the author of his own oppression. By employing character traits of various characters, these works depict the way of life of citizens in developing countries especially during the colonial and post-colonial period. The research has demonstrated that the problems encountered by citizens in the developing world originate from the citizens themselves. Therefore, the research has identified the actions done by citizens that result in self-defeat. The theories that guided this research are Realism of Friedrich Hegel and Deconstruction of Jacques Derrida. Deconstruction theory aided in showing how untrue the views held by many authors are about the causes of oppression to the common man. Most authors attribute suffering of the common man to poverty, poor leadership and archaic traditions among other reasons. The research has demonstrated that to a larger extent, it is the common man who is the author of his or her oppression. Realism enabled the researcher to describe and analyze the problems encountered by citizens in which they oppress themselves. This research was carried out in the library and texts were selected through purposive sampling focusing on *Mstahiki Meya, Kilio cha Haki* and *Amezidi*. The outcome from the selected texts was presented in the following order: chapter one entails topic of study, research questions, objectives of the study, scope of study, literature review, the purpose of the study and the theoretical framework. Chapter two entails ways through which common man oppresses himself or herself. Chapter three has dealt with effect of oppression on the common man by focusing on the selected texts. Chapter four entails different ways through which common man can prevent oppression and chapter five entails the outcome of the research and the researcher's recommendations. It is expected that this research will be of importance in revealing the role of the ordinary person in liberating or oppressing himself or herself. It will also be of great significance to the citizens in comprehending their roles in determining good leadership.

UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

Dhuluma: Ni kitendo kisicho cha haki: uonevu, ukatili (Kamusi ya Kiswahili Sanifu, 1981).

Dhuluma ni hali ya kutumia mamlaka au uwezo kwa njia isiyo haki; katili au kuwataabisha wengine. Ni hali ya kuhisi kubebeshwa mizigo kiakili au kimwili. Katika utafiti huu, dhuluma itachukuliwa kumaanisha matendo yoyote ya mwananchi yanayokiuka haki za mwananchi yuyo huyo. Itajumuisha kukubali kudanganywa, kukubali kupigwa, kutojiamini au kutotoa maoni yao kuhusu yale mabaya yanayowakumba.

Mwananchi: Mtu ambaye ni mwenyeji wa nchi fulani. Katika utafiti huu, mwananchi au wananchi ni watu wa kawaida hasa wanaotawaliwa na ambao ni wahusika katika tamthilia teule ambazo zinarejelea nchi za Afrika Mashariki.

Nchi zinazoendelea: Nchi zinazoendeleza shughuli za kuboresha uchumi wao baada ya kuzoroteshwa na ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo unaotokana na ubepari hasa katika Bara la Afrika. Nchi zitakazoangaziwa katika utafiti huu ni zile za Afrika Mashariki ambazo ni Kenya, Uganda na Tanzania.

YALIYOMO

Mada.....i

Ungamo ii

Tabaruku.....iii

Shukrani iv

Ikisiri vi

Abstract vii

Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu.....viii

Yaliyomo ix

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi 1

1.1 Suala la Utafiti 3

1.2 Maswali ya Utafiti.....4

1.3 Malengo ya Utafiti 5

1.4 Sababu za Kuchagua Mada.....5

1.5 Upeo na Mipaka.....7

1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada 8

1.7 Misingi ya Nadharia.....19

1.7.1 Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa. 19

1.7.2 Nadharia ya Udenguzi 23

1. 8 Mbinu za Utafiti 28

1.8. 1 Muundo wa Utafiti 28

1. 8.2 Mahala pa Utafiti 28

1. 8.3 Uteuzi wa Sampuli 29

1. 8. 4 Ukusanyaji wa Data 29

1. 8.5 Uchanganuzi wa Data 29

1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo 30

1.9 Hitimisho 30

SURA YA PILI: CHANZO CHA DHULUMA KWA MWANANCHI

2.1 Utangulizi 31

2.2 Itikadi 31

2.3 Uchumi 41

2.4 Matusi na Dharau 47

2.5 Ufisadi 53

2.6 Hitimisho 58

SURA YA TATU: ATHARI ZINAZOTOKANA NA DHULUMA KWA MWANANCHI

3.1 Utangulizi 60

3.2 Kifo 60

3.3 Umaskini 68

3.4 Utengano wa Kijamii 75

3.5 Hitimisho 81

SURA YA NNE: MIKAKATI YA MWANANCHI KATIKA KUZUIA DHULUMA DHIDI YAKE

4.1 Utangulizi 83

4.2 Kuwachagua Viongozi Bora 84

4.3 Kuweka Juhudi 89

4.4. Kuwa Jasiri 94

4.5 Kufahamu Haki 99

4.6 Hitimisho 102

SURA YA TANO: HITIMISHO

5.1 Utangulizi 104

5.2 Muhtasari Wa Utafiti 105

5.3 Matokeo Ya Utafiti 108

5.4 Mchango Wa Utafiti 111

5.5 Mapendekezo 113

MAREJELEO 115

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Baadhi ya watunzi wanaamini kwamba umaskini wa wakazi wa nchi zinazoendelea umesababishwa na unyonyaji wa kimataifa. Pia, wanaamini kwamba miongozo na mipango ya maendeleo ya nchi zinazoendelea haitilii maanani mahitaji ya kimsingi ya wananchi wa mataifa hayo (Wafula, 1999). Utafiti huu kupitia fasihi kama kioo cha jamii unapania kuonyesha jinsi mwananchi wa kawaida kupitia kwa matendo na maamuzi yake anavyojidhulumu. Waandishi Al- Amin Mazrui, Timothy Arege na Said Ahmed Mohamed wanaonyesha kwa kutumia sifa za wahusika jinsi wahusika mbalimbali wanajidhulumu. Wahusika katika tamthilia za *Kilio cha Haki (1981), Mstahiki Meya (2009)* na *Amezidi (1995)* wamesawiriwa kuwakilisha wananchi katika ulimwengu halisi. Hivyo basi, tabia zao, shida zao na ufanisi wao unafanana na tabia, shida na ufanisi wa wananchi wa kawaida katika ulimwengu halisi.

Kabla ya ukoloni mkongwe, ilichukuliwa kuwa wakoloni ndio waliowanyanyasa Waafrika kwa kila njia hasa katika mataifa yaliyotawaliwa na wakoloni. Si ubaguzi wa rangi, si kiuchumi na si kisiasa. Kutokana na mwelekeo huu, Waafrika waliungana wakaanza kupigania uhuru wao, jambo lililosababisha vifo vingi (Kareithi, 1969). Hata hivyo, walifanikiwa kujikomboa kutoka kwa dhuluma za mkoloni. Ajabu ni kuwa, baada ya kujinyakulia uhuru, shida za Waafrika hazikuisha bali zilibaki Afrika na kuendelezwa na Mwafrika mwenyewe dhidi ya Mwafrika mwenzake. Badala

ya kupatikana kwa suluhisho, pamekuwapo na lawama na kunyosheana vidole na kusababisha mtafaruku zaidi. Kwa mfano, baada ya uhuru, shida zilizomkumba Mkenya wakati wa ukoloni kama vile umaskini, njaa na mauaji bado zipo. Mathalan, baada ya kujinyakulia uhuru, Waafrika walianza kuzozana kuhusu nani awe kiongozi wa nchi zao. Mzozo huu ulisababisha kutoaminiana miongoni mwa Waafrika anavyodokeza Abdilatif Abdalla (1973: 36) katika shairi lifuatalo:

> Mamaetu Afrika, wanayo tu msibani
> Msiba umetufika, ndugu hatusikizani
> Kila mmoja ataka, awe mshika sukani
> Litawezekana lini? Hebu tuamuwe mama
>
> Wale maadui zetu, haweshi kutufitini
> Si watu hawa si watu, ni wanyama wa mwituni
> Hawapendi mamaetu, kukuona u furahani
> Bali uwe simanzini, ndivyo watakavyo mama
> Ndivyo mwanzo ndugu zetu, wenda kinyume na sisi
> Wakishika kila chetu, na kukiuza rahisi
> Waivunda hadhi yetu, sote tuliyo weusi
> Wapenda zao nafusi, na maaduizo mama

Katika shairi hili, Abdalla (1973) anaonyesha jinsi Waafrika walivyokuwa waking'ang'ania mamlaka baada ya kujinyakulia uhuru jambo lilosababisha uhasama kati ya Waafrika wenyewe na kuanza kupigana.

Katika utangulizi wa Diwani ya *Dhifa* (2008), Wamitila anaeleza kuwa Kezilahabi ametumia taswira inayowasawiri viongozi kama fisi, mazimwi, majibwa na madikteta ambao ndio chanzo cha utawala mbaya, ubaguzi miongoni mwa dhuluma nyingine. Kwa mfano, shairi la *Madomo Mapana* (Kezilahabi, 2008: 7) linaonyesha kuwepo kwa viongozi ambao wanajifikiria wenyewe huku raia na nchi zenyewe zinafanananishwa na ng'ombe

anayekamuliwa maziwa mpaka akatokwa na damu. Ni kutokana na mtazamo huu kuwa dhuluma nyingi kwa wananchi husababishwa na viongozi, ambapo utafiti umechunguza nafasi ya mwananchi katika shida zinazoikumba Afrika Mashariki. Ili kufanikisha utafiti huu, tamthilia za *Mstahiki Meya*, *Amezidi* na *Kilio cha Haki* zilizoandikwa na Timothy Arege, Said Ahmed Mohamed na Al-Amin Mazrui mtawalia zimesomwa na kuchambuliwa. Wahusika katika tamthilia hizi wamesawiriwa kuwakilisha wananchi katika nchi za Afrika Mashariki ambazo ni miongoni mwa nchi zinazoendelea. Aidha, utafiti umechunguza shida anazokumbana nazo mwananchi wa kawaida na wajibu wake katika kukomesha shida hizo.

1.1 SUALA LA UTAFITI

Miongoni mwa majukumu ya fasihi katika jamii ni kuipa jamii mwelekeo, kutoa maadili, kuonya, kuelimisha, kushauri kati ya majukumu mengine. Baadhi ya waandishi wamezingatia masuala ya dhuluma katika kazi zao na wamefanya hivyo kwa kutumia mashairi, hadithi, tamthilia na hata tasnifu wakiwa na lengo la kuhamasisha, kuonya na kuhimiza waliodhulumiwa kujifunga kibwebwe kukabiliana na dhuluma zinazowakumba na kuwapa tumaini. Kwa mfano, kuna tafiti zilizoshughulikia dhuluma dhidi ya watoto (Burgess, 1979), dhuluma dhidi ya wanawake (Momanyi, 1998) na dhuluma dhidi ya wanaume (Gitau, 2005). Sababu nyingi zimetolewa kueleza chanzo cha dhuluma hizi zikiwemo uongozi mbaya, umaskini na utamaduni uliopitwa na wakati. Orodha ya chanzo cha dhuluma kwa watoto, wanawake na

wanaume ambao ni wananchi huepuka kutaja nafasi ya mwananchi mwenyewe katika kusababisha dhuluma zinazomkumba. Ni kutokana na kutomchunguza kikamilifu mwananchi ili kubainisha nafasi yake katika masaibu yanayomkumba ambapo utafiti huu umepania kuchanganua nafasi ya mwananchi katika kuendeleza dhuluma anazokumbana nazo katika maisha. Aidha, utafiti huu umechunguza maigizo katika tamthilia za *Mstahiki Meya* (2009) yake Timothy Arege, *Amezidi* (1995) yake Said Ahmed Mohamed na *Kilio cha Haki* (1981) yake Al- Amin Mazrui ili kubainisha namna suala la mwananchi wa kawaida kama mdhulumu wa maslahi yake lilivyosawiriwa kupitia wahusika na maudhui mbalimbali. Utafiti unanuia kuonyesha mchango au nafasi ya mwananchi wa kawaida katika dhuluma anazokumbana nazo na njia anazoweza kuzitumia kuepukana na dhuluma hizo.

1.2 MASWALI YA UTAFITI

Utafiti huu utaongozwa na maswali yafuatayo:

a) Tamthilia za *Kilio cha Haki*, *Mstahiki Meya* na *Amezidi* zimebainisha chanzo cha dhuluma kuwa nini?

b) Ni athari zipi zinazotokana na dhuluma kwa mwananchi?

c) Mwananchi anaweza kutumia mikakati gani kujiepusha kutoka kwa dhuluma zinazomkumba kwa mujibu wa tamthilia zilizoteuliwa?

1.3 MALENGO YA UTAFITI

Uhakiki wa tamthilia za *Kilio Cha Haki*, *Mstahiki Meya* na *Amezidi* utafanywa kutimiza malengo yafuatayo:

a) Kuonyesha namna tamthilia za *Kilio cha Haki*, *Mstahiki Meya* na *Amezidi* zilivyobainisha chanzo cha dhuluma.
b) Kubainisha athari zinazotokana na dhuluma kwa mwananchi.
c) Kuonyesha mikakati anayoweza kuitumia mwananchi kuepukana na dhuluma kwa mujibu wa tamthilia zilizoteuliwa.

1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Kulingana na Mohamed (2001), msanii ana dhima ya kuelimisha, kuongoza na hata kukashifu maovu yaliyopo katika jamii kwa vile huathirika jinsi wanajamii wengine huathirika, ndiposa huandika masuala yaliyomo kwenye jamii kama vile kazi na ukosefu wa kazi, unyonyaji, ukoloni na ubeberu, uzalendo, usaliti miongoni mwa mambo mengine. Kutokana na masuala haya, utanzu wa tamthilia una sehemu muhimu katika dhima ya fasihi ya kukosoa, kuhamasisha, kutahadharisha, kufundisha, kuelimisha na kufafanua utamaduni wa jamii. Uhakiki wa tamthilia za *Mstahiki Meya*, *Amezidi* na *Kilio cha Haki* umefanywa ili kuupa utanzu wa tamthilia dhima yake inayostahiki. Uhakiki huu umekusudia kuonyesha jinsi utafiti huu kuhusu utathmini wa mwananchi kama mdhulumu wa maslahi yake unavyoweza kuwa onyo kwa jamii dhidi ya mienendo inayoweza kuwafanya wajidhulumu.

Vilevile, utafiti huu unalenga kuonyesha mchango wa mwananchi katika dhuluma zinazomkumba kinyume na mtazamo wa baadhi ya waandishi ambao hushikilia kuwa mwananchi hudhulumiwa na walio mamlakani pekee. Kwa mfano, inaaminika kuwa kwa kiwango kikubwa, viongozi huwasababishia wananchi njaa, ukame na mambo mengine mengi yenye athari hasi katika maisha ya wananchi. Ndiposa Kezilahabi (2008) anawafananisha viongozi na mazimwi, majibwa na madomo mapana katika mashairi yake ya *Jibwa, Madomo Mapana* na *Zimwi* katika Diwani ya *Dhifa.* Aidha, katika Diwani ya Msimu wa Tisa (2007), Kithaka wa Mberia pia amewasawiri viongozi kama wasaliti katika mashairi ya *Usingizini*, *Tope la Mizozo, Werevu* na *Msimu wa Tisa*.

Fauka ya utafiti huu kuwa onyo kwa wananchi, umekusudia kubainisha vitendo vya wananchi vinavyoweza kusababisha dhuluma ili vyepukwe. Aidha utafiti huu umeonyesha umuhimu wa mwananchi katika maendeleo na maongozi mema ya nchi. Isitoshe, mada hii itakuwa ya manufaa makubwa kwa wahakiki na waandishi wa fasihi katika kuyaandika yale ambayo yatakuwa kama mwongozo wa mwananchi aliyewajibika. Mada hii imechaguliwa kubainisha umuhimu wa mwananchi katika kutatua dhuluma zinazomkumba na pia kutoa uelewa wa masuala na mwananchi bora. Kwa hivyo, uhakiki wa tamthilia zinazozungumzia dhuluma unahitajika kwa sababu utapendekeza njia mwafaka za kukabiliana na dhuluma.

1.5 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu umeshughulikia tamthilia tatu ambazo ni *Mstahiki Meya* (2009) ya Timothy Arege, *Kilio cha Haki* (1981) ya Al- Amin Mazrui na *Amezidi* (1995) ya Said Ahmed Mohamed. Tamthilia hizi zinasawiri vyema masuala yanayoathiri jamii katika viwango vya kiuchumi kama vile ukosefu wa kazi, mishahara duni na kupanda kwa gharama ya maisha; viwango vya kijamii kama vile ufisadi na mauaji na katika kiwango cha kisiasa kama vile uongozi mbaya miongoni mwa masuala mengine. Aidha, zinashughulikia suala la dhuluma linaloathiri jamii ya sasa pakubwa hasa katika mataifa ya Afrika Mashariki. Isitoshe, kutokana na usomaji wa awali wa mtafiti, tamthilia hizi zina wahusika wengi wanaolingana na wananchi wa kawaida hivyo kuwezesha kupatikana kwa data inayofaa na ya kutosha.

Japo kuna tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu usawiri wa wahusika katika tanzu mbalimbali za fasihi, utafiti huu uliegemea zaidi upande wa usawiri wa mwananchi kama mdhulumu wa maslahi yake kwa sababu dhuluma kama ufisadi, mauaji na umaskini zinaendelea kuathiri jamii kwa kiasi kikubwa na sampuli hizi tatu yaani tamthilia za *Mstahiki Meya*, *Kilio cha Haki* na *Amezidi* zina data ya kutosha kuhusu jinsi mwananchi wa kawaida anavyojidhulumu. Katika kushughulikia mada hii, utafiti huu umechunguza jinsi mwananchi alivyo mdhulumu wa maslahi yake katika viwango vya kisaikolojia, kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa kusudi la kuonya wananchi kuepukana na mienendo

inayoweza kuwatia katika dhuluma mbalimbali zinazotokana na viwango hivyo.

Utafiti huu umeangalia maudhui yanayotumiwa kusawiri suala la dhuluma ambayo ni: dini, uongozi, utamaduni, taasubi ya kiume, utabaka, umaskini uozo wa kijamii, kazi, siasa na kifo. Aidha, utachunguza jinsi wahusika huathiriwa na dhuluma mbalimbali pamoja na kuchunguza nafasi ya tamthilia hizo katika kukabiliana na suala la mwananchi kama mdhulumu wa maslahi yake na ulivyorejelea changamoto zinazotokea.

Uteuzi wa tamthilia hizi ulifaa madhumuni ya utafiti huu kwa vile zina upekee fulani: zina data ambayo mtafiti alishughulikia. Zinazungumzia suala la dhuluma kwa kuwaangazia wahusika walioathiriwa moja kwa moja. Uhakiki wa tamthilia hizo ulitoa uelewa mpana wa jamii katika kukabiliana na suala la dhuluma kwa kuwa waandishi wa fasihi hutoa malighafi yao kwenye mazingira yao.

1.6 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Waandishi wengi wamejihusisha na masuala yanayohusu dhuluma dhidi ya wanadamu. Watafiti hao wametafiti vitengo mabalimbali vya maisha ya binadamu. Kuna wale ambao wameshughulikia dhuluma za kimapenzi dhidi ya watoto ambao wanaathirika kisaikolojia (Burges, 1979; Lynch na Roberts, 1982), dhuluma dhidi ya wanawake (Momanyi, 1998; Ndungo, 1985 na Kimani, 2003) na wengine wakatafitia dhuluma dhidi ya wanaume (Gitau, 2005 na Laititi, 2004). Tafiti hizi zinahusiana na utafiti huu kwa sababu

zinaangazia suala la dhuluma. Tofauti iliyopo ni kuwa utafiti huu unaangazia mwananchi kama mdhulumu wa maslahi yake ilhali tafiti hizo zingine zinahusisha chanzo cha dhuluma na uongozi mbaya, dini na mila zilizopitwa na wakati.

Ngugi (1972) anaeleza jinsi yeye na Waafrika wenzake nchini Kenya walivyouza jasho lao kwa chini ya shilingi kumi kwa kulima mashamba ya kahawa ya Walowezi na mwishoni mwa juma au mwezi, huwapatia wafanyabiashara pesa hizo ili wapate sukari, unga au nafaka. Kulingana na Ngugi, hawa wafanyakazi ndio waliozalisha mali lakini hawakufaidika kwa vyovyote, mazao ya jasho lao yaliwanufaisha Wahindi wafanyabiashara na Wazungu Walowezi nchini Kenya na hata Uingereza. Kulingana na Ngugi, huenda hali hii ndio iliyosababisha kuundwa kwa vuguvugu la Mau Mau. Maelezo yake Ngugi yanahusiana na mada ya utafiti huu hasa anapoeleza kuhusu dhuluma iliyotokana na malipo duni kwa Waafrika. Aidha, Waafrika waling'amua kuwa kudhulumiwa kwao kulitokana na wao wenyewe ndiposa wakaanzisha vuguvugu la Mau Mau ili kujikomboa.Vilevile, Ngugi anahusisha mfumo wa elimu ya kikoloni na shida nyingi kwa vijana Waafrika waliopata fursa ya kwenda shule. Anaangazia kujichukia kwa Waafrika kama athari iliyotokana na kupata maarifa ya elimu ya kikoloni. Kulikuwapo na ubaguzi wa rangi katika shule na katika matumizi ya vifaa vya kufunzia. Mfumo huu wa elimu ulionyesha kutokuwepo na usawa na uliendeleza fikra za utumwa. Maelezo haya yanatofautiana na utafiti huu kwa kuwa Ngugi anasawiri mfumo

wa elimu ya kikoloni kama chanzo cha shida zilizomkumba Mwafrika bila kuonyesha jinsi Mwafrika alivyochangia dhuluma dhidi yake. Hili ndilo pengo utafiti huu unapania kuziba kwa kuonyesha jinsi Mwafrika kama mwananchi wa kawaida anavyochangia dhuluma dhidi yake.

Katika insha yake ya *The Novelist as a Teacher* katika *Morning yet on Creation Day*, Achebe (1975) anaonyesha ukweli kuhusu jinsi utamaduni wa Mwafrika umesambaratishwa na ukoloni wa Uingereza. Kazi zake kama vile *Things Fall Apart* zilikusudiwa kuondoa kasumba iliyoshikiliwa na Wazungu kuwa Waafrika hawajastaarabika. Achebe ameeleza jinsi Waafrika waliamini kasumba hiyo na kuanza kuiga tamaduni za Wazungu zinazochukuliwa kuwa bora zaidi. Kwa hivyo, Achebe analenga kuwafunza wasomaji Waafrika na Wazungu kuenzi utamaduni wa Kiafrika na kuisaidia jamii yake kujiamini. Mtazamo huu wa Achebe unahusiana na utafiti huu kwa vile unaonyesha jinsi Mwafrika (mwananchi) anavyoshawishika haraka na kuupenda utamaduni wa kigeni ambao unaweza kumdhulumu. Tofauti ni kuwa, Achebe hakumshirikisha mwananchi moja kwa moja kama mdhulumu wa maslahi yake kupitia ukengeushi bali anauona ukoloni kama chanzo cha kukengeuka kwa Mwafrika.

Shaaban Robert (2003) anaona kuwa uaminifu na kutenda haki ni nuru ya maisha bora kwa mwanadamu hapo baadaye. Dhamiri hii inajidhihirisha katika

insha yake ya *Umri* anaposema, “Milango ya nyuma ya kufikia bahati ilikuwa mingi lakini haikunishawishi hata kidogo” (Shaaban, 2003: 2).

Suala hili linajitokeza hata katika jamii za Kiafrika za siku hizi, kwani watu wengi hutumia milango ya nyuma katika kufikia mafanikio yao. Shaaban Robert anaeleza kuwa dhuluma na uonevu vimekuwa ni vipingamizi vikubwa katika mafanikio ya mtu ya kila siku na ni ukuta katika maendeleo ya kibinafsi na ya jamii kwa jumla. Ili jamii iweze kuondokana na hali hii, ni lazima iungane pamoja na kupinga dhuluma na uonevu. Uhakiki huu unahusiana na mada ya utafiti kwa sababu unaangazia dhuluma na madhara yake. Tofauti iliyoko ni kule kutomhusisha mwanachi moja kwa moja na dhuluma na maonevu anayokumbana nayo katika maisha yake.

Gibbe (1979) anaeleza kuwa fasihi ina majukumu ya kuelimisha na kusisimua. Katika kuelimisha, ina jukumu la kuichora jamii kama ilivyo. Fasihi hujaribu kuyamulika matatizo yanayoisonga na kuinyonya jamii. Fasihi inapaswa kuwafungua watu macho iufichue uchafu uliojaa katika jamii. Wakandamizaji wafichuliwe na wanaokandamizwa wapewe mwongozo sahihi waitambue hali yao yenye nguvu ya kupambana na wanaowaangamiza. Utafiti huu unaangazia ukandamizaji unaotekelezwa kwa mwananchi na mchango wake katika kuendeleza ukandamizaji huo dhidi yake bila kusahau nafasi aliyonayo katika kupunguza au kukomesha ukandamizaji huo. Zaidi ni kuwa, ili fasihi iwe na manufaa, ina jukumu la kukosoa na kuiongoza jamii katika lengo lake la kukabiliana na maovu yaliyojaa katika jamii husika. Utafiti huu unakusudia

kuonyesha kuwa ni jukumu la kila mwanajamii kuwajibika katika kuimarisha maisha ya jamii bali si wachache ambao hutwikwa jukumu hilo na mambo yakienda mrama, husingiziwa.

Burges (1979) anaeleza kuwa watoto wamekuwa wakidhulumiwa na wazazi wao na asasi mbalimbali za kijamii. Utafiti wake ulibaini kuwa watoto walidhulumiwa kwa kuchapwa, kutusiwa na kunyimwa hata mahitaji ya kimsingi kama vile chakula. Anaonyesha kuwa watoto wanastahili kustarehe, wahisi upendo na usalama wakiwa miongoni mwa watu wanaowaamini. Kauli hii itafaidi utafiti huu kwa sababu asasi kama vile ndoa inatokana na wananchi, hivyo basi utafiti huu utafaragua matendo ya watoto kama wananchi ambayo yanasababisha dhuluma dhidi yao. Lynch na Roberts (1982), wanaonyesha kuwa dhuluma zina athari nyingi katika maisha ya watoto. Wanaeleza kuwa ingawa mtoto anaonekana kuwa msahaulifu wa matukio fulani, hukumbuka zaidi vitendo vya dhuluma. Maelezo haya ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu yanadokeza athari za dhuluma kwa mwananchi.

Ngugi (1981) anaona kuna umuhimu wa Waandishi wa Kiafrika kuandika kuhusu masuala yanayowaathiri walio wengi katika jamii na wajitenge kutoka ushawishi wa walio mamlakani na mabepari. Walio wengi anaowarejelea Ngugi ni wananchi ambao wamenyanyaswa na mabepari. Maelezo yake Ngugi ni muhimu kwa utafiti huu kwa vile yanadokeza kuwa wananchi wanaathirika mikononi mwa viongozi na walio na ushawishi mkubwa kiuchumi. Hata hivyo,

Ngugi hatoi suluhu kwa matatizo yanayowakumba wananchi wala hawasawiri wananchi kama chanzo cha matatizo yao ila tu anawahimizia waandishi wayaangazie matatizo hayo. Pengo la kutowashirikisha wananchi kama chanzo cha shida zao ndilo utafiti huu unapania kuliziba.

Ndungo (1985) alitafiti mabadiliko ya taswira ya mwanamke katika nyakati mbalimbali za kihistoria kulingana na mabadiliko katika mazingira yake. Alichunguza hali ya mwanamke kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya uhuru. Kutokana na utafiti wake, picha inayojitokeza ni ya kiumbe duni ambacho kimeshurutishwa na mifumo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kuchukua nafasi ya nyuma baada ya mwanamume. Utafiti huu umetofautiana na wake kwa sababu utawalenga wananchi wote wakiwemo wanawake.

Chacha (1986) akiihakiki Tamthilia ya Ukame anawasawiri baadhi ya wahusika kama wabinafsi. Kwa mfano, Mambo anasababisha kifo cha mamake anapozikwa na mapande ya udongo ndani ya kisima. Mambo anakuwa chanzo cha kifo cha mamake kwa sababu ya kutojenga bwawa la maji licha ya kwamba ni mbunge wa eneo hilo na alipewa pesa za mchango wa ujenzi wa bwawa. Kutokana na ubinafsi, anazitumia pesa hizo kwa mahitaji yake kwa kuwa wanakijiji wa Mbute wamezoea shida zao. Mzee Heri anakumbuka namna watu wa Mbute walivyodanganywa na Mambo. Walichanga pesa za mradi wa maji lakini hakuwajengea. Kifo cha mamake Mambo kinamfanya awe mnyenyekevu na mwenye utu. Janga linalompata Mosi (mamake Mambo)

limesababishwa moja kwa moja na ulafi wa Mambo (Wafula, 1999). Maelezo haya yanachangia katika utafiti huu kwa vile yanabainisha ubinafsi kama njia mojawapo ya mwananchi wa kawaida kujidhulumu. Mwandishi anadhamiria kutuonyesha hali inayowakumba watu wenye tamaa na ubinafsi kama Mambo.

Momanyi (1998) anaeleza kuwa dini imetumiwa kuhalalisha ubwana na utwana mbali na kuainisha majukumu ya mwanamume. Chini ya kivuli cha dini ya Kiislamu, itikadi na desturi za Waswahili zinaweza kuainishwa hasa zile zinazomwathiri mwanamke. Utafiti wa Momanyi unaingiliana na utafiti huu kwa vile tafiti zote zinaangazia masuala ya dhuluma. Tofauti iliyopo ni kuwa Momanyi anashughulikia dhuluma dhidi ya mwanamke ilhali utafiti huu unaangazia dhuluma dhidi ya mwananchi akiwemo mwanamke. Pia, amehusisha chanzo cha dhuluma na dini ya Kiislamu ilhali utafiti huu unapania kuonyesha chanzo cha dhuluma kwa mwananchi kuwa mwananchi mwenyewe.

Akiihakiki *Tamthilia ya Hatia* yake Penina Mlama, Wafula (1999) anaeleza jinsi machafuko yanazuka ambapo vikundi vya wanakijiji vinavyotetea pande zinazopingana vinashambuliana. Mapigano na majeraha yanakuwa makubwa. Katikati ya mapigano haya, Cheja anaanza kupiga nduru, akiungama kwamba hakutungwa mimba na Sembuli wala Mkami. Anawaeleza wanakijiji yote yaliyompata hata akadanganywa na Juma kumsingizia Sembuli. Wanakijiji wanagundua shida aliyowazushia Cheja na kuanza kuyatibu madonda

aliyosababisha. Katika uhakiki huu Cheja amejisababishia dhuluma kisaikolojia anaposababisha majeraha makubwa kati ya vikundi vya wanakijiji. Uhakiki huu ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu unadokeza uongo au kudanganywa kama njia mojawapo mwananchi anaweza kutumia kujidhulumu. Aidha, katika *Tamthilia ya Marejeo* ya Chacha Nyaigoti Chacha, Wafula anaeleza kuwa ijapokuwa Ulaya imeonyesha kuwa katili kwa kurutubisha ubinafsi na kuchochea mgawanyiko na vita katika nchi za bara la Afrika, mtunzi hana tashwishi kuwa Mwafrika amejisababishia baadhi ya matatizo yake. Mtazamo huu unaoana na suala la utafiti ambalo ni mwananchi (Mwafrika) kama mdhulumu wa maslahi yake hasa katika nchi zinazoendelea.

Wafula (1999) akiihakiki tamthilia ya *Uasi* (1980) yake Jay Kitsao, anabainisha dhuluma dhidi ya mtoto wa kike inayotokana na desturi za Kigiriama. Desturi hizi ziliwaruhusu wazee matajiri kuwaoa wasichana ‘wabichi’ waliopaswa kuwa mabinti zao. Tabia hii inamdhalilisha mwanamke daima mbele ya mwanamume. Uhakiki huu unafaa utafiti huu kwa vile unamwangazia mtoto wa kike ambaye ni mwananchi. Tofauti iliyopo ni kuwa, chanzo cha dhuluma dhidi ya mtoto wa kike imehusishwa na desturi mbaya ya Kigiriama ilhali utafiti huu unapania kumsawiri mwananchi kama chanzo cha dhuluma anazokumbana nazo.

Kimani (2003) akitafiti kuhusu suala la dhuluma dhidi ya wanawake, anabainisha kwamba mwanamke anakabiliwa na dhuluma za aina nyingi kutoka kwa mwanamume. Ndoa na dini ni baadhi ya asasi za kijamii

zinazotumiwa katika kuwadhulumu wanawake. Utafiti wake Kimani ni muhimu katika utafiti huu kwa vile unadokeza baadhi ya asasi zinazosababisha dhuluma ambazo zitafaraguliwa kubaini jinsi mwananchi anavyozitumia kujidhulumu.

Laititi (2004) amefanya utafiti juu ya unyanyasaji unaofanyiwa wanaume ambao wamestaafishwa mapema. Ana maoni kuwa visa vya wake kuwanyanyasa waume wao vimeongezeka. Amebainisha kuwa baadhi ya wanaume waliofutwa kazi hutumikishwa na wake zao ambao wanachukulia kuwa mwanamume kukosa uwezo wa kiuchumi ni sawa na kushushwa hadhi kama kiongozi wa nyumba.

Gitau (2005) katika utafiti wake juu ya unyanyasaji wa mwanamume katika fasihi andishi ya Kiswahili anaeleza kuwa, wanaume hupitia unyanyasaji wa aina mbalimbali kutokana na mahusiano yao na wanawake na wanaume wengine. Anafafanua jinsi wanaume wanaishia kudhulumiwa kwa sababu ya kutazamiwa na wanajamii kutekeleza majukumu kama vile kutunza familia ilivyoamriwa na dini. Utafiti wa Gitau unatofautiana na utafiti huu kwa sababu umeshughulikia dini kama chanzo cha dhuluma dhidi ya mwanamume ilhali utafiti huu unalenga kumsawiri mwananchi kama chanzo cha dhuluma dhidi yake. Isitoshe, utafiti huu unamlenga mwananchi kwa jumla bali si mwanamume tu inavyojitokeza katika utafiti wa Gitau.

Nangira na Rapando (2005) katika uhakiki wao wa *Tamthilia ya Kifo Kisimani* ya Kithaka Wa Mberia wanaeleza kuwa, watu wanapokosa kufika katika mkutano wa Bokono, tunapata hisia kuwa watu wamechoka na uongozi mbaya lakini wanaogopa kujitokeza hadharani. Kauli hii ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu inadokeza jinsi watu (wananchi) wanavojidhulumu kwa kutojitokeza waziwazi kupinga dhuluma dhidi yao. Wanaendelea kufafanunua kuwa, Bokono hapati kutanabahi kuwa hali ya hatari inanukia. Amezibwa macho na washauri wake ili asione kuwa anawadhulumu watu. Hajui kuwa wakati ambapo watu wananyimwa haki zao, hali ya kutoridhika huzuka. Watu wanapokosa kuridhika, maasi mengi hujitokeza. Bokono kama mwananchi anajidhulumu anaposhikwa na umma kwa kuidhulumu kwa sababu ya kutojua, kujaa majisifu na tamaa. Kitendo cha Gege (mwananchi) cha kumuua Mwelusi (mwananchi mwenzake na ndugu yake) ni kuendeleza utawala dhalimu wa viongozi walioko mamlakani. Utawala huu dhalimu unasaidiwa kunawiri kupitia vibaraka kama vile Batu, Zigu, Talui na Mweke ambao wanawakilisha wananchi katika utafiti huu.

Ng'etich (2011) anaangazia dini kama chombo cha kuwadhulumu waumini. Anasema kuwa shetani amelaumiwa kwa sababu ya makosa hata yale yanayosababishwa na mwanadamu. Shetani analaumiwa kwa kusababisha dhiki, wizi, unyang'anyi na unyanyasaji. Matatizo haya yote yanasababishwa na wanadamu wengine lakini lawama zote zinamwendea shetani. Maelezo yake Ng'etich yanaingiliana na utafiti huu kwa sababu yanaelekeza katika

matendo ya Waumini ambao ni wananchi yanayosababisha dhuluma. Tofauti ni kuwa Ng'etich anaihusisha dini na matatizo yanayowakumba waumini ilhali utafiti huu unalenga kumsawiri mwananchi kama chanzo cha matatizo yake. Pia, Ng'etich ameshughulikia dhuluma dhidi ya waumini wa dini ya Kikristo ilhali utafiti huu unalenga wananchi kwa jumla wakiwemo Wakristo.

Aidha Ng'etich anafafanua jinsi dini imetumiwa kusisitiza ubinafsi ili kuwatenganisha waumini na kuendelea kuwatawala. Mtazamo huu una umuhimu katika utafiti huu kwa vile unadokeza njia mojawapo anayoweza kuitumia muumini ambaye ni mwananchi katika kujidhulumu. Akiihakiki tamthilia ya *Nitaolewa Nikipenda* yao Ngugi Wa Thiong'o na Ngugi Wa Mirii, Ng'etich anaeleza jinsi watu maskini wanaonekana kuwa wenye dhambi. Mtu anastahili kuridhika na atosheke na baraka aliyopata kutoka kwa Mungu. Hata hivyo, umaskini na njaa husababishwa na matajiri na wengine wao ni Wakristo. Uhakiki huu utafaa utafiti huu kwa kuangazia umaskini kama mojawapo ya dhuluma inayomkumba mwananchi. Isitoshe, utafiti huu utafaragua matendo ya mwananchi ambayo yanasababisha umasikini tofauti na mtazamo wa Ng'etich kuwa umaskini husababishwa na wakristo matajiri. Vilevile, Ng'etich anadokeza sababu za dhuluma miongoni mwa waumini kuwa: kuhusisha Mungu na umaskini, ustahimilivu wa dhuluma kuhusishwa na wokovu, matumizi ya ushuhuda, ubinafsi, kutoa ahadi nyingi zisizotimia, utamaduni, vitisho, kutumia nafasi ya uongozi kidhalimu, ujanja na unafiki miongoni mwa sababu nyingine. Sababu hizi zitasaidia katika utafiti huu kwa

kuwa baadhi yazo zitafaraguliwa ili kumsawiri mwananchi kama mdhulumu wa maslahi yake.

Udurusu huu wa maandishi ni muhimu kwa sababu umeonyesha pengo jinsi waandishi wengi hawajamshughulikia mwananchi kama chanzo cha matatizo yake. Wale ambao wanakaribia kufanya hivyo, wanaonyesha kuwa dhuluma dhidi ya mwananchi zinatokana na umaskini, viongozi na uongozi mbaya, dini na mila zilizopitwa na wakati. Udurusu huu wa maandishi umeonyesha pengo lililoachwa na waandishi ambalo ni kutomsawiri mwananchi wa kawaida kama chanzo cha dhuluma zinazomkumba.

1.7 MISINGI YA NADHARIA

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa iliyoasisiwa na Maxim Gorki na Udenguzi yake Jacques Derrida. Nadharia hizi zina uwezo wa kuelekeza kwa njia ya kitaalamu. Nadharia ya Udenguzi iliweza kufaragua matendo ya mwananchi ili kuonyesha jinsi yanavyoweza au yanasababisha dhuluma dhidi yake na nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa iliweza kuonyesha yale ambayo anatakikana kuyafanya mwananchi ili kuzuia dhuluma dhidi yake.

1.7.1 NADHARIA YA UHALISIA WA KIJAMAA.

Neno “uhalisia” lilitumiwa kwa mara ya kwanza huko Ufaransa katika mwaka wa 1850 ili kueleza kazi za sanaa zilizojikita katika kusawiri ulimwengu kama ulivyo wala sio kama unavyofikiriwa kuwa (Hegel, 1971). Uhalisia huzingatia

namna ukweli unavyosawiriwa katika nyakati mbalimbali. Kazi hii ya uhalisia iliwekewa msingi na mwanafalsafa Hegel katika kitabu chake *Aesthetics.* Mtaalamu huyu alipendekeza matumizi ya neno hili kuelezea kazi ya sanaa iliyo na wahusika ambao matendo yao yanachochewa na hali ya kisaikolojia iliyowazunguka. Wahusika na wahakiki wengi waliotumia nadharia ya uhalisia waliamini ya kwamba dhima ya mwandishi ni kuonyesha ukweli jinsi ulivyo na pia kuweza kusuta maovu ya kijamii. Hapa mwandishi anapaswa kutoa picha ya jamii na hivyo kuwa kama kurunzi ya jamii na kutumia kipawa chake kuchora wahusika na mazingira yanayokubalika katika jamii ya wakati wake kwa sababu mazingira haya huwa na uhalisi unaoaminika. Kutokana na kusakini kwa ubepari katika sehemu nyingi za Ulaya ambazo zilikuwa kitovu cha uhalisia, wachochole walishinikizwa katika kuzalisha mali lakini faida yote iliwaendea mabwenyenye jambo lililosababisha mgongano kati ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa. Mgongano huu hutokea kwa sababu kila mara kuna tabaka la wanaonyonya na tabaka la wanaonyonywa. Hivyo inabidi kuwa na mapinduzi dhidi ya mifumo ya kuzalisha mali inayohimili unyonyaji. Mapinduzi yanayotokea baadaye yanaongeza tumaini la ujenzi na uimarishaji wa jamii inayozingatia usawa (Eagleton, 1976). Mkinzano kati ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa ndio uliosababisha kuzuka kwa nadharia ya uhalisia wa kijamaa pale wanajamii walipong'amua kwamba mahitaji ya jamii yanatawaliwa na mahitaji ya kiuchumi wala si fikra au majaaliwa (Khaemba, 1999). Kutokana na maelezo haya, nadharia ya uhalisia wa kijamaa ilitumika kama kifaa cha kuleta mabadliko katika uhalisi ulioko na kunuia kuonyesha

jamii katika uyakinifu wake na hatua zake za kimabadiliko. Aidha nadharia ya uhalisia wa kijamaa ilikusudia kuleta usawa hivyo kuathiri uhalisia wa maisha.

Msokile (1993) anaeleza kuwa uhalisia wa kijamaa ulianza rasmi wakati wa kipindi maalum cha historia hasa baada ya mapinduzi ya kijamaa ya Urusi ya 1917. Arvon (1973) anasema kuwa mojawapo ya kazi za Gorky kama vile *Mother* (1906) iliweka misingi madhubuti ya kwanza ya fasihi halisia, unyama na mapambano baina ya matabaka yalionekana wazi. Uhalisia wa kijamaa huzingatia kwa undani historia ya jamii na mivutano yake. Sifa kubwa ya uhalisia wa kijamaa ni kutetea masilahi ya wafanya kazi na kuwapa matumaini ya siku za usoni. Kwa mujibu wa Maxim Gorky (1975), mmojawapo wa waasisi wa uhalisia wa kijamaa, mambo yote yanayotamanika ulimwenguni yameumbwa na kuelezwa na binadamu. Anaendelea kufafanua kuwa, ni jambo la kuhuzunisha kuwa mtu amezaa na kuendeleza dhuluma dhidi ya binadamu mwenzake (Wafula na Njogu, 2007). Uhalisia wa kifasihi unaashiria uwezo wa kusawiri au kueleza hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha katika muktadha wa jamii inayozungumziwa; kuwa na wahusika halisia wanaopatikana katika hali halisi iliyofungamana na masimulizi na matukio ya kihistoria. Basi, mwanafasihi hana budi kuzingatia historia ya jamii anayoizungumzia na kuonyesha mivutano ya kitabaka kama sehemu ya maisha. Gorky anashikilia kwamba maisha ni matendo na maisha ni uumbaji. Juu ya haya, lengo la kuishi ni kukuza na kusambaza vipawa vitakavyomwezesha mtu kupigana na kushinda pingamizi dhidi yake.

Madhumuni ya maisha pia ni kudumisha afya ya mtu, kumwezesha kuishi kwa furaha, afurahie uwezo wake wa kuidhibiti na kuitawala dunia. Naye Lukacs (1978) anasema kwamba uhalisia wa kijamaa kwa kawaida humtaka mwandishi asawiri uhalisi wa ukweli kihistoria. Senkoro (1987) anaeleza kuwa uhalisia wa kijamaa huhakikisha kuwa uwezo wa kila mtu hujengwa, huimarishwa na kukidhiwa kwa kusudi kubwa la kuyashinda kabisa mazingira ya mtu huyu kwa manufaa ya jamii nzima. Ni tapo lenye kumjenga mtu mwenye furaha na amani, ni tapo la watu wanaobadilisha na kujenga upya ulimwengu. Lengo la uhalisia wa kijamaa ni kuhakikisha ushindi dhidi ya mazingira makali na kupambana na udhalimu wa aina yoyote. Kutokana na ufafanuzi huu, utafiti huu ulitathmini mwananchi kama mdhulumu wa maslahi yake kwa kurejelea tamthilia ya *Mstahiki Meya*, *Kilio cha Haki* na *Amezidi* kwa kuangazia mihimili ifuatayo:

1. Wahusika wa kimaendeleo: Hawa ni wahusika wanaonuia kuipindua na kubadilisha hali yao ya maisha. Ni wahusika wenye nia ya kumiliki njia kuu za kuzalisha mali katika jamii yao. Mhimili huu ni muhimu katika kubainisha njia mbalimbali wanazoweza kuzitumia wananchi katika kujikomboa kutokana na dhuluma zinazowakumba.
2. Pamoja na kusawiri matukio kihistoria, wahusika hutekeleza matendo yao kitabaka. La mno ni kwamba tabaka la wanyonge huweka juhudi kujipa mamlaka na nguvu za kiuchumi. Mhimili huu utasaidia katika kuonyesha mbinu zinazotumiwa na tabaka linalokandamiza katika

kuendeleza ukandamizaji na yale matendo ya tabaka linalokandamizwa ambayo yanaendeleza ukandamizaji.

3. Binadamu huonyeshwa kiuyakinifu. Wahusika ambao hutumiwa kama vipaza-sauti vya watunzi hupuliziwa uhai mathalani wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu unaofahamikiwa nao. Mhimili huu ni muhimu katika kuonyesha yale ambayo wananchi wanatakiwa kuyafanya ili kujiokoa kutokana na dhuluma kwa kuzingatia mawazo ya mhusika kipaza- sauti.

Mihimili ya nadharia ya uhalisia wa kijamaa inafaa utafiti huu kwa sababu ilitumiwa kupendekeza namna ya kutatua dhuluma katika jamii ili kuunda jamii mpya itakayokuwa bora zaidi na kuihamasisha na kuizindua umma kuchochea mabadiliko.

1.7.2 NADHARIA YA UDENGUZI

Udenguzi ni nadharia iliyoasisiwa na Mfaransa Jacques Derrida (1967). Alianza kutumia neno ‘deconstruction’ alipokuwa akijadili athari za kuelewa lugha kama maandishi bali si usemi (Derrida, 1976). Anasema kuwa, mtazamo ambao umekubalika kuhusu ulimwengu na lugha ukichunguzwa kwa kuangazia matumizi ya ishara tunazozifahamu, taswira itakayojitokeza ni tofauti na yale tunayoyafahamu. Kulingana naye, kile ambacho kimejulikana kutokana na mazoea hakifahamiki kwa sababu ya kuzoeleka tu. Kitu hicho kikiwekwa katika mchakato wa kukifahamu, itabainika kuwa maelezo kukihusu ni potovu. Anaeleza zaidi kuwa udenguzi huhusu ukinzani wa jozi za

maneno. Kuhusu jozi hizo ni kuwa jamii za Kimagharibi zimejenga upendeleo wa wazi pale neno moja katika jozi husika daima linawakilisha utukufu wa kile kinachopaniwa kufikiwa kama kitu asilia huku dhana ya pili ya jozi hiyo ikiangaliwa kama ghushi isiyo safi na ya daraja ya chini. Wanafilosofia wa awali kama anavyodokeza Derrida, waliuona ulimwengu kama unaojengwa na vitu vya kimsingi na vinavyostahili kupewa kipau mbele kama vilivyo safi, vya wastani na vilivyokamilika huku upande wa pili wa jozi nao ukifafanuliwa na vitu vilivyotandwa na utata na vyenye doa. Kwa sababu hiyo, usanifu wa hoja katika nchi za kimagharibi una tabia ya kuviona vitu na hali mbalimbali kwa namna ya upendeleo. Pamoja na mgao huo ambao wanafilosofia wa kijadi walipania kuujenga, udenguzi hulenga kufutilia mbali mipaka na kuonyesha kuwa jozi za maneno ni mfano wa sarafu moja yenye pande mbili. Ili kuifahamu matini, Derrida (1976:50) anasema:

> Kusoma kwa makini kwa matini huleta vinyume ambavyo havina mwisho. Hata hivyo, msomaji hatakiwi kukoma kusoma bali anapaswa kuendelea kusoma na kung'amua vinyume vingi kadri ya uwezo wake. Aidha kile kinachorejelewa huwa ni ishara ambayo aghalabu huendelea kubadilika na kuwa kitu kingine, yaani kinachorejelewa pia hurejelea kitu kingine na azimio la udenguzi ni kuainisha matini kwa njia ya kisanaa ili kuonyesha kile hakifahamiki (Tafsiri yangu).

Haja kuu ya udenguzi ni kuonyesha kuwa ile maana inayochukuliwa kuwa halisi yaweza kuwa tepetevu. Zoezi la mhakiki yeyote kujaribu kufasiri maana ya matini au kazi haliwezi kufaulu kikamilifu kwa sababu mitazamo huwa tofauti na isiyoweza kujisimamia, kujitawala wala kujitegemea. Aidha, udenguzi hujaribu kutofungia nje maarifa zaidi na unapoendelezwa hujidengua katika harakati ya kutafuta msingi wake na furaha ya kisicho na mwisho. Hata

hivyo, kuna madai kwamba Derrida alikuwa anaendeleza fikra za Hegel, Freud na Heidegger. Wanafalsafa hao walidai kuwa lugha kama ishara ina uwezo wa kujifafanua tukiitazama kwa undani.

Udenguzi ni nadharia inayoangazia mabadiliko yanayomwezesha msomaji kuumbua au kubomoa muundo wa matini na kazi ya fasihi ili kuifasiri vingine. Kwa mfano, vitu vilivyozoeleka huchukuliwa kufahamika sawasawa lakini uchunguzi wa vitu hivyo ukifanywa, itabainika kuwa uelewa wake ni potovu kwa sababbu kile kilichozoeleka huwa ishara ya kitu kingine ambacho pia huwa ishara ya kitu tofauti na ishara hizi huendelea kujitokeza bila kukoma, hapa dhana ya maana kuwa telezi hujitokeza. Chimerah na Njogu (1999) wanaeleza kwamba nadharia ya udenguzi huzama zaidi katika kuchambua matini kwa mtazamo badalia unaomulika pembe zote za maana yake. Wanaeleza zaidi ya kwamba udenguzi huhusisha juhudi za kuelewa muundo wa lugha kwa kuipondaponda, kuipepetapepeta na kuipeperusha ili kuona ikiwa panatokea vidato vya kinyume.

Wafula na Njogu (2007) wanaeleza kuwa kila usomaji wa kazi ya sanaa, hata na mhakiki yule yule ni toleo jipya la kazi hiyo. Kwamba, hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi kwa sababu dhana huendelea kubadilika na kuahirisha maana yake ya mwisho.

Kamuf (1991) anasema kuwa pengine fasiri nyingine isiyotiliwa mkazo ndiyo huweza kuwa ya kweli na bayana zaidi. Hii ina maana kuwa, haiwezekani kufasiri matini kwa maana moja tu. Matini ya fasihi huwa na maana

mbalimbali ambazo hutofautiana. Gasche (1986) anasema kuwa maana inayoonekana kuwa imara na ya kimantiki zaidi huweza kuwa tepetevu na isiyo na mashiko. Culler (1982) anaeleza kuwa maana inayohusishwa na kazi ya sanaa hujumuisha kile kilichoachwa nje, kilichopuuzwa au kilichonyamazishwa. Kulingana naye, udenguzi hutilia maanani uchambuzi wa makini wa matini kwa kutazama yanavyohusiana na matini nyingine.

Gale (2003) anaonyesha kuwa nadharia ya udenguzi inachukulia kwamba matini ya fasihi huwa na maana mbalimbali zinazokinzana. Kwamba kazi ya fasihi huweza kufasiriwa kwa zaidi ya njia moja. Critchley (1992) udenguzi hupendekeza mitazamo anuwai na kuhusisha wazi jambo ambalo hudokeza udenguzi kama dhana ya kimaadili.

Mbinu kuu na muhimu inayotumiwa na wanaudenguzi ni ukinzani wa jozi za maneno hasa kuwa jamii za kimagharibi zimejenga upendeleo wa wazi pale neno moja katika jozi husika daima linawakilisha utukufu au kile kinachopaniwa kufikiwa kama kitu adili huku dhana ya pili ya jozi hiyo hiyo ikiangaliwa kama ghushi, isiyo safi na ya daraja ya chini. Aidha kupitia uchanganuzi makini wa lugha ya matini, wadenguzi hudhihirisha ukinzani na utepetevu wa matini hizo. Hili ndilo linalowapelekea wadenguzi kudai kuwa matini hujiumbua na kujikomboa yenyewe wala sio wao wanafanya hivyo. Wanavyodai, hii ni sifa ya azali na iliyomo katika lugha kwani tangu jadi lugha imejengeka kama mfumo wenye ukinzani na unaotofautisha maana (Burman na Mclure, 2005).

Kutokana na maelezo haya, tuliweza kutathmini mwananchi kama mdhulumu wa maslahi yake kwa kuangazia mihimili ifuatayo:

1. Hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi. Wahakiki huweza kutoa fasiri tofauti za jambo moja ambazo huweza kukinzana maadam wana ushahidi wa kutosha. Mhimili huu ulionyesha kinaya kwa mwananchi kudai kuwa anadhulumiwa na walio na mamlaka kumbe ni mwananchi anayejidhulumu mwenyewe katika jamii inayopatikana katika tamthilia ya *Mstahiki Meya, Kilio cha Haki* na *Amezidi*.
2. Kazi ya fasihi huwa na maana ya ndani inayopatikana ikifasiriwa kwa makini. Mhimili huu ni muhimu katika kubaini kiishara matendo wayatendayo wananchi kujidhulumu kwa kuangazia tamthilia teule. Vilevile, kuonyesha dhuluma mbalimbali ambazo zimerejelewa kiishara.
3. Kazi ya mhakiki ni kuibua na kujumuisha kile kilichonyamazishwa, kilichopuuzwa na kuachwa nje na wahakiki wengine na hata kisichotiliwa uzito na mwandishi. Yaani, jukumu la mhakiki si kubainisha mambo yaliyoshughulikiwa waziwazi na mwandishi bali kumulika mianya inayojitokeza katika utungo. Mhimili huu ulionyesha matendo ya wananchi ambayo hayatiliwi maanani lakini huwa chanzo cha mateso yao.

Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa ilisaidia katika kubainisha dhuluma anazokumbana nazo mwananchi, jinsi anavyojidhulumu na kupendekeza namna ya kutatua dhuluma hizo ili kuunda jamii mpya na bora zaidi. Kwa

upande mwingine, nadharia ya udenguzi ilifaa utafiti huu katika kuonyesha jinsi waandishi wa tamthilia teule wanavyomfaragua mwananchi ili kuweka wazi nafasi yake katika dhuluma zinazomkumba. Kupitia kwa nadharia hii, mwananchi (mhusika) alionyeshwa kuwa na nia nzuri katika vitendo vyake kisha vikadenguliwa ili kubainisha jinsi vilivyoweza kuendeleza dhuluma dhidi yake.

1. 8 MBINU ZA UTAFITI

1.8. 1 MUUNDO WA UTAFITI

Matokeo ya utafiti yameandikwa kinathari kwa kuzingatia matokeo ya utafiti ya maktabani kutoka vitabu vilivyosomwa.

1. 8.2 MAHALA PA UTAFITI

Utafiti huu umefanywa maktabani. Maktaba zilizotumiwa katika kufanya utafiti huu ni tatu: Maktaba za chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi na Moi nchini Kenya. Maandishi mbalimbali yamedurusiwa maktabani, vikiwemo vitabu vya fasihi vilivyoteuliwa kwa minajili ya mada hii, magazeti, majarida na vitabu vinavyozungumzia dhuluma dhidi ya masilahi ya mwananchi vimesomwa pamoja na utafiti kufanywa kwenye mtandao ili kupata data mwafaka. Aidha, tafiti za awali kuhusu dhuluma dhidi ya wananchi (wahusika) zimesomwa ili kuelewa nadharia, mbinu za kukusanya data, uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti.

1. 8.3 UTEUZI WA SAMPULI

Vitabu vilivyolengwa ni tamthilia tatu: *Mstahiki Meya (2009), Kilio cha Haki (1981)* na *Amezidi (1995)* zilizoandikwa na Timothy Arege, Al-Amin Mazrui na Said Ahmed Mohamed mtawalia. Tamthilia hizi zimeteuliwa kwa njia makusudi kwa sababu ni miongoni mwa kazi za fasihi zinazoangazia masuala ambayo yanapatikana katika nchi za Afrika Mashariki. Wananchi wa nchi hizi wanakumbwa na matatizo mengi yakiwemo magonjwa, njaa, mauaji miongoni mwa matatizo mengi mengineyo. Matatizo haya kwa kiwango kikubwa yamehusishwa na majanga na viongozi lakini utafiti huu unapania kuonyesha jinsi mwananchi alivyo chanzo cha matatizo hayo.

1. 8. 4 UKUSANYAJI WA DATA

Data ya utafiti huu ilikusanywa kutoka tamthilia tatu za Kiswahili za: *Mstahiki Meya* (2009), *Amezidi* (1995) na *Kilio cha Haki* (1981). Mtafiti alisoma tamthilia hizi zote kwa kina na kuyatenga kwa kuyaandika mambo yote yaliyo muhimu kwa utafiti huu katika daftari ili kumwezesha kukamilisha utafiti kwa kupata data iliyotosheleza mahitaji ya utafiti.

1. 8.5 UCHANGANUZI WA DATA

Uchanganuzi uliongozwa na maswali na malengo ya utafiti kuonyesha namna mwananchi ni mdhulumu wa maslahi yake katika tamthilia teule, kuonyesha shida mbalimbali anazojisababishia na mapendekezo ya jinsi ya kukabiliana nazo kutokana na tamthilia teule. Utafiti huu umeongozwa na mihimili ya

nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa na udenguzi kwa kuzingatia tamthilia ya *Mstahiki Meya, Kilio cha Haki* na *Amezidi*.

1.8.6 UWASILISHAJI WA MATOKEO

Matokeo yamewasilishwa kwa njia ya maelezo ambayo yamezingatia malengo ya utafiti ambayo yameonyesha namna mwananchi ni mdhulumu wa maslahi yake mwenyewe, kubainisha shida mbalimbali zinazomkumba mwananchi na kubainisha mapendekezo ya anachotarajiwa kufanya kama mwananchi ili kuboresha maisha yake.

1.9 HITIMISHO

Katika sura hii, vipengele muhimu katika tasnifu vimejadiliwa. Vipengele hivi vimeonyesha namna suala la utafiti lilivyochipuka, malengo na misingi ya nadharia iliyoongoza utafiti, mapitio ya maandishi na mbinu za utafiti zilizotumika. Sura zinazofuata zimejengeka kutokana na sura hii.

SURA YA PILI

2.0 CHANZO CHA DHULUMA KWA MWANANCHI

2.1 UTANGULIZI

Sura ya kwanza ilijadili sababu ya kuchagua mada, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na upeo wa utafiti. Sura hii imeangazia jinsi mwananchi wa kawaida anavyojidhulumu kupitia kwa matendo yake na ufafanuzi kutolewa kwa kuchagua tamthilia teule ambazo ni *Kilio Cha Haki*, *Amezidi*, *Mstahiki Meya* na mitazamo mbalimbali ya wataalam.

Aghalabu, dhuluma hutokana na ubinafsi au ujeuri ambapo mjeuri hasa anapokasirika humpiga mdhulumiwa na hata kumnyang'anya mali yake. Aidha, kuna wanaotumia maneno ili kuwaumiza wengine kwa kuwabandika majina ya kuwatia aibu, kuwatukana au kuwadhihaki kila wakati. Vilevile, kuna wanaoharibu mahusiano kwa kueneza uvumi mbaya kuwahusu wengine na wanaolipiza kisasi; yaani wanageuka kuwa wadhalimu baada ya kudhulumiwa. Aidha, kuna dhuluma zinazotokana na kunyimwa kwa huduma za kimsingi (Gisele, Alyson na Cindi, 2005). Yafuatayo ni baadhi ya mambo ambayo huchangia katika kujidhulumu kwa mwananchi wa kawaida:

2.2 ITIKADI

Itikadi ni mfumo wa mawazo fulani ambayo ni msingi wa mwelekeo fulani wa kichumi au kisiasa (Mavisi, 2007). Kiasilia, maana ya istilahi 'itikadi' inatokana na maandishi ya mwanafalsafa wa Kijerumani Karl marx na mwenzake Friedrich Engels (Abdulla, 2014). Katika uchanganuzi wao wa

kimsingi wa jamii, walifafanua itikadi kama dhana na imani za tabaka tawala katika kipindi maalum. Dhana na imani za tabaka tawala ndizo hutamalaki taratibu za kuunda fikra, mawazo na mielekeo ya wanajamii kwa ujumla. Kwa hivyo, mfumo wote wa fikra za tabaka tawala ndio unajenga itikadi ya jamii fulani. Watawaliwa hukubali hali ya ukengeushi ambayo kwa kawaida wangeasi dhidi yake. Hali hii ya ukengeushi imediriki kuitwa "ung'amuzi potoshi" (Eagleton, 1991). Kwa mfano, fikra na maoni ya wananchi wa kawaida katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki* ni kuwa mzungu ni mtu bora zaidi na hana kasoro katika maamuzi yake. Imani hii inawafanya Waafrika ambao ni wawakilishi wa wananchi wa kawaida wasipinge baadhi ya amri za waajiri wao Wazungu japo zinasababisha dhuluma dhidi yao. Waafrika hasa waliopewa fursa ya kuwaongoza Waafrika wenzao katika shamba la mwajiri Mzungu wanatoa habari jinsi wafanyakazi wenzao walivyo na mbinu wanazoweza kuzitumia kudhibiti 'ushenzi' wao ili wasimsumbue Bwana Delamon. Ushenzi unaorejelewa hapa ni baadhi ya mbinu wanazozitumia wafanyakazi kujinasua kutoka kwa mtego wa dhuluma dhidi yao hasa ule wa malipo duni. Badala ya Zari na Shindo kuwaibia Waafrika wenzao siri ya jinsi ya kupinga dhuluma kutoka kwa Bwana Delamon, wanawazuia wenzao wasipiganie haki zao kutokana na fikra potovu kuwa wenzao ni washenzi. Kwa mfano, Delamon anapomuuliza Zari sababu ya kutowadhibiti wafanyakazi ili wasiandamane anamjibu kuwa:

> Yaani... yaani ni wale... wale viongozi wao tu. Ni yule Lanina tu...yule mwanamke mshenzi... yule... (Mazrui, 1981: 8).

Badala ya Zari kuwatetea wafanyakazi na kuwa mkombozi wao wa kichinichini, anawataja viongozi wao kwa adui yao na kumpa nafasi nzuri ya kukabiliana na juhudi zao za kujikomboa kutokana na dhuluma. Hata kama Zari ni msaidizi wa Bwana Delamon, hafaidiki kwa lolote. Yeye ni chombo cha kufanikisha malengo ya Delamon, kwa hivyo anabakia kuwa mwananchi wa kawaida licha ya kupakwa mafuta ya cheo cha 'usaidizi'. Lakini anaendeleza dhuluma dhidi yake na wananchi wenzake wa kawaida kwa kukubali kutumiwa na Bwana Delamon kupinga maandamano na migomo shambani. Anajiunga na Delamon kwa kukubali hali ya ukengeushi kuwa Waafrika ni washenzi. Aidha, Zari kama mwananchi wa kawaida anadidimiza juhudi za kujikomboa na kuwakomboa wenzake anapojazwa na fikra za taasubi ya kiume. Jambo hili linajitokeza anapomrejelea Lanina kama mwanamke mshenzi. Haoni umuhimu wa juhudi za Lanina za kuwaongoza wenzake kupigania maslahi yao kwa sababu yeye ni mwanamke.

Wafanyakazi kama wananchi wa kawaida wanaendeleza dhuluma dhidi yao kwa kumpa Delamon fursa ya kutumia nguvu zao na kuwanyang'anya ardhi yao kwa gharama ndogo sana inavyobainika kutokana na maneno ya Lanina:

> ...nyinyi hamkuja hapa kwa manufaa yetu
> Hamkuja hapa kwa maendeleo ya nchi yetu.
> Mmekuja kwa maslahi na faida yenu wenyewe.
> Mmekuja kutudhulumu tu
> Kutumia nguvu zetu
> Kutunyanganya ardhi yetu kwa gharama ndogo
> isiyokuwa na thamani (Mazrui, 1981: 13).

Wafanyakazi wanakubali kufanya kazi nyingi bila kulalamika kwa muda kutokana na imani kuwa japo wamelemewa na mzigo wa maisha, ni kwa manufaa yao. Imani na kasumba hii potovu waliojazwa na Bwana Delamon

inawafanya kuwa kimya kwa muda wanapodhulumiwa huku Bwana Delamon akiendelea kutengeneza faida kwa jasho lao. Hata Askari wa kwanza ambaye ni Mwafrika na mwananchi wa kawaida amejazwa fikra za kiitikadi na kukengeuka kuwa Mwafrika ni mpumbavu na hana haki kwa sababu hata akipatiwa hiyo haki hatajua cha kuifanyia. Jambo hili linajitokeza Askari wa kwanza anapompiga Lanina kofi na kusema:

> Wacha upuzi wako huo!
> Haki! Haki! Unapigania kitu ambacho
> hata ukipewa hujui ukifanye nini!
> Mpumbavu wee! (Mazrui, 1981: 14)

Askari kama mwananchi wa kawaida anajidhulumu kwa kupinga juhudi za Lanina za kutetea haki za wafanyakazi wakiwemo askari ambao wanatumiwa visivyo kuwanyayasa Waafrika wenzao. Askari amejazwa fikra kuwa Bwana Delamon ndiye msingi wa kuendeleza uchumi hali ambayo hataki ipingwe japo anajiendeleza mwenyewe huku wananchi wa kawaida wakiumia.

Aidha Shindo na Zari ambao ni Waafrika na wananchi wa kawaida wanashirikiana na Delamon kuwadhulumu Waafrika wenzao kwa imani kuwa Bwana Delamon ana uwezo ambao hawana. Kutokana na sababu hii, wanapotumiwa na Bwana Delamon kwa manufaa yake hawang'amui, ndiposa Shindo anatumiwa kumshawishi Tereki kuwa kiongozi wa chama cha wafanyakazi ambacho lengo lake ni kuyatetea maslahi ya Bwana Delamon badala ya wafanyakazi. Tereki anapomwambia Shindo kuwa anahitaji muda wa kufikiri, Shindo anaongozwa na fikra kuwa Delamon ndiye nguzo ya maendeleo kwa sababu ya tabaka lake la juu na kusema:

> Waafrika wapumbavu sana
> Mzungu huyu anajaribu kumsaidia

na yeye ati anajidai
anataka kufikiria kwanza.
Kufikiria! Kufikiria!
Ana akili gani za kufikiri,
mshenzi yule! (Mazrui, 1981: 19)

Hapa Shindo anamjaza Tereki mawazo ya kiitikadi kuwa Bwana Delamon ana akili nyingi na maamuzi yake hayapaswi kupingwa japo yanawaumiza wananchi wa kawaida. Aidha, Shindo na Zari wanajidhulumu na kuwadhulumu wafanyakazi wenzao kutokana na ubinafsi na wanajaribu juu chini kumjaza Tereki mawazo ya kibinafsi hivyo kuendeleza dhuluma dhidi yao na wafanyakazi wenzao. Mwishowe, Tereki anakubali kuwa kiongozi wa chama kinachoanzishwa na Delamon kwa madhumuni ya kuendeleza utawala wake huku wafanyakazi ambao ni wananchi wa kawaida wakiteseka licha ya kuwa wanachama wa chama cha kuyatetea maslahi yao.

Isitoshe, kitendo cha Shindo, Zari na Tereki kuungana pamoja na kupinga juhudi za ukombozi zinazoongozwa na Lanina ni chanzo cha dhuluma dhidi yao kwa sababu kama baadhi ya wananchi wa kawaida, wanapunguza idadi ya wapiganiaji wa haki za wananchi na wafanyakazi hivyo shinikizo la kufanyiwa haki likionekana kutoka kwa wananchi wachache tu. Pia, pingamizi zao zinaoyesha kuwa wanachokipigania Lanina na wenzake si cha muhimu kwa sababu wenzao hawawaungi mkono na wanakashifu harakati zao. Pili, upinzani na mtazamo wao Shindo, Zari na Tereki kuhusu kutokuwa na haja ya kupigania haki za wananchi wa kawaida vilevile unavunja hamu ya wananchi wengine kupigania haki zao hivyo kupunguza idadi ya wapiganiaji haki. Kwa mfano, mmoja wa wafanyakazi anamuunga mkono Tereki kuwa wameongezwa mshahara na hataki kujipatia shida kwa kufukuzwa kazi baada

ya kugoma. Kile mfanyakazi huyu hajui ni kuwa Tereki anayatetea maslahi yake kutokana na ubinafsi na haoni umuhimu wa kupigania haki za wafanyakazi wenzake. Aidha, mfanyakazi huyu hajui kuwa japo ameongezwa mshahara, muda wa kufanya kazi pia umeongezwa kuliko awali kwa hivyo hakuna nafuu yoyote katika dhuluma dhidi yake. Kwa hivyo, anaendelea kujidhulumu kupitia kwa ujinga wake na kufuata mwelekeo wa Tereki bila kuuhoji kwa sababu yeye ni kiongozi.

Mwengo ambaye ni bwanake Lanina anamshuku Lanina kuwa malaya. Fikra hizi zinatokana na tabia ya Lanina kushirikiana na wenzake wa kiume katika harakati ya kutetea maslahi yao kama wafanyakazi. Jambo hili linajitokeza Lanina anaposema:

> **Lanina**: Na wewe unasikiliza maneno ya watu Mwengo?
> Ndiyo, watu wanasema mengi.Watu wanasema
> mimi ni malaya kwa sababu nashirikiana na
> wafanyakazi wenzangu wanaume! Wewe pia
> unaamini kuwa mimi malaya Mwengo? (Mazrui, 1981: 33).

Maelezo haya yanadokeza itikadi waliyonayo watu kuwa mwanamke yeyote anayeshirikiana na wanaume ni malaya na hizi ni fikra potovu ambazo hudidimiza ukombozi wa mwanamke. Bila shaka watu anaowarejelea Lanina ni wananchi wa kawaida wakiwemo wafanyakazi. Watu hawa wanaendeleza dhuluma dhidi yao wanapomvunja Lanina moyo kwa kusema yeye ni malaya katika harakati ya kuwatetea na kupinga dhuluma dhidi yao. Isitoshe, Mwengo akiongozwa na taasubi ya kiume haoni umuhimu wa harakati za Lanina za kupigania haki. Anataka Lanina abaki nyumbani kuchunga na kutunza watoto kwani hilo ndilo jukumu lake kama mwanamke kulingana na utamaduni na

mwanamke yeyote anayeshirikiana na wanaume ni malaya. Kulingana na Mwengo, shughuli za Lanina za kupigania haki zinafaa kufanywa na mwanamume bali si mwanamke. Hafahamu kuwa juhudi za Lanina za kutetea maslahi ya wananchi zitamfaidi yeye na kuzipinga ni sawa na kuendeleza dhuluma dhidi ya mwanamke na wananchi wengine wa kawaida.

Katika *Tamthilia ya Mstahiki Meya* (Arege, 2009), swala la itikadi kama chanzo cha dhuluma linajitokeza kutokana na jinsi wananchi wa kawaida wanavyomwona Meya kuwa mtu wa hadhi ya juu sana jambo linalompa kiburi. Kwa hivyo, wananchi wa kawaida wanajifanya duni mbele ya Meya na kumpa fursa ya kuwadhulumu atakavyo. Mradi yeye ni kiongozi, wananchi wa kawaida wanamrejelea na kumshughulikia kwa njia ambayo inaonyesha ana mamlaka na ni muhimu kuliko vyumbe wote. Kwa mfano, Mstahiki Meya anakasirika anapoletewa mayai madogo kinyume na ilivyokuwa kawaida. Isitoshe, anapochomwa na chai, anamlimbikizia lawama Dida kuwa ametumwa kumchoma na chai. Hata Dida anaonyesha athari ya itikadi anapomhudumia kwa unyenyekevu wa kumuabudu. Dida anakubali kuwa yeye ndiye mwenye makosa na kuomba msamaha hata kama Meya ndiye mwenye makosa:

> **Meya:** Sina haja na hadithi zako za pole. Amekutuma nani kunichoma kwa chai mapema hii? Una njama gani?
>
> **Dida:** (*Anagundua kuna chai iliyomwagikia kiti na meza*.) Samahani sana Mstahiki baba Meya. Nimetia chai chupani kama kawaida. (*Huku akipangusa samani na koti la Meya*.) Nasikitaka kuona haya Mstahiki. Pole!
>
> **Meya:** (*Bado akiwa amemtazama*.) Hizo pole haziondoi wala

kufuta chochote hata ukizitema nyingi kiasi gani.

Dida: (*Kwa unyenyekevu*.) Ndiyo Mstahiki!

Meya: (*Akiashiria sahanini*.) Je, na haya mayai?

Dida: Yana nini baba?

Meya: (*Kwa ukali)* Wewe huoni si kama zamani?

Dida: Naona baba.

Meya: Sababu?

Dida: Mwenye kuyaleta Mstahiki Meya anasema hali zimebadilika. Kuku wanataga madogo hivi.

Meya: (*Kwa dharau*) Kisha bado unamruhusu kunipunja kwa kuleta viyai kiasi hiki? Eeh? (Arege, 2009: 9).

Mazungumzo haya kati ya Meya na Dida yanabainisha jinsi Dida kama mwananchi wa kawaida anavyojidhulumu kwa kujidunisha mbele ya Meya kwa kumwita baba na kumwomba msamaha ilhali hajamkosea, hivyo basi kumpa Meya nafasi ya kumtusi na kumdhalilisha. Unyenyekevu huu wa kupita kiasi ambao unampa Meya nguvu ya kumdhulumu Dida unatokana na fikra za Dida kuwa kiongozi siku zote yu sawa na hakosi. Hapa Dida hang'amui kuwa ana umuhimu mkubwa katika kufanikisha uongozi wa Meya na ana haki ya kusimama kidete kutetea haki zake na kumkosoa Meya.

Itikadi hii ya kukubaliana na Meya kwa sababu yeye ni kiongozi inamuumiza Dida hasa Meya anapohusisha dharau katika amri zake kwa Dida. Aidha, wananchi wa kawaida wa Cheneo hawachunguzi sababu ya Mstahiki Meya kuwapeleka watoto wake ng'ambo kwa ajili ya masomo na mke wake kwa ajili ya matibabu ilhali kuna shule na hospitali katika mji wa Cheneo. Labda nikutokana na fikra kuwa ni jambo la kawaida watu walio na uwezo wa

kifedha mara nyingi kupeleka aila zao katika nchi za ng'ambo kwa huduma mbalimbali. Bila shaka wangechunguza wangetambua kuwa ni viwango vya elimu vilivyoshuka katika mji wa Cheneo. Huenda ndiyo maana kuna vijana wengi wasio na kazi ilhali wamehitimu kutoka vyuo vikuu. Kwa hivyo, wananchi wa kawaida katika mji wa Cheneo wamechangia kuwepo kwa elimu duni kwa kunyamaza wanapomwana Meya akiwapeleka watoto wake ng'ambo kusoma ilhali kuna shule Cheneo naye ndiye kiongozi wa kuhakikisha kwamba elimu ni bora.

Katika tamthilia ya *Amezidi* (Mohamed, 1995), Ame na Zidi wameigiza nafasi mbalimbali zikiwemo za wananchi wa kawaida na kama viongozi dhalimu. Sura hii iliangazia maonyesho ambamo Ame na Zidi ni wananchi wa kawaida na ibainishe jinsi wanavyochangia katika dhuluma zinazowakumba. Ame akiwa mwanafunzi, anajua kuwa kukariri mawazo ya Archimides hakujaleta manufaa yoyote hasa katika taaluma ya uhandisi. Anashangaa kwa nini hawajaunda nyambizi kutokana na mawazo ya Archimedes:

> **Mwanafunzi**: (Haonekani.) Suala!
>
> **Mwalimu:** Uliza!
>
> **Mwanafunzi:** Hivi ... hivi baada ya kukariri mawazo ya Archimides kwa miaka mingi, kwa nini hatujaweza kuunda nyambizi? (Mohamed, 1995: 30)

Japo hawajaiunda nyambizi, bado Ame na wanafunzi wenzake kama wananchi wa kawaida wanaendelea kukariri mawazo yake Archimedes. Archimedes alikuwa mwanasayansi ambaye maarifa yake yalitumiwa katika uundaji wa nyambizi. Hii ni kutokana na fikra kwamba mawazo na elimu kutoka nchi

zilizoendelea ni bora lakini ajabu ni kuwa wanapowahitaji wahandisi, huwaagiza kutoka nje. Hii ni kwa sababu elimu wanayoipata wanafunzi ni ya nadharia tu haiwezi kutumiwa katika uundaji na wanajidhulumu kama wananchi wa kawaida wanapong'amua hili na kutofanya mabadiliko yoyote wala kulalamika ili mfumo wa elimu ubadilishwe. Ndio maana katika ofisi, mashine ya kuchemsha maji, friji na simu zimeharibika na wanafunzi walioajiriwa baada ya kuhitimu kama Wahandisi kutoka chuo kikuu hawawezi kutengeneza mashine hizo kwa sababu walifundishwa nadharia tu:

Bosi: Mashine ya kuchemsha maji ya moto imeshatengezwa?

Msaidizi: Bado!

Bosi: Friji je?

Msaidizi: Bado pia.

Bosi: Na simu nazo, naona hazitoki nje?

Msaidizi: Bado mzee!

Bosi: Na birika la maji ya moto?

Msaidizi: Bado kabisa!

Bosi: Wanafanya nini basi wale vijana wetu tuliowajiri juzi, wale wahandisi wetu waliomaliza chuo kikuu juzi?

Msaidizi: Wanababaisha.

Bosi: Maana yake nini?

Msaidizi: Wanasema walifundishwa nadharia tu ...
(Mohamed, 1995: 42.)

Bosi analiona jambo la kawaida Wahandisi wa kwao wanapokosa ujuzi wa kutengeneza mashine mbalimbali ofisini mwake. Hashtuki kwa sababu ya itikadi kuwa Waafrika hawawezi kuunda na kutengeneza badala yake

anafurahia kwa kuwa akija mhandisi kutoka nje anaweza kushirikiana naye; kwa maana ya kunufaika kibinafsi. Hii itikadi kuwa Waafrika hawawezi kutengeneza imetokana na Waafrika wenyewe kwa sababu ya kufahamu chanzo chake kuwa mfumo mbaya wa elimu na bado hawafanyi lolote kuubadili na hivyo kuyabadili mawazo kuwa Waafrika wanaweza kuunda vitu mbalimbali ikiwemo nyambizi. Hapa mwanafunzi ambaye baada ya kuhitimu atakuwa mwananchi wa kawaida amejidhulumu kwa kukosa viwango vya kimataifa vya kitaaluma kwa kuendelea kujifunza yale ambayo tayari anafahamu hayatamsaidia maishani.

2.3 UCHUMI

Kulingana na Engels (1975) chanzo cha historia ya kunyonywa na kukandamizwa kwa wanawake ilianza wakati jamii ya binadamu ilipogawanyika katika matabaka mbalimbali. Jamii ilipobadilika na kuwa ya kitabaka, ilianzisha urithi upande wa kuumeni. Kutokana na haya, umilikaji wa mali ulimwendea mwanamume ukiwemo pia ukiritimba wa nyenzo za uzalishaji mali. Hali hii ilimpa mwanamke uwezo mdogo kiuchumi akilinganishwa na mwanamume. Kwa hivyo, akawa mtumwa kwa mwanamume ambaye alimdunisha mwanamke kwa kuwa na uwezo mdogo kiuchumi. Nafasi ya mwanamke iliendelea kuwa nyuma kutokana na tofauti za kikazi. Kazi nyingi za hadhi kama vile uongozi zilitengewa wanaume huku jamii ikifunzwa kuamini kuwa mahala panapomfaa mwanamke ni nyumbani. Maoni yake Engels ni muhimu kwa sababu mwanamke ni mmoja wa wananchi

wa kawaida anayeshughulikiwa katika utafiti huu na utabainisha jinsi baadhi ya wanawake kama wananchi wa kawaida wanavyochangia dhuluma dhidi yao kwa sababu ya kutojifunga kibwebwe kujiinua kiuchumi. Kwa mfano, tamthilia ya *Kilio cha Haki* inamsawiri Lanina kama mwanamke maskini ambaye licha ya kufahamu hivyo, habadili njia za kujiinua kiuchumi. Tunaelezwa kuwa mwanzo alikuwa kwenye shamba la Bwana Rhodeman kama mfanyakazi na alichochea mgomo wa nyongeza ya mshahara lakini hakufaulu. Anafanya vivyo hivyo katika shamba lake Delamon na badala ya nyongeza, anafutwa kazi. Delamon anajua kuwa Lanina ana uhitaji mkubwa ndiposa anamshika, anamtesa na kumwachilia atakavyo. Aidha mamake Lanina kama mwananchi wa kawaida anachangia katika hali yake ya chini ya kiuchumi pamoja na ya bintiye. Hili linabainika anapotofautiana naye katika harakati zake za kuboresha hali ya maisha ya wafanyakazi. Kulingana naye, Lanina anastahili kukaa nyumbani na kutunza watoto na kuacha fikra za kihalifu na za kujifanya sawa na waume. Hapa mamake Lanina anamvunja Lanina moyo, badala ya kumuunga mkono anampinga hivyo kudidimiza juhudi zake za kupata nyongeza ya mshahra na kujiinua kiuchumi. Hivyo mamake Lanina anaendeleze dhuluma dhidi yake na kuendelea kumpa Delamon na baadhi ya wanaume fursa ya kuwatawala.

Vilevile, katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, mamake Dadavuo Kaole anajidhulumu kiuchumi kwa kutofanya lolote ili kuhakikisha kuwa hali yake ya kiuchumi inaandamana na hali ya kiuchumi ya mji wa Cheneo. Hamudu

gharama ya mahitaji ya kimsingi kama vile chakula lakini haitishi mwajiri wake nyongeza ya mshahara. Badala yake, yeye na mwanawe wanakula kiporo kilichokusudiwa mbwa kwa sababu ya kutomudu bei ya makaa. Aidha, hang'amui umuhimu wake katika kuhakikisha kuwa maisha ya Meya ni shwari hivyo kutumia fursa hiyo kudai nyongeza zaidi ya mshahara. Kutokana na hali yake ya chini kiuchumi na bila kutia juhudi zozote kuiboresha, anasababisha kifo cha mtoto wake kwa kumlisha chakula kilicho na sumu.

Akishughulikia usawiri wa wahusika makahaba katika riwaya za Said Ahmed Mohamed, Muindi (1990) ameonyesha kuwa sababu zinazowavutia wanawake kushiriki katika tabia hii ambayo inachukuliwa kuwadhulumu wanawake ni uwezo mdogo wa kiuchumi walionao. Wanawake hawa hawana kazi maalum wala mtaji wa kuanzisha biashara. Japo utafiti huu haushughulikii usawiri wa wahusika makahaba, maoni yake Muindi yanadokeza kuwa ukosefu wa uwezo wa kujikimu kimaisha waweza kumuingiza mwananchi wa kawaida katika shughuli inayowezesha kudhulumiwa kwake au mwenye uwezo mkubwa kiuchumi kumdhulumu aliye na uwezo mdogo. Hata hivyo tamthilia za *Kilio Cha Haki*, *Amezidi* na *Mstahiki Meya* zimetumiwa katika utafiti huu kutoa picha ya jinsi wasio na uwezo mkubwa kiuchumi wanavyochangia katika hali zao za uwezo mdogo hivyo kuwapa walio na uwezo mkubwa kiuchumi fursa ya kuwadhulumu. Wafanya kazi wamegoma kwa sababu ya unyonyaji na udhalimu uliozidi shambani inavyobainika katika tamthilia ya *Kilio cha Haki* (1981). Japo wanafahamu kuwa wanadhulumiwa, wanaendelea kumfanyia

Delamon kazi na kulalamika tu mateso yalipozidi. Wafanyakazi kama wananchi wa kawaida wanajidhulumu kwa kuendelea kumfanyia Delamon kazi kwa muda mrefu na kwa malipo duni na kulalamika baadaye baada ya kugundua kuwa hali zao za kiuchumi zinaendelea kuzorota badala ya kuwa bora kwa kuwa wanafanya kazi. Wafanyakazi hawa wangekataa kwa pamoja kumfanyia Delamon kazi, angewabembeleza kwa kuwapa mshahara bora hivyo kuwainua kiuchumi na kuwathamini. Vilevile, wafanyakazi walikuwa na fursa ya kutafuta kazi nyingine ya kujiimarisha kiuchumi bila kudhulumiwa. Lakini uhitaji wao mkubwa ambao unatokana na uzembe na ukosefu wa umoja miongoni mwao unawasababishia dhuluma shambani mwa Delamon. Ndiposa wanapogoma katika harakati ya kutaka kuboresha malipo yao wanasikika wakiimba:

Sauti za wafanya – kazi

Mimi niliyekuwa nikiteswa kama fahali
Nikiwa silalamiki, kimya kama jabali
Kwa nini...
    Mimi kulemewa na mzigo wa maisha
    na kudidimizwa kwa uzito wa wakati
Kwa nini...
    Matunda ya jasho linitokalo kwa dhati
    kuwa sumu chungu inileteayo mauti
Kwa nini...
    Hii mikono majuruhi ijengeayo umati
    kuniacha nje nikilalia simiti
Kwa nni eee
Kwa nini eee
Eee... nimeshazinduka. (Mazrui, 1981: 7)

Wafanya kazi wanadokeza jinsi wanavyoteswa na mwajiri wao ambaye ni Bwana Delamon. Ajabu ni kuwa hawalalamiki hadi pale mateso yanapozidi. Kutolalamika kwao mapema ndiyo kunachangia mateso wanayoyapitia. Wanawakilisha tabaka la chini ambalo mara nyingi ni tabaka linalojikandamiza

kwa visingizio kama vile kukosa kazi au kulipwa mshahara duni. Ili kuwadhibiti, Bwana Delamon ambaye ni mwakilishi wa tabaka la juu anawaita askari ambao wanawafukuza wafanya kazi. Kisha Lanina na Tereki wanatiwa pingu na askari kwa hatia ya kuchochea mgomo. Baadaye, Tereki ambaye ni mwananchi wa kawaida anaangukia njama rahisi ya Bwana Delamon ya 'tenga utawale' anapomtumia Shindo kumshawishi kuwa kiongozi wa chama cha wafanyakazi na kuongoza atakavyoshauriwa na Delamon. Kukubaliana kwake Tererki na mdhulumu wake kunadidimiza juhudi za wafanyakazi za kujinasua kutoka umaskini hivyo kumpa Delamon mazingira mwafaka ya kuwadhulumu. Kutokana na ubinafsi, Shindo, Zari na makachero ambao ni wananchi wa kawaida wanakuwa wasaidizi wa mdhulumu wa wenzao kwa kuwanyamazisha wanapojaribu kujiinua kiuchumi kwa kutaka nyongeza ya mshahara. Ndiposa Shindo anamwambia Tereki kuwa akijua namna ya kuwaongoza wafanya kazi wenzake atapata manufaa makubwa kazini na madhumuni ya Delamon ni kuongeza pato la shamba lake na kumnufaisha yeye sio wafanyakazi wote. Uchumi kama mwanzo wa dhuluma unabainika Tereki alipokubali kuwa kiongozi wa chama cha wafanya kazi kutokana na ubinafsi huku wafanyakazi wenzake wakiendelea kufanya kazi ngumu kwa mshahara mdogo.

Tamthilia ya *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) inaonyesha jinsi Wanacheneo wanavyokosa huduma muhimu kwa sababu ya hali zao za chini kiuchumi. Jambo hili linabainika pale ambapo mamake Dadavuo Kaole anashindwa kukimudu chakula bora wala makaa ya kukipikia. Alimpatia mtoto wake wali

na maharage yaliooza na kumsababishia maradhi. Wanacheneo walimchagua Meya kwa imani kuwa angeboresha hali yao ya maisha lakini sivyo ilivyo kwa sababu hali yao ya maisha ni ngumu. Aidha, Wanacheneo walishindwa kumudu gharama ya matibabu na dawa zenyewe hazipo na wengine walikufa kwa njaa. Watu wengi hawana ajira, walio nayo mishahara yao haitoshi wala hailipwi kwa wakati. Wanacheneo kama wananchi wa kawaida ndiyo wamejisababishia shida hizi kwa kumchagua kiongozi ambaye hayajali maslahi yao. Tunaelezwa kuwa, licha ya shida zinazowakumba, Wanacheneo wamemchagua Mstahiki Meya mara tatu na Meya anaamini akitaka kuchaguliwa mara nne, tano au sita, bado Wanacheneo watamchagua. Bila shaka kuimarika kwa uchumi wa nchi na wananchi kunategemea kiongozi. Kiongozi akiwa na sera mbaya za kiuchumi, uchumi wa nchi utasambaratika na ni jukumu la wananchi kuhakikisha kuwa uchumi wao umeimarika kwa kumchagua kiongozi bora. Japo uchumi wa Cheneo umezorota, wananchi hawambadilishi kiongozi kwa vipindi vitatu, hivyo dhuluma zinazowakumba zinatokana na maamuzi yao ya kumchagua kiongozi mbaya.

Said Ahmed Mohamed katika *Amezidi* (1995) amesawiri Bara la Afrika kama eneo lenye utajiri mkubwa. Lina makaa, almasi, dhahabu, shaba, mafuta na chuma. Licha ya utajiri huu mkubwa, Ame na Zidi ambao wanawakilisha wananchi wa kawaida hawapendi kufanya kazi. Hawaoni haja ya kupenda kazi na Mungu yupo na ardhi ipo ambayo ni bikra. Wanatumia muda wao mwingi kulala na hawafikirii jinsi ya kutumia malighafi waliyonayo kujiinua kiuchumi.

Kutokana na uzembe wao, wanajidhulumu kwa majanga kama vile njaa na ukame na kulazimika kuomba misaada ambayo vilevile inawadhulumu kwa kuwa hahitajiki katika nchi zilizoendelea. Wangekuwa wamejiimarisha kiuchumi kwa kutia bidii, wangejenga hata bwawa ambalo lingetumika kuhifadhi maji ya kunyunyiza kwenye mimea. Kutokana na ukame, nchi za Marekani na Uingereza zilitoa misaada ya magunia milioni kwa milioni ya nafaka nayo Ufaransa ikatoa madawa ambayo huko hayahitajiki. Hapa mwandishi wa tamthilia hii anatumia kinaya kuikejeli Afrika kuwa wana utajiri na bado wanategemea misaada kutoka nchi za magharibi. Ni bayana kuwa, Bara la Afrika lina malighafi nyingi lakini uvivu unaosababisha kutotumiwa kwa malighafi hizo umeleta uwezo mdogo wa kiuchumi. Hali hii imezipa nchi zilizoendelea faida zaidi kutokana na matumizi ya malighafi kutoka Afrika na kuwaacha Waafrika wa kawaida maskini.

2.4 MATUSI NA DHARAU

Matumizi ya lugha ndiyo yanayokuza na kupalilia mawazo yenye taasubi za kiume. Ubaguzi wa kiuana hujitokeza kupitia ishara za lugha ya kitamathali katika asasi kama vile ukoo, ndoa, dini au maelezo kuhusu maumbile na matumizi mengineyo ya lugha (Escholz, 1982). Maoni yake Escholz yanaungwa mkono na Wafeministi na yanaonekana kuegemea upande wa unyanyasaji wa wanawake. Hata hivyo ni muhimu ibainike kuwa matumizi ya lugha kwa njia hasi kwa mfano, matusi hayamwathiri tu mwanamke bali hata mwanamume na watoto. Gitau (2005) anayapa maoni haya nguvu katika utafiti

wake juu ya kunyanyaswa kwa mwanamume. Anabainisha matusi kama chanzo cha dhuluma kwa mwanamume. Matusi na dharau miongoni mwa wananchi wa kawaida husababisha uhasama na kuvunja umoja miongoni mwao. Utengano miongoni mwa wananchi wa kawaida humpa mdhulumu fursa ya kuwadhulumu zaidi.

Katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki*, Zari anawavunja moyo Lanina na Tereki kwa kuwaita washenzi wanapotetea haki zao. Japo Zari ni msaidizi wa Delamon, haheshimiwi na Delamon kwa hivyo yeye ni sawa na mwananchi wa kawaida na anapowatusi na kuwavunja moyo wapiganiaji haki, anajidhulumu vilevile.

Lanina anapowatembelea wazazi wake baada ya kufunguliwa kutoka kizuizini, babake anamkana na kumtusi kwa sababu ya taasubi ya kiume na utamaduni kuwa mahali pake mwanamke ni nyumbani. Shughuli za kupigania haki ni za wanaume na mwanamke anayeshirikiana na wanaume katika kupigania haki ni mwacha mila na malaya. Babake Lanina kama mwananchi wa kawaida anajidhulumu kwa sababu haki anazozipigania Lanina zitamfaidi pia. Lakini anapomvunja moyo kwa kumtusi na kumkana ina maana kuwa hali zao za maisha zitaendelea kuwa mbaya licha ya kufanya kazi. Lengo la babake Lanina ni kupata heshima kutoka kwa wanakijiji ambao wanaisema familia ya kina Lanina vibaya kuwa Lanina ameasi utamaduni. Aidha, wanakijiji pia ambao ni wananchi wa kawaida wanamchochea babake Lanina kumtusi hivyo kudidimiza juhudi za Lanina za kuwakomboa kutoka dhuluma zinazowakumba

na kuwapa wanaowadhulumu fursa ya kuendeleza dhuluma zaidi bila pingamizi:

Lanina: Baba, mbona...

Baba: Baba? Umesema nini?
Babako mimi?
Mimi sikuzaa malaya!

Lanina: (Kwa kustaajabu) Babaa!...

Baba: Nimekwambia usiniite baba, husikii?
Ndiyo! Mimi sikuzaa malaya!
Wala si kuzaa wana wasaliti!
Ndiyo! Sikuzaa binti yeyote
anayeweza kuisaliti nchi yake.
Sikuzaa binti anayetaka uume!
Hee – he! Mimi Seromanga!
Mimi! Mimi nizae mke – mume!
Heee – he! Labda mtu mwingine; si mimi!
(Mazrui, 1981: 37 – 38)

Maneno ya babake Lanina yamejaa taasubi ya kiume, yaani Lanina ametupilia mbali mila na kushirikiana na wanaume kupinga kudhulumiwa na Delamon. Kwa kufanya hivyo, anatiwa kizuizini na kumwachia bwanake jukumu la kuwalea watoto kinyume na mila zao. Kulingana na Mzee Seromanga, Lanina ni mwanamke na hastahili kushiriki matendo ambayo ni ya wanaume kulingana na utamaduni kama kupigania haki kwa sababu kwa kufanya hivyo, anakuwa mke - mume. Hakika ni kuwa, Mzee Seromanga anajidhulumu kwa kuwa shida za kiuchumi hazimwathiri Lanina pekee bali hata Seromanga pia na kupinga juhudi za kumhauni kwa kusingizia utamaduni uliopitwa na wakati ni sawa na kuwa chanzo cha dhuluma dhidi yake.

Musa na mmoja wa wafanya kazi kama wananchi wa kawaida wanazozana kutokana na tofauti za kimtazamo jinsi Delamon analiendesha shamba lake. Musa anahisi kuwa japo Delamon amewapa nyongeza, hawaruhusu kufanya

‘over - time’ na wanalazimishwa kufanya kazi zaidi wakati wa kawaida. Mfanya kazi haoni zaidi ya kupata nyongeza; cha muhimu kwake ni mshahara kuongezwa lakini haoni kuongezeka kwa kiwango cha kazi:

Mfanya-kazi : Si tumepewa nyongeza!

Musa: Wacha ujinga wewe!

Mfanya-Kazi: Mjinga? Mimi mjinga? Wewe usiniite mjinga nakwambia!

Musa: Mjinga! Tena mjinga sana! Kwani huoni...
(Mazrui, 1981: 43)

Musa na mfanyakazi wanajidhulumu kama wananchi wa kawaida kwa kusababisha utengano kati yao kupitia kwa matusi badala ya kuwa na umoja na kupanga jinsi ya kujiepusha na dhuluma dhidi yao. Utengano miongoni mwa wananchi wa kawaida hupunguza idadi ya wanaopigania haki hivyo kuwapa wadhulumu fursa ya kuendelea kuwadhulumu.

Tamthilia ya *Mstahiki Meya* (2009) nayo imebainisha jinsi Dida kama mwananchi wa kawaida anavyojidhulumu kwa kukubali kuathirika na njama ya matusi na dharau ya Mstahiki Meya. Anatumia lugha ya vitisho ili kumjaza Dida uoga ajione mwenye makosa na iwe rahisi kwake Meya kumdhibiti kwa urahisi naye Dida anapatikana na mtego huu:

Meya: (*kwa ukali*.) Hivi una nini?

Dida: (*Anashangaa. Anajibu kwa upole.)* Mstahiki Meya... lipo lililoenda kombo? Samahani sana...

Meya: Sina haja na hadithi zako za pole. Amekutuma nani kunichoma kwa chai mapema hii? Una njama gani?

Meya: (*Akiashiria sahani.*) Je, na haya mayai?

Dida: Yana nini baba?

Meya: (*Kwa ukali.*) Wewe huoni si kama zamani?

Dida: Naona baba.

Meya: Sababu?

Dida: Mwenye kuyaleta mstahiki meya anasema hali zimebadilika. Kuku wanatga madogo hivi.

` **Meya:** (*Kwa dharau*) Kisha bado unamruhusu kunipunja kwa kuleta viyai kiasi hiki? Eeh? (Arege, 2009: 9)

Dida anamruhusu na kumtia Meya motisha ya kuonyesha dharau dhidi yake kwa kuwa mnyenyekevu kupita kiasi. Maisha ya Meya nyumbani hayawezi kunyooka bila watumishi kama Dida. Kwa hivyo, Dida anaweza kutumia fursa inayotokana na umuhimu wake nyumbani mwa Meya kuzuia uoga unaotokana na dharau na matusi ya Meya na kupigania haki zake. Lakini anaporuhusu athari ya dharau kumzuia kupigania haki zake kama vile heshima kutoka kwa mwajiri wake, basi anajidhulumu kama mwananchi wa kawaida.

Aidha, wananchi wa kawaida wa Cheneo wanajidharau na wadhulumu wamegundua hili ndiposa wana ujasiri wa kuwadhulumu. Japo wanakumbwa na shida ambazo zinatokana na uongozi mbaya, hatuoni yeyote kati ya wananchi wa kawaida akijitokeza kuania uongozi wa mji wa Cheneo ili kuboresha maisha ya wenzake. Kwa sababu ya kuona kuwa hawawezi kuwa viongozi, wanamchagua Meya mara tatu jambo linalomtia kiburi na ujasiri wa kukosesha huduma muhimu kama vile huduma za afya kimakusudi. Kutokana na kujidharau, wananchi wa kawaida wamejidhulumu kwa kujiona duni hivyo kuwapa wasiowajali fursa ya kuwaendeshea maisha visivyo.

Katika *Amezidi* (Mohamed, 1995), Maisha ya Ame na Zidi ambayo yamejaa uvivu na uzembe yanafanya wajidharau na wadharauliwe na watu wengine. Kwa mfano, Ame ambaye amechukua nafasi ya Mari mwanamke mpenziwe Zidi anamkejeli Zidi kwa kuwa na ndoto ya mapambo mazuri ya nyumba lakini hafanyi lolote kutimiza ndoto yake. Zidi anapomwambia Mari kuwa anapaswa kufurahi na kucheka, Mari anamjibu kwa njia ya kumdunisha na kila kitu alichonacho:

> **Mari:** Kwa nini? Kwa hayo makochi na masofa ya upepo? Kwa hivyovitanda vya majani? (*Anaonyesha yale majani yaliyotandikwa sakafuni*.) Kwa hilo rediogramu lililomo kwenye fikra? Kwa hiyo TV ya mawazoni?Limejaa ... limejaaa ... limejaa kasri ... (Mohamed, 1995: 21).

Hapa Ame na Zidi wakiigiza nafasi ya mwananchi wa kawaida wanajicheka wenyewe. Wanajidhulumu kwa kutofanya bidii ili kupata vitu vya kufanya maisha yao yawe bora. Wana mawazo mazuri lakini hawafanyi chochote kuyatekeleza na uzembe wao unajitokeza katika matumizi ya dharau.

Kitendo cha Ufaransa kutoa madawa ya msaada ambayo huko hayahitajiki ni matusi kwa Ame na Zidi ambao wanawakilisha wananchi wa kawaida. Hii ni ishara ya dharau lakini Ame na Zidi ndiyo wanaojisababishia haya kwa kutotia bidii kuyaboresha maisha yao kwa kutumia malighafi kochokocho walinayo. Ufaransa haithamini Ame na Zidi ndiposa inawapatia madawa ambayo yanaweza kuwadhuru zaidi. Ame na Zidi wanapokubali misaada kama hii, inafanya wenye kuwapatia kuwadharau na pia kuwafanya Ame na Zidi kutoona umuhimu wa kufanya kazi. Isitoshe, hii ni njama ya nchi zilizondelea ya kuunda urafiki wa bandia ili Ame na Zidi washawishike na kuwapatia malighafi yao. Ame na Zidi bila kugundua wanakubaliana na njama hii hivyo

kwendelea kujidhulumu kwa kudharauliwa na kupatiwa misaada isiyo na maana likiwemo paja la ng'ombe kutoka EC linalosababisha kuumwa kwa tumbo kwa Zidi.

2.5 UFISADI

Akiihakiki tamthilia ya *Wingu Jeusi*, Mahero (1992) anaeleza kuwa dhuluma katika tamthilia hiyo imetokana na siasa ya tamaa ya ukubwa wa kupindukia, ufisadi, ukabila na unafiki. Anaendelea kueleza kuwa, jamii imekuwa nzuri tangu kuchipuka kwake. Uzuri huu huchafuliwa pindi mazingira yanayodhalilisha utu yanapotokea. Mazingira haya yanaweza kuwa asilia kama njaa, ukame na magonjwa jinsi ilivyokuwa katika jamii za kale. Aidha, wanadamu wanaowakandamiza wenzao kwa kuzingatia maslahi yao ya kibinafsi ni sehemu kubwa ya mazingira haya machafu leo hii hasa kutokana na ubepari. Uhakiki wa tamthilia za *Kilio Cha Haki*, *Mstahiki Meya* na *Amezidi* uliangazia jinsi mwananchi wa kawaida anavyojidhulumu kwa kupalilia ufisadi katika mazingira yake.

Tamthilia ya *Kilio Cha Haki* imebanisha jinsi wananchi wa kawaida wanavyochangia kuwepo kwa ufisadi kama ifuatavyo: Mwanzo, hawahoji matumizi mabaya ya vyombo vya usalama dhidi yao wanapogoma. Aidha, wanajua hasa wafanyakazi kuwa Delamon ni fisadi lakini hatuoni dhuluma hiyo ikijitokeza miongoni mwa malalamishi yao. Kutokana na kukimya kwao,

wadhulumu wanapata fursa nzuri inapobainika katika matumizi ya askari bila kufuata sheria yoyote ila tu urafiki unaotokana na ushirikiano wa kifisadi:

Delamon: (*Akijaribu kujifanya mchangamfu kidogo*)
Halo! Kamishna...Ooo nzuri tu...Ha! Ha!Ha!...
Hapana, si kwa sababu hiyo...Kesi hiyo
imeshafutwa na yule inspekta wa Kihindi...
Nani?...Naam, ndiye huyo...
(*Anasikiliza. Anacheka kidogo*)
Leo tuna shida ya aina nyingine kabisa
Aaaa... wafanya - kazi wetu wamegoma na...
(*Anasikiliza kwa makini*)
Kwa nini tusikuarifu mapema? *(Kimya kidogo*)
Aaa! Tulidhani tutaweza kuyatengeneza
Sisi wenyewe, lakini... (Mazrui, 1981:9)

Mazungumzo kati ya Delamon na Kamishna Henderson yanabainisha watu walio na uhusiano wa karibu na wa kisiri ambapo baadhi ya matendo yao hayafuati sheria kwa sababu ya ubinafsi na wako tayari kusaidiana hata kwa kuvunja sheria. Wananchi wa kawaida hasa wafanyakazi wamewaruhusu kuvunja sheria kwa kukimya na kuliona kama jambo la kawaida. Vilevile, wafanyakazi wanapalilia ufisadi wanaposhindwa kumtetea Lanina na Tereki wanapokamatwa. Wanatawanyika wanapowaona askari na kuwaacha Lanina na Tereki wakitiwa pingu kwa tuhuma za kuchochea mgomo. Baadaye baada ya kuachiliwa kwa Lanina na Tereki, hawahoji kwa nini wanaachiliwa bila kufunguliwa mashtaka hata baada ya kuambiwa kuwa waliachiliwa kwa amri ya Bwana Delamon. Hapa Lanina na Tereki kama wananchi wa kawaida wanachangia kuwepo kwa ufisadi kwa kumpa mdhulumu wao fursa ya kuwa askari na jaji bila kupinga au kuweka wazi tendo hilo la kifisadi lijulikane na liwe miongoni mwa malalamishi ya wafanyakazi. Aidha, Tereki kama mwananchi wa kawaida anapalilia ufisadi kwa kushawishika haraka na

kukubali njama za kifisadi za Bwana Delamon za kuwa kiongozi wa chama cha kuwanyanyasa wafanyakazi huku akifaidika kwa kulipwa na Delamon:

> **Tereki:** Na wafanyakazi hao watanufaika vipi?
>
> **Shindo:** Madhumuni ni kuongeza pato la hili shamba na kukunufaisha wewe - siyo wafanyakazi wote. Kama si hivyo hapana faida ya sisi kukujia wewe. Kwa hali yoyote hawatakosa chochote hapa na pale. (Mazrui, 1981: 17.)

Mbinu ya 'tenga utawale' anayoitumia Delamon inatokana na ufisadi. Tereki kutokana na ubinafsi anakubali azimio la Delamon. Mwishowe wafanya kazi wanapata nyongeza lakini wanafanya kazi zaidi ya wakati wa kawaida.

Aidha, tamthilia ya *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) imebainisha jinsi Wanacheneo ambao ni wawakilishi wa wananchi wa kawaida wanapata shida nyingi kwa sababu ya kuupatia ufisadi fursa ya kushamiri. Kwanza kabisa, Meya anauza ardhi ya umma aliyoinyakua na kutumia mapato yake kuwapeleka watoto wake ng'ambo ili wapate mafunzo lakini Tatu, Beka na Medi kama wananchi wa kawaida na pia kama wawakilishi wa wafanyakazi ambao ni wananchi wa kawaida hawataji wala kuorodhesha ufisadi huu miongoni mwa shida zinazowakumba. Isitoshe, hawaulizi sababu ya Meya kuwapeleka watoto wake na mke wake ng'ambo kupata elimu na matibabu mtawalia ilhali kuna shule na hospitali katika Mji wa Cheneo. Vilevile, wangehoji alikotoa hela za kugharamia shughuli za aila yake ng'ambo licha ya hali ngumu ya maisha iliyokuwepo hata kwa matajiri kama Meya anavyodokeza Bili. Wawakilishi wa wafanyakazi na wafanyakazi wenyewe kama wananchi wa kawaida wanapokosa kufanya uchunguzi na kuweka wazi

matendo ya ufisadi, basi wanachangia dhuluma dhidi yao kama vile ukosefu wa huduma za elimu na afya bora. Kutokemea matendo ya ufisadi na wananchi wa kawaida kumchagua Meya mara tatu licha ya ufisadi wake, kunampa ujasiri wa kutaka kulifilisi Baraza la Cheneo zaidi kwa kukiuka mkataba wa kandarasi kimakusudi hivyo kumlipa mwanakandarasi fidia ambayo pia angefaidi huku uchumi wa wananchi wa kawaida hasa wafanyakazi ukizorota. Mwisho, Mhubiri ambaye ni miongoni mwa wananchi wa kawaida anaendeleza ufisadi kwa kukubali uongo wa Meya kuwa kila wanapokutana, Meya husukumwa na kutaka kuacha kazi ya umeya na kumfuata. Anashawishika na maelezo yake Meya na kumpongeza na kupongeza uongozi wake na kusahau kuyakemea maovu kama vile afya na elimu duni, mazingira mabaya ya kufanyia kazi na malipo duni miongoni mwa shida nyingine zinazotokana na ufisadi. Kisha Mhubiri anakubaliana na mpango wa baraza wa kugharamia petroli ya kumpeleka na kumrudisha kutoka kwa baraza baada ya maombi pamoja na sadaka ya shilingi laki moja kila mwezi. Hapa Mhubiri kutokana na ubinafsi anaungana na Meya kuendeleza ufisadi kwa kuwa hela anazotarajia kupokea ni za maendeleo ya Mji wa Cheneo.

Tamthilia ya *Amezidi* imedokeza pia jinsi Ame na Zidi wanavyouendeleza ufisadi wanapoigiza nafasi ya wananchi wa kawaida. Kwa mfano, Zidi anapoigiza kama mwalimu haelewi anachokifunza na hataki kuulizwa maswali na mwishowe anawapotosha wanafunzi kwa kuwaambia waimbe wimbo wa utajiri ambao unahusu utajiri walio nao na hivyo hakuna haja ya kusoma. Ame

naye kama mwanafunzi haweki bidii masomoni kwa sababu wao ni matajiri na hawana haja ya kufikiri kwa vile wanaweza kuwalipa wengine wawafikirie, wawafanyie utafiti na wawavumbulie. Tabia ya mwalimu na mwanafunzi inasababisha ukosefu wa mafundi na kulazimisha mafundi kuagizwa kutoka nje. Mafundi wanaoagizwa hushirikiana na wadhulumu wa wananchi wa kawaida kupanga mikakati ya kupora mali ya umma. Aidha, hali hii imewapa wadhulumu wao fursa ya kutobadilisha mfumo wa elimu ambao ni wa kinadharia kwa sababu elimu ya kutengeneza itawanyima nafasi ya kuifisidi umma.

Isitoshe, wafanyakazi ambao wanawakilisha wananchi wa kawaida wanaedeleza ufisadi kutokana uoga. Baada ya mdhulumu (Bosi) wao kupora pesa na kuunda orodha ya uongo ya vitu vilivyonunuliwa, anawatisha wafanyakazi na mmoja wao anapojaribu kuuliza suala, Bosi anamkemea na kumnyamazisha. Tunatarajia wenzake kumuunga mkono katika kuhoji kupotea kwa pesa na kwa nini wanashirikishwa wote lakini wananyamaza hivyo kumpa Bosi nafasi ya kuuficha uovu wake kama inavyojitokeza:

Bosi: Sawa – ah, aa ... aaa. (*Anaonekana kakasirika sasa*.) Hapa pameingia mtindo ... mtindo wa kudokoadokoa fedha za taifa, mali ya umma, mali ya wananchi ...wengine wanatumia wizi wa kalamu ... wengine wa dhahiri shahiri ... sasa nimekwiteni kukuambieni tunafanya uchunguzi wa kuyafuatilia mambo ... aliyemo hatoki na asiyekuwemo haingii. Na tutakayempata, kwanza kazi basi, na kisha mahakamani ...

Sauti ya Mfanyakazi: Suala mzee ...

Bosi: Hiki si kipindi cha masuala na majibu – hii si stesheni ya redio ...
Hapa ofisini, tena ofisi yenyewe ya Bosi ... hapa tunafanya kazi, hatuulizi masuala na kupeana majibu ... Tawanyikeni mrejee mwahala mwenu mwa kazi... (Mohamed, 1995: 46).

Hapa wafanyakazi wanatawanyika bila pingamizi bila shaka kutokana na uoga. Wanajidhulumu kwa kuwa kila wakati Bosi atakapokuwa akificha matumizi yake mabaya ya pesa atakuwa anawatisha.

2.6 HITIMISHO

Sura hii ililenga kubainisha jinsi mwananchi wa kawaida anavyojisababishia dhuluma kwa kuwajibika au kutowajibika. Yaliyorejelewa kama njia anazozitumia mwananchi wa kawaida kujidhulumu ni itikadi, uchumi, ufisadi, matusi na madharau. Itikadi imebainishwa kupitia jinsi wananchi wa kawaida wanavyowaona na kuwafikiria wadhulumu wao kama wasio na dosari na wanaostahili heshima hasa katika maamuzi yao. Kasumba hii imechukuliwa kuwa ya kweli na wanaoongozwa na kukosa kufanya juhudi zozote kwani kwao kudhulumiwa ni majaliwa. Katika upande mwingine, uchumi umebainishwa kama chanzo cha dhuluma pale ambapo wasio na uwezo wa kiuchumi ambao ni wananchi wa kawaida hawatii juhudi katika kujiinua kiuchumi na kukosa kuwa chambo cha wadhulumu. Aidha, wananchi wa kawaida wenyewe huwapinga na kuwashtumu wenzao wanaowapigania ili kuinuka kiuchumi hivyo kudidimiza juhudi za kujikomboa. Matokeo ya matusi ni kuwa wananchi wa kawaida wanapowatusi wenzao, huwavunja moyo na kuvunja umoja miongoni mwao ambao ni muhimu katika vita dhidi ya dhuluma. Aidha, matusi pamoja na madharau hupunguza uwezekano wa wanaodhulumiwa kuungana na kupinga dhuluma dhidi yao hivyo kuwapa wanaowadhulumu fursa ya kuendelea kuwadhulumu zaidi. Ufisadi

umejadiliwa kwa kuangazia baadhi ya matendo anayoshiriki mwananchi wa kawaida ambayo hupalilia ufisadi kama vile kutoufichua ufisadi unapotendwa au kuungana na wafisadi kwa sababu ya ubinafsi.

Njia alizozitumia mwananchi kujidhulumu zimefasiliwa kwa mujibu ya nadharia ya udenguzi. Wanaanchi wengi wameshiriki matendo yanayochangia dhuluma dhidi yao bila kujua. Kwa mfano, baadhi ya tamaduni kama vile taasubi ya kiume zikifasiliwa kwa makini zinabainika kuwa vizuizi katika ukombozi wa mwananchi wa kawaida hasa mwanamke.

SURA YA TATU

3.0 ATHARI ZINAZOTOKANA NA DHULUMA KWA MWANANCHI

3.1 UTANGULIZI

Katika sura ya pili, utafiti umeangazia jinsi wananchi wa kawaida wanavyojisababishia dhuluma kwa kuwajibika au kutowajibika. Baadhi ya mambo yaliyoshughulikiwa na ambayo wananchi wa kawaida hushiriki au kutoshiriki na kujisababishia dhuluma ni itikadi, uchumi, dharau na ufisadi. Katika sura hii, tumechunguza athari zinazotokana na dhuluma dhidi ya mwananchi wa kawaida. Aidha, athari hizi zimehusishwa na aina ya dhuluma ambayo au ambazo ni chanzo cha athari husika. Zifuatazo ni athari zinazotokana na dhuluma kwa mwananchi wa kawaida:

3.2 KIFO

Katika tamthilia ya *Kilio cha Haki* (1981), kifo kama athari ya dhuluma kinajitokeza pale ambapo Tereki na Shindo wanauawa na wafanya kazi wengine. Mauaji haya yanasababishwa na hasira walionayo Musa na wenzake kutokana na kunyanyaswa na kusalitiwa na Tereki na Shindo kama wananchi wa kawaida. Kulingana na Bwana Delamon, unyonyaji lazima uwepo na watu wote hawawezi kuwa sawa. Anatumia mtazamo huu katika kuwaongoza wafanyakazi katika shamba lake kwa ushirikiano wa Tereki na Shindo bila kung’amua kuwa wafanyakazi walikuwa wamechoka kuvumilia na walikuwa tayari kupigana au kufa katika harakati ya kukomesha ufukara. Katika

kufanikisha azimio lao, Dewe, Musa na watu watatu wanawaua Delamon, Shindo na Tereki:

Dewe: Damu imwagikeee!

Watu: Imwagikeee! Imwagikeee!
Damu imwagikee! (Mazrui, 1981: 72)

Delamon na washirika wake wanauawa kwa sababu ya kuwadhulumu wafanyakazi kwa kuwalipa mshahara mdogo, kuwaundia chama ambacho sheria zake ni za kutetea maslahi ya Bwana Delamon na wakuu wa chama cha wafanyakazi badala ya wafanyakazi wenyewe na kuwaitia wafanyakazi askari ambao huwachapa na kuwaumiza wanapogoma katika harakati ya kupigania haki zao. Kifo hasa cha Tereki na Shindo kimetokana na hasira ya wafanyakazi kwa sababu ya kuungana na mdhulumu wao yaani Bwana Delamon na kwendeleza sera zake za kuwadhulumu wafanyakazi wenzao.

Nayo tamthilia ya *Mstahiki Meya* (Arege, 2009), inasawiri kifo kama athari ya dhuluma pale ambapo Dadavuo Kaole ambaye ni mtoto wa miaka mitatu anakufa kutokana na usaliti na kutowajibika kwa wananchi wa kawaida wa Cheneo. Kutowajibika kwao kunabainika wanapomchagua Mstahiki Meya mara tatu licha ya kuwa kiongozi mbaya. Meya anakuwa na kiburi na hata kusema kuwa hata akitaka uongozi mara ya nne, tano na hata sita bado atachaguliwa. Kiburi hiki kinamfanya kutowajibika katika kuwapa Wanacheneo huduma muhimu kama afya hivyo kusababisha vifo kama cha Dadavuo Kaole. Mamake ambaye ni mfanyakazi nyumbani mwa Meya halipwi

mshahara wa kutosha na mshahara wenyewe huchelewa. Kutokana na kutokuwa na uwezo wa kifedha, anamlisha Dadavuo kiporo cha wali na maharagwe kwa sababu makaa na mafuta ya kukitokosa yamepanda bei. Isitoshe, siku nyingi wamekuwa wakila chakula walichopimiwa mbwa. Dadavuo anaendesha kwa kula chakula kilichooza na badala ya kutibiwa kikamilifu, anaandaliwa mchanganyiko wa sukari na chumvi katika maji moto kwa sababu dawa zenyewe hazipo:

> **Siki:** Waridi andaa mchanganyiko wa sukari na chumvi katika maji moto. Huenda itasaidia kidogo...
>
> **Waridi:** Hayo lakini si matibabu.
>
> **Siki:** Mwandalie tu. Dawa tulizonazo ni *pain killers* tu! Afadhali kufanya jambo kuliko kutofanya kabisa. Labda itauwezesha mshumaa kuwaka hadi meli zinazosubiriwa zimalize kupambana na mawimbi. (*Kwa upole*) Waridi, wawashie taa ya tumaini. Ganga ganga za mganga huleta tumaini (Arege,2009: 6).

Siki anathibitisha kuwa hakuna dawa muhimu zahanatini licha ya kuwa ni jukumu la uongozi wa Cheneo kuhakikisha kuwa Wanacheneo wanapata huduma bora za afya. Badala yake, Mstahiki Meya anadanganya kuwa ameagiza dawa na zipo njiani. Huu ni usaliti kwa Wanacheneo ambao walimchagua kwa matumaini kuwa atawaongoza kwa njia mwafaka. Kwa hivyo, kifo cha Dadavuo Kaole kimesababishwa na kutowajibika kwa mamake Dadavuo Kaole kama mpiga kura na kama mzazi na mlezi mwema hasa kwa kukosa kuomba nyongeza ya mshahara au kujishugulisha na njia nyingine mbadala za kutafuta riziki ili awe na uwezo wa kununua chakula bora na kugharamia matibabu bora ya mtoto wake.

Isitoshe, ukosefu wa dawa zahanatini na mazingira duni ya kufanyia kazi unasababisha kifo cha mtoto wa mama mdogo wa Waridi. Hali hii inatokana na kutowajibika kwa wananchi wa Cheneo hasa kwa kuwachagua viongozi wabaya. Waridi anasema, "Lilikuwa jambo la kusikitisha kumtazama mtoto wa mama mdogo akifia mikononi mwangu naye amenitazamia kuokoa maisha ya bwana mdogo. Haikuwa rahisi kwetu sote." (Arege, 2009: 36). Waridi aliacha kazi ya uuguzi kwa kuwa watu walikufa akitazama na hangeendelea kufanya kazi ambayo haimnufaishi yeye na watu wengine. Japo Baraza la mji limeelezwa kuhusu ukosefu wa dawa, halijafanya lolote licha ya ahadi nyingi kwamba hali hii inashughulikiwa. Ndiposa Tatu ambaye ni mwakilishi wa wafanya kazi anasema kuwa,

> Watu wanakufa kwa sababu ya kukosa dawa. Ni hali ya kusikitisha! Afadhali watu wangekuwa wanakufa kwa kushindwa kulipia dawa zilizopo. Sasa tungekuwa tunalishinikiza baraza la mji kuwapa watu dawa hata kama kwa mkopo. Muda wote niliolifanyia Baraza hili kazi, si kupata kuona hali kama hii. Watu wanajifia kama nzi! (Arege, 2009: 38.)

Watu anaowarejelea Tatu ni wananchi wa kawaida na wanakufa kutokana na ubinafsi, uoga wa kuukabili uongozi mbaya wa Meya. Wanajidharau hivyo kutowania uongozi wa Cheneo ili kuyaboresha maisha yao. Kutojiamini kwa wananchi wa kawaida kunampa Meya kiburi hasa wanapomchagua mara kadha licha ya kuwadhulumu hadi kuwasababishia vifo. Ndiposa Beka ambaye pia ni mwakilishi wa wafanyakazi anaeleza jinsi kutojali kwa Meya na wenzake kulivyosababisha kifo cha mtoto wa mwenzao. Anasema:

> Juzi mtoto wa Kerekecha amekufa kama nzi. Amemfia mikononi mwake mwenyewe Kerekecha akitazama. Sisi tunaambiwa hakuna dawa na zinapokuwepo tunaambiwa

> kulipia ilhali madiwani mna bima ya matibabu katika hospitali kubwa. Nyinyi na familia zenu. Sisi mnatutaka kulipia. Tutalipia vipi iwapo za kununulia chakula hazitoshi? Kula Sukuma na dona kila siku ni jambo wengi wetu hata hatuliwezi (Arege, 2009: 69.)

Maelezo yake Beka yanathibitisha wazi kuwa kifo cha mtoto wa Kerekecha kimesababishwa na Kerekecha mwenyewe kama mwananchi wa kawaida. Mchango wake unatokana na kuwa miongoni mwa waliowachagua viongozi wenye ubinafsi ambao wana bima katika hospitali kubwa hivyo kutokuwa na haja ya kushughulikia hospitali za wananchi wa kawaida. Aidha, Kerekecha amesababisha kifo cha mtoto wake kwa kutotia bidii ili kujiinua kiuchumi apate hela za kujikimu kama vile kumpeleka mtoto wake kwa hospitali kubwa.

Aidha, njaa ambayo inatokana na uzembe na uvivu wa Wanacheneo imechangia kuwepo kwa vifo katika mji wa Cheneo. Tunaelezwa kuwa baadhi ya Wanacheneo wanakufa kwa njaa kwa sababu hawawezi kumudu gharama ya chakula. Hata sembe na sukuma ni vigumu kutiwa mezani. Mwandishi anatoa mfano wa sembe na sukuma ambacho ni chakula cha kiwango cha chini sana ili kusisitiza jinsi walivyo wazembe huku wakisingizia ukosefu wa kazi. Walio na kazi nao wakisingizia kuchelewa kulipwa na mshahara wenyewe kuwa duni. Kwa hivyo, kifo kinachotokana na njaa kimesababishwa na wananchi wa kawaida wa Cheneo kuwachagua viongozi wasiofaa. Ili kuthibitisha kuwa njaa inawaangamiza Wanacheneo, Siki anamweleza Meya kuhusu kitoto kilichofia mikononi mwake siku iliyotangulia. Meya hashtuliwi na kifo cha kitoto hicho, badala yake anasema, “Huyo mmoja tu? Unadhani wangapi wananiunga mkono? Cheneo ina watu wangapi?” (Arege,2009: 12).

Matamshi yake Meya yanadhihirisha kutojali kwake kutokana na kiburi cha uhakika wa kuchaguliwa tena kwa sababu amechaguliwa tayari mara tatu licha ya shida hizo na wananchi wale wale wanaolalamika kuhusu shida zinazosababishwa na uongozi wake. Kutokana na kiburi alichopewa na wananchi wa kawaida waliomchagua, hashughulikii shida zinazowakumba kimakusudi hivyo kusababisha vifo.

Katika hali ya kutetea uongozi wa baraza la Cheneo, madiwani hutumia nguvu kupita kiasi dhidi ya wananchi wanaoupinga hasa kwa kuandamana na kugoma. Wananchi wa kawaida huupinga uongozi wa Meya na baraza lake kwa sababu umeshindwa kubuni nafasi za kutosha za kazi, walio na kazi hulipwa mshahara mdogo ambao haulipwi kwa wakati, hali ngumu katika mazingira ya kazi, ukosefu wa dawa hospitalini na njaa. Lakini kulingana na viongozi wa Mji wa Cheneo, haya ni madai tu kwa sababu mji wa Cheneo umepiga hatua kimaendeleo na wanaogoma au kuandamana ni wachochezi ambao sharti wakomeshwe. Wanapowakomesha, polisi ambao hufuata amri za wakuu wao huwaumiza na wakati mwingine kuwaua waandamanaji ambao ni wananchi wa kawaida. Jambo hili linajitokeza katika mazungumzo kati ya Meya na Diwani wa Kwanza:

> **Diwani 1**: Mstahiki Meya kitengo changu mimi hakina shida. Ni kuwaamrisha vijana wetu wa usalama kulinda Baraza.
>
> **Meya:** Mara hii sitaki kusikia mtu amekufa. Mwaka wa kuomba kura utakapofika sitataka mizuka yao kuniandama. Itaniletea tatizo wakati wa uchaguzi.
>
> **Diwani 1:** Nitawaambia kutembeza virungu kiasi cha kuwafanya kutulia nyumbani. (Arege, 2009: 19).

Mazungumzo haya yanafanyika katika ofisi ya Meya baada ya kuwaita madiwani ili kutafuta suluhu kwa wasioridhika na uongozi wao. Mazungumzo haya yanadhihirisha kuwa hapo awali katika harakati ya kuwanyamazisha waliopinga uongozi wao, kuna mtu aliwahi kufa. Kitendo cha viongozi cha kuwaua wananchi wa kawaida wanapojaribu kujieleza ni cha kidhuluma lakini wanaosababisha dhuluma hii dhidi yao wenyewe ni wananchi wa kawaida kwa kuwachagua viongozi wabaya licha ya kufahamu uovu wao.

Katika upande mwingine, tamthilia ya *Amezidi* (1995), imetumia jazanda kuonyesha jinsi ambavyo Bara la Afrika lina shida nyingi licha ya kuwa na utajiri mkubwa kutokana na kuwepo kwa ardhi yenye rutuba na madini kama almasi, shaba na makaa. Shida hizi zinajumuisha magonjwa na njaa na zimekithiri kutokana na ujinga, mapuuza na hata ufisadi walionao wananchi wa kawaida wanaowakilishwa na Ame na Zidi. Mapuuza, ujinga na uvivu kama njia moja ya kujidhulumu unasababisha kifo ambacho ni athari ya dhuluma. Kwa mfano, redio inatangaza kuwa katika kijiji cha Fujo, maelfu kwa maelfu ya watu wanakufa kwa njaa kila siku na sababu ni ukame. Mvua hazijanyesha kwa miaka mingi na Umoja wa Mataifa unaandaa misaada. Janga hili linatokana na ile dhana kuwa Afrika ni Bara tajiri na halina haja ya kufikiri kuhusu mbinu za kisasa za kilimo kwa sababu linaweza kuwalipa watu wengine walifikirie. Ndiposa mwanafunzi anasema:

> ... ni kwamba tu matajiri; na tajiri hana haja ya kufikiri,
> anaweza kuwalipa watu wengine wamfikirie, wamfanyie

> utafiti, wamvumbulie... Sisi matajiri tunapenda njia ya mkato ... tunapokea, badala ya kufikiri, watu wanafikiri kwa niaba yetu; badala ya kuvumbua tunavumbuliwa ... badala ya kuunda tunaundiwa... (Mohamed, 1995: 32- 33).

Hili ni jibu analotoa mwanafunzi kuhusu sababu za kutounda nyambizi baada ya kukariri mawazo ya Mwanasayansi Archimides kwa miaka mingi. Fikra hizi kuwa hakuna haja kufikiri ni fikra za kizembe na kijinga na zinachangia kutokuwepo kwa juhudi zozote miongoni mwa wananchi wa kawaida za kutatua shida zinazowakumba katika Bara la Afrika. Janga kama la njaa ambalo linasababisha kifo lingeepukwa ikiwa Waafrika wangefikiri jinsi ya kulima hasa kwa kuzingatia mbinu za kisasa za kilimo kama vile matumizi ya trekta na mbolea. Badala yake, wanatumia viserema na samadi ya ng'ombe kama mbolea.

Zidi, Ame na majirani zake wanakufa kutokana na kipindupindu pia na msaada wa nyama ya EC. Msaada wa nyama kutoka EC ni mbovu na kutokana na kutojali kwao na uvivu, wanakubali misaada ambayo hahitajiki katika nchi zilizoendelea. Nchi zilizoendelea zinatumia Afrika kama jaa la bidhaa wasizohitaji kama nyama inayosababisha kifo cha Zidi, Ame na jirani zao ambao wanawakilisha wananchi wa kawaida. Misaada ni mbinu wanayoitumia kuwahadaa Waafrika kuwa hao ni rafiki na wanaweza kuwasaidia katika kila hali. Lakini ujinga umewafunga macho na akili Ame na Zidi wasione kuwa ni njama ya kuwafanya wavivu ili washawishike kwa urahisi kuwapatia malighafi yao. Wanapokubaliana na nchi zilizoendelea bila kugundua njama zao, wanajidhulumu kwa kujisababishia kifo kutokana na misaada yao yenye sumu.

Aidha, Ame na Zidi kama wananchi wa kawaida wanajisababishia kifo kwa kukubali mfumo wa elimu ambao huwasaidii kutatua shida zinazowakumba kama vile njaa na magonjwa. Wanafunzi wa Kiafrika hukariri tu mawazo ya wataalamu kutoka nchi zilizoendelea lakini hawawezi kuunda wala kubuni chochote cha kuboresha maisha yao. Ndiposa Zidi na Ame hawana ujuzi wa kuichunguza misaada kutoka EC ili kutathimini ubora wake kabla ya kuitumia. Kutokana na ukosefu wa maarifa, Zidi anakufa kwa kula msaada wa nyama mbovu kutoka EC.

3.3 UMASKINI

Tamthilia ya *Kilio Cha Haki* (1981) inabainisha umaskini katika wimbo wa wafanyakazi waliogoma kwa sababu ya unyonyaji na udhalimu uliozidi shambani. Wanalalamika kwa kulemewa na mzigo wa maisha kwa kuwa hawana maisha mazuri kama vile nyumba nzuri hata kama wanafanya kazi. Hali hii inadokeza kuwa, japo wanafanya kazi, mishahara yao ni midogo na haiwasaidii kugharamia mahitaji muhimu hivyo kuwaletea umaskini inavyojitokeza katika sauti zao:

Sauti za wafanya kazi

Mimi niliyekuwa nikiteswa kama fahali
Nikawa silalamiki, kimya kama jabali
Kwa nini..
    Mimi kulemewa na mzigo wa maisha
    na kudidimizwa kwa uzito wa wakati
Kwa nini...
    Matunda ya jasho linitokalo kwa dhati
    kuwa sumu chungu inileateayo mauti
Kwa nini...
    Hii mikono majuruhi ijengeayo umati
    Kuniacha nje nikilalia simiti
Kwa nini eee
Kwa nini eee
Eee... nimeshazinduka (Mazrui, 1981: 7).

Hapa wafanya kazi kama wananchi wa kawaida wanadokeza hali yao ya umaskini ambayo wamejisababishia wenyewe kwa kumruhusu mdhulumu wao kuwatesa bila kulalamika. Miongoni mwa mateso waliyojipatia ni kulemewa na mzigo wa maisha ambayo ni ishara ya umaskini kutokana na mshahara duni. Kwa hivyo, hawana uwezo wa kuwa na nyumba nzuri na chakula bora. Kutomudu mahitaji ya kimsingi umesababishwa na unyonyaji na udhalimu uliozidi shambani ambapo wafanyakazi wanafanya kazi nyingi kwa muda mrefu lakini faida na mshahara mkubwa unachukuliwa na Bwana Delamon na kuwafanya wafanyakazi kuwa na uhitaji usio kikomo. Ndiposa Lanina anamwambia Delamon kuwa,

> ... Nyinyi hamkuja hapa kwa manufaa yetu, hamkuja hapa kwa maendeleo ya nchi yetu. Mmekuja kutudhulumu tu kutumia nguvu zetu, kutunyang'anya ardhi yetu, kuinyonya nchi yetu kwa gharama ndogo isiyokuwa na thamani (Mazrui, 1981: 13).

Kinaya ni kuwa, licha ya kufahamu kuwa Delamon hakuja kwa maendeleo ya nchi yao, bado Lanina na wafanyakazi wenzake wanamfanyia Delamon kazi kwa muda mrefu bila kulalamika. Kwa hivyo umaskini wao Lanina na wafanyakazi kama wananchi wa kawaida unasababishwa na wao wenyewe.

Labda ni kutokana na umaskini ndiposa Tereki anashawishika kuwa kiongozi wa chama cha wafanya kazi anachokianzisha Delamon ili kutetea maslahi yake. Tereki anapewa ahadi ya manufaa mengi ambayo bila shaka ni mshahara mkubwa ukilinganishwa na wa wafanyakazi wenzake ila tu afahamu jinsi ya kuwaongoza wenzake kulingana na sera za Delamon. Ujuzi anaohitaji kuwa nao Tereki ni wa kuwadhulumu wenzake kwa manufaa yake na ya Bwana

Delamon. Anahitaji kumwongezea Delamon pato kwa kuhakikisha wanafanya kazi zaidi, kwa muda mrefu na kwa malipo duni huku akipuuza malalamishi yao. Bila shaka mpango wake Tereki kama mwananchi wa kawaida ni wa kuwafanya wenzake kuwa maskini. Ndiyo maana Shindo anamwambia Tereki kuwa, "Ukijua namna ya kuwaongoza wafanyakazi wenzako, basi utapata manufaa makubwa kazini," (Mazrui, 1981: 17). Manufaa anayoyarejelea Shindo bila shaka ni cheo ambacho kinaandamana na ongezeko la pato la kumfaidi yeye na jamii yake. Uhitaji mkubwa wa Tereki hadi kufikia kiwango cha kuwasaliti wenzake unachochewa na mshahara duni aliolipwa. Harakati ya Tereki kuongeza pato la shamba bila kuwajali wafanyakazi wenzake ni kitendo cha kidhuluma. Anasababisha umaskini miongoni mwa wafanyakazi kwa sababu chini ya uongozi wake, wafanyakazi waliongezwa pesa lakini muda wa kufanya kazi nao ukaongezwa hivyo hali ya umaskini kubaki licha ya nyongeza hiyo ya mshahara.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* (2009), umaskini kama athari ya dhuluma unajitokeza kwa njia mbalimbali. Mwanzo, ni pale ambapo wananchi wa Cheneo hawana pesa za kulipia huduma za kimsingi kama vile matibabu kwa sababu ya kutotafuta kazi nyingine zaidi ya ile ya mji wa Cheneo ambayo malipo ni duni. Tunaambiwa kuwa wananchi wanapoenda zahanatini, hawana pesa za kununua hata karatasi ya kunakilia maelezo kuhusu ugonjwa wao. Sababu inayotolewa kuhusu ukosefu huu ni kuwa nchi ni maskini. Lakini ukweli ni kuwa wananchi wa kawaida kama vile wafanyakazi na viongozi wao

waliendelea kuwachagua viongozi wabaya na kushuhudia wakiufilisi mji kwa ufisadi bila kuwakashifu. Kwa mfano, Meya anatumia pesa za umma kuwapeleka watoto wake ng'ambo kusomea huko. Isitoshe, ananyakua ardhi ya umma kwa matumizi yake binafsi:

> **Meya:** ... mimi nimeuza vipande vyangu vitatu vya ardhi kupata pesa kwa ajili hii. Nimebakiza vitano *incase* . Wewe nilikugawia vine. Unaweza kuuza kimoja au viwili kwa ajili hiyo. Vingine viweke kwa ajili ya hao watoto unaowahangaikia, hasa ile *prime plot* (Arege, 2009:27).

Hapa Meya anamweleza mshauri wake Bili alikotoa pesa za kumpeleka mke wake ng'ambo kwa matibabu. Ardhi ya umma waliyoinyakua ingeweza kutumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kama vile kuitenga kwa ujenzi wa viwanda au kilimo ambavyo vingewapa wananchi ajira ambayo ingeimarisha maisha yao lakini hatuoni wananchi wenyewe wakiuangazia uovu huu.

Aidha wafanya kazi wa baraza ambao ni wawakilishi wa wananchi wa kawaida ni maskini kwa kuwa hawawezi kumudu gharama ya chakula bora. Kwa mfano, mamake Dadavuo Kaole anamlisha wali na maharage yalolala kwa sababu ya kukosa hela za kununua makaa ya kukitokosa kwa kuwa mshahara wake ni mdogo na haulipwi kwa wakati licha ya kuwa anafanya kazi kwa Meya. Mama amejisababishia ufukara huu kwa kwendelea kufanya kazi kwa Meya ilhali mshahara ni duni. Vilevile, anajidhulumu kwa kutong'amua umuhimu wake katika maisha na uongozi wa Meya ili autumie kuitisha nyongeza ya mshahara ili kujiondoa kwenye lindi la umaskini.

Wananchi wa kawaida wakiwemo wafanyakazi wanawachagua viongozi wasiowajali hivyo kuwasababishia umaskini. Kwa mfano, japo baraza lina

upungufu wa pesa, Meya anaamrisha walinda usalama waongezwe mshahara na madiwani wasitozwe kodi. Kodi ni muhimu katika kuimarisha uchumi wa nchi kwa sababu ndiyo hutumiwa kuwalipa wafanyakazi mishahara na kuboresha miundo misingi ikiwemo kuhakikisha uwepo wa dawa hospitalini. Madiwani wanapokataa kutozwa kodi wanadhihirisha ubinafsi na usaliti kwa waliowachagua na ina maana kuwa utoaji wa huduma muhimu kama ulipaji wa mishahara hulemazwa kwa sababu pesa hupungua. Upugufu huu husababisha wafanyakazi ambao ni wananchi wa kawaida kulipwa mshahara mdogo na wakati mwingine huchelewa. Haya ni baadhi ya yanayowakumba Wanacheneo waliojifanya maskini kwa kuwachagua viongozi wasiowajali licha ya kufahamu hivyo kutokana na chaguzi za hapo awali. Isitoshe, walimchagua kiongozi dikteta ambaye hataki kusikiliza ushauri unaonuia kuwanufaisha wananchi wa kawaida waliomchagua. Ndiposa Meya anaposhauriwa na Diwani wa Tatu kuwa mwananchi wa kawaida hajanufaika na hata wafanyakazi hawalipwi kwa wakati anasema, “Tusipoteze muda mwingi. Ndiyo hayo. Umeyasikia Bwana Uchumi na kazi. Sawasawa?” (Arege, 2009: 23). Msimamo wake Meya ni wa kidikteta ambao unachangia umaskini katika maisha ya wananchi wa kawaida kutokana na maamuzi yake mabaya ya kiuchumi. Kutokana na ushauri mbaya wa Bili, Meya anapanga korti imlipe mwanakandarasi fidia baada ya Meya kuisimamisha kandarasi yake bila kufuata utaratibu unaofaa. Kisha akubaliane naye fungu atakalompa baada ya baraza kumlipa. Mpango huu ni hatari kwa uchumi wa Baraza la Cheneo ambalo tayari halina pesa za kutosha kuwaajiri Wanacheneo waliohitimu,

kuwalipa mishahara ya kutosha na kwa wakati ufaao na kuwapatia huduma za kimsingi kama vile afya. Hatari ya kiuchumi iliyoko ni kuwa Baraza litalipia huduma ambazo hazikutolewa hivyo kubakisha hela chache kwa maendeleo ya mji wa Cheneo. Ndiposa sauti za wanacheneo zinasikika zikisema:

> **Sauti:** Mstahiki Meya tusikie
> Sikiliza sauti zetu zinazokulilia
> Zikidai haki kufanyiwa.
> Maslahi bora ni haki yetu
> Malipo bora ni haki ya mfanyakazi
> Huduma za afya ni haki yetu
> Tumechoka kudhalilishwa
> Na daima kupuuzwa
> Tunataka kusikilizwa
> Na maslahi yetu kuangaliwa (Arege, 2009: 30).

Sauti hizi za wananchi wa kawaida zinalalamikia maslahi bora ambayo hayapo kutokana na umaskini unaosababishwa na ufisadi miongoni mwa dhuluma zingine walizojisababishia wafanyakazi kama wananchi wa kawaida kwa kumchagua kiongozi dikteta.

Aidha, tamthilia ya *Amezidi* nayo imeonyesha umaskini kama athari ya dhuluma ifuatavyo: mwanzo, baada ya Zidi kugundua kuwa mhogo alioung'oa ni wa mwisho na mvua haijanyesha mwaka mzima, Ame anamuuliza ikiwa ameshapeleka maombi ya msaada huko Umoja wa Mataifa au kuomba ruzuku nchi za Magharibi yaani EC. Misaada wanayoipata kama wananchi wa kawaida imewapumbaza kisaikolojia kufikia kiwango cha kuwa wazembe hivyo kukosa kutia bidii ili kujitegemea katika kiwango cha vyakula. Umaskini huu unatokana na urafiki wa nipe nikupe kati ya nchi za Afrika na nchi za Magharibi ambako Waafrika hupokea bidhaa za thamani ya chini kama vile

dawa na nyama ambayo hahitajiki katika nchi zilizoendelea. Katika kuendeleza urafiki huu, nchi za Magharibi huchukua bidhaa za thamani ya juu kama vile dhahabu na almasi. Mataifa haya huunda mali ya thamani ambayo nchi za Afrika hununua kwa bei ghali kwa kutumia pesa za nchi za magharibi ambazo zina thamani kubwa kuliko pesa za Afrika. Hali hii ya kununua bidhaa kwa bei ghali na kwa pesa za kigeni husababisha umaskini katika nchi zinazoendelea kwa sababu ya kutotia bidii. Lakini Ame na Zidi ambao wanawakilisha wananchi wa kawaida hawaoni jinsi utajiri wao wa malighafi unavyoweza kuwasababishia umaskini hasa wanapoutumia kumtuma mtu mweupe kuwafikiria, kuwavumbulia, kuwaundia na kuwajaribia. Wanajisababishia umaskini kutokana na ujinga. Wasilolijua ni kuwa mtu mweupe ndiye anayepata manufaa ambayo wangeyapata ikiwa wangetia bidii na kutumia utajiri wa malighafi waliyonayo inavyojitokeza katika wimbo ufuatao:

Tajiri kasimama
Kasimama kwa maguu yake
Hana anacho!
Anacho hana!
Kope si zake
Kope ni zake
Kasimama kwa maguu yake
Kwenye mgongo wake mwenyewe
Magondi yake marefu na mwili wake mzito
Kasimama huku kalala
Kalala yu macho!
Au yu macho kalala!
Ndani ya tumbo lake mna makaa
Mna makaa ya mawe
Ndani ya tumbo lake mna almasi
Almasi ya thamani
Ndani ya tumbo lake mna dhahabu
Mabonge, mabonge ya dhahabu...
Tajiri kashiba
Ndiyo maana kalala
Ashibaye hulala
Huku wengine humpakuwa (Mohamed, 1995: 33 – 34).

Wimbo huu unabainisha utajiri walio nao Waafrika lakini bado wanakumbwa na umaskini kwa sababu ya kuwaachia wengine jukumu la kutumia mali hiyo kujitajirisha huku Waafrika wakinufaika kwa kiwango kidogo hasa kwa misaada.

3.4 UTENGANO WA KIJAMII

Utengano wa kijamii kutokana na dhuluma unabainika pale ambapo watu waliokuwa pamoja kikazi au kifamilia huachana hasa kikundi kimoja kinapojihusisha na watawala dhalimu na kuendeleza mbinu zao za kidhalimu. Aidha, wananchi wanaweza kujitenga na aila zao kwa kutoroka au kuhama kutoka kwa mazingira ambayo ni magumu kufanya kazi au kuishi kutokana na dhuluma. Wakati mwingine dhuluma husababisha uhasama ambao huchochea vita miongoni mwa wananchi hivyo kuwatenganisha zaidi. Kwa mfano, tamthilia ya *Kilio cha Haki* (1981) inabainisha utengano kati ya Lanina na wasaidizi wa Bwana Delamon ambao ni wananchi wa kawaida ila tu walijiunga na mdhulumu wao kwa sababu ya ubinafsi inavyobainika katika mazungumzo yafuatayo:

> **Lanina:** Tafadhali tusipoteze wakati. Nashindwa kufikiri ni jambo gani kubwa hivyo la kuwajaza hofu namna hiyo. Siku nyingi tumefanya kazi pamoja, kwa nini sasa mnaogopaogopa namna hii? Semeni tu! Mlilonalo lolote semeni!
>
> **Pelekha:** Aaa ... unajua Lanina ... Delamon yuko ...yuko tayari kukurudisha kazini.
>
> **Lanina:** Kumbe! Kumbe mmekuja hapa kunishawishi niungane nanyi katika kuwasaliti wafanyakazi wenzetu! Tereki!

Hata wewe Tereki! ... (Mazrui, 1981:51)

Pelekha, Tereki na Matovu wanaungana na Bwana Delamon kuwanyanyasa wafanyakazi wenzao na wanajaribu kumshawishi Lanina aungane nao ili kuendelea kuongeza faida kwa shamba lake japo hawalitambui hili. Lanina anatengana nao kwa kutokubaliana na mtazamo wao. Kisha anawafukuza kwa sababu wanashirikiana na Bwana Delamon ambaye huwalipa wafanyakazi mshahara mdogo na huwaita askari ambao huwachapa na kuwaumiza wafanyakazi wanapogoma. Mwishowe Tereki na Shindo wanauawa na wafanyakazi wenzao kwa sababu ya kushirikiana na aliyewasababishia dhuluma nyingi yaani Bwana Delamon.

Aidha dhuluma inasababisha utengano wa kijamii ambapo wanafamilia huachana kwa kulazimishwa na wanaoendeleza dhuluma au hujiunga na vyombo vya dhuluma kwa hiari kutokana na ubinafsi wa kujitakia makuu bila kuwajali wenzao. Mathalan, Lanina anashikwa kwa makosa ya kuwachochea wafanya kazi, anafungiwa gerezani kwa wiki kadhaa na kuteswa kwa kupigwa na mwishowe kuwachiliwa bila kufunguliwa mashtaka. Hapa vyombo vya usalama kama vile askari na gereza vimeruhusiwa na wananchi wa kawaida kuwadhulumu wananchi wenyewe hasa wafanyakazi kwa kuwatenganisha na wapendwa wao kama inavyobainika Lanina anaporudi kutoka kizuizini:

> **Mwengo:** Lanina! Lanina! Wewe unajua siku ngapi sasa umeniweka bila ya usingizi. Unajua siku ngapi sasa watoto wanakula chakula kibichi? Wewe! wewe ...
>
> **Lanina:** Hebu Mwengo poa kidogo kwanza tafadhali. Utawamsha watoto. Poa tuweze ...
>
> **Mwengo:** Nipoe! Mimi nipoe! Wewe mwanamke una kichaa wewe!

> Wewe si mzima wewe! Umeniweka wiki zote hizi na wasiwasi halafu ... unaniambia nipoe. Unafikiri mimi jiwe wewe ... sina hisia! (Mazrui, 1981: 29)

Bila shaka Mwengo hafurahii utengano kati yake na mke wake Lanina kwa siku kadhaa kwa sababu majukumu yanamzidi na zaidi ya yote, anakuwa na wasiwasi mwingi kuhusu hali ya Lanina ambao unamkosesha usingizi. Hata hivyo, si mapenzi yake Lanina kumwacha mume wake bali mume wake na baadhi ya wafanyakazi wamekataa kuungana na Lanina ili kukemea na kukomesha utengano wa kijamii unaoletwa na wadhulumu hasa kwa kutofuata sheria. Vilevile, dhuluma imesabisha utengano kati ya Lanina na Babake. Lanina anaposhirikiana na wafanyakazi wenzake kupigania haki za wafanyakazi zilizokiukwa na Bwana Delamon, babake hafurahii kwa sababu harakati zake zinasababisha kukamatwa kwake. Kulingana na babake Lanina, harakati za kupigania haki ni shughuli za wanaume na mwanamke anayeshirikiana nao ni malaya na mwacha mila. Kwa hivyo, anamkana Lanina kuwa mtoto wake na kumtusi. Hali ingekuwa shwari yaani wafanyakazi wangekuwa wanalipwa mishahara bora na mazingira ya kazi kuwa salama, basi Lanina hangeshiriki upiganiaji wa haki za wafanyakazi. Angebaki nyumbani kutekeleza majukumu yake inavyostahiki kulingana na utamaduni. Pia, Mzee Seromanga na Mwengo kama wananchi wa kawaida wangeshiriki katika harakati za kupigania haki basi Lanina angebaki nyumbani kuichunga na kuitunza familia. Lakini wanapojitenga na utetezi wa haki wanajidhulumu kwa kuwacha mwanya ambao anauziba Lanina kinyume na utamaduni na kuwafanya wachekwe na kuachiwa majukumu ya nyumbani. Lanina anapoenda kinyume na matarajio ya utamaduni, anatengana na babake.

Utengano kama athari ya dhuluma pia unabainika katika tamthilia ya *Mstahiki Meya.* Hapa kuna utengano unaotokana na mazingira magumu ya kufanyia kazi au baadhi ya wafanyakazi kutoridhika na matokeo ya kazi zao. Hali hii inatokana na ukosefu wa miundo misingi ya kuboresha mazingira ya kazi kwa sababu ya uongozi mbaya unaosababishwa na ubinafsi, uongo na ufisadi. Katika upande mwingine, utengano umesababishwa na tofauti za kimtazamo kuhusu hali halisi ya mambo katika mji wa Cheneo kati ya watawala na watawaliwa au miongoni mwa watawala wenyewe. Kwa mfano, Waridi kama mwananchi wa kawaida anaiwacha kazi ya uuguzi kwa sababu ya kufanya kazi katika mazingira magumu ambamo hamna dawa na maji. Matokeo yake ni kuwa watu wanakufa akiwatazama. Hali hii inamfanya ajihisi mtu asiye na umuhimu wowote kwa Wanacheneo ndiposa anaona ni bora ajitenge na kazi kwa sababu ya kujidhulumu kwa kushawishika haraka na kukubali uongo wa Meya kuwa dawa zi njiani. Japo Meya na Siki ni ndugu wanatengana. Utengano huu unasababishwa na Meya anapohisi kuwa Siki hathamini uongozi wake anapomweleza kuwa watu waliomchagua kwa imani kuwa angeziboresha hali zao wana shida. Uongozi wa Mstahiki Meya unawadhulumu kwa kupandisha hali ya maisha ilhali mishahara haipandi inavyobainika Wanacheneo wanaposhindwa kumudu gharama za matibabu. Siki anapojaribu kumjuza haya kama ndugu yake na kuwa ni hatari kuwaongoza watu wenye matatizo yanayosababishwa na baraza, anaona kuwa

haheshimu uongozi wake na badala yake anamwita mlinzi wake amwondoe Siki:

> **Meya:** Mwondoe huyu hapa mara moja! Hakikisha mtu huyo halikaribii lango kuu kuanzia sasa. Jengo langu alione paa. *Alright?*
>
> **Gedi:** *Yes sir* (Arege, 2009: 15)

Mazungumzo haya yanabainisha chuki na utengano kati ya Meya na Siki kutokana na hali halisi ya jinsi Wanacheneo wanavyodhulumiwa ambayo Meya hakubaliani nayo. Siki anawakilisha wananchi na wafanyakazi wa kawaida ambao wanadhulumiwa na uongozi mbaya wa Meya. Aidha, Diwani wa Tatu hawapatani kuhusu hali halisi ya kiuchumi katika Mji wa Cheneo. Diwani wa Tatu hafurahishwi na jinsi Meya, Diwani wa Kwanza na wa Pili wanavyoliendesha Baraza kiuchumi. Meya anapendekeza madiwani wasilipe kodi ilhali mfanyabiashara wa kiwango cha chini kama mama muuza ndizi analipa kodi ili kuchangia kulijenga taifa. Licha ya hayo, Baraza lina naksi ya shilingi milioni mia moja ishirini, watu wengi hawana ajira na walio na ajira mishahara yao haitoshi wala hailipwi kwa wakati. Meya, Diwani wa Kwanza na wa Pili wanapogundua kuwa Diwani wa tatu hawaungi mkono katika mipango yao ya kulifilisi baraza, wanamtenga katika baadhi ya maamuzi na kumlazimisha kukubaliana nayo baadaye.

Isitoshe, kuna utengano kati ya nchi zilizoendelea na nchi za Afrika katika kiwango cha kiuchumi inavyobainika katika tamthilia ya *Amezidi*. Utengano huu ni wa kimakusudi na unaendelezwa na misaada wanayoipokea Waafrika

kutoka nchi zilizoendelea. Kulingana na Waafrika, kupata misaada hasa wanapokumbwa na shida ni ishara ya mapenzi na urafiki mkubwa. Ndiyo maana wanawaruhusu wachukue malighafi yao ambayo wanaitumia kuendeleza chumi zao huku Waafrika wakiendelea kuwa wahitaji licha ya kuwa na madini kama almasi na dhahabu miongoni mwa madini nyingine. Utengano huu wa kiuchumi umewasababishia Waafrika majanga mengi kama vile njaa na ukame ambayo yangedhibitiwa ikiwa Waafrika wangetumia utajiri wao wa madini mbalimbali. Waafrika wanajidhulumu na nchi zilizoendelea wanapoziuzia malighafi yake kwa bei ya chini na kisha kuuza bidhaa itokanayo na malighafi hiyo barani Afrika kwa bei ghali na kupunguza kiwango cha hela kinachoweza kutumika katika miradi mingine ya kuleta maendeleo. Hata hivyo, Waafika hawang'amui hili, uwepo wa malighafi na madini aina mbalimbali ambayo hawaitumii kuunda mali ni ithibati tosha kuwa wao ni matajiri inavyojitokeza mwanafunzi anaposema,

> .. Sisi matajiri tunapenda njia ya mkato ... tunapokea, badala ya kufikiri, watu wanafikiri kwa niaba yetu; badala ya kuvumbua tunavumbuliwa ... badala ya kuunda tunaundiwa, badala ya kujaribu tunajaribiwa ... tunanunua mali tayari. Hiyo ndiyo njia ya mkato. Maadamu fedha tunazo ... mashekhofu ... mashekhofu... tena nini? Wacha tumtume mtu mweupe. Yeye alitutuma siku nyingi, au siyo? (Mohamed, 1981: 33).

Inabainika wazi kuwa Waafrika ni wazembe na hutumia pesa nyingi kuagizia bidhaa kutoka kwa nchi zilizoendelea. Pesa ambazo wangeziokoa ikiwa wangetumia malighafi yao kuzalisha mali badala ya kuwauzia watu weupe malighafi yiyo hiyo na kisha kununua bidhaa itokanayo nayo kwa bei ghali na kwa sarafu ya kigeni ambayo thamani yake ni kubwa. Kasumba hii kuwa

Waafrika ni tajiri pamoja na uzembe walionao umeongeza mwanya kati ya chumi za Afrika na nchi zilizoendelea.

3.5 HITIMISHO

Lengo la sura hii lilikuwa kuonyesha athari zinazotokana na dhuluma dhidi ya mwananchi wa kawaida. Athari zilizobainishwa ni kifo, umaskini na utengano. Kifo kama athari ya dhuluma kilifafanuliwa kwa kuangazia matendo ya wananchi wa kawaida ambayo yaliwasababishia kifo moja kwa moja au yalichangia kifo kwa njia moja au nyingine. Kwa mfano, kuna vifo vilivyosababishwa na njaa, ukosefu wa dawa hospitalini na uzembe miongoni mwa wananchi wa kawaida. Kwa upande mwingine, umaskini hasa kwa wananchi wa kawaida umesawiriwa kama athari ya dhuluma kupitia kwa njia wananchi wa kawaida wanavyoishi na uhitaji mkubwa. Japo wengine wameajiriwa, hawana uwezo wa kununua chakula bora, dawa, kuwalipia watoto wao karo na hata kuishi katika nyumba nzuri. Uchochole huu unatokana na uzembe wa wananchi wenyewe na kuruhusu ufisadi miongoni mwa viongozi. Mwisho ni athari ya utengano na uhasama. Athari hii imebainishwa kwa kurejelea kubomoka kwa mahusiano kati ya watu wa familia moja au miongoni mwa wafanyakazi ambao wanawakilisha wananchi wa kawaida. Mahusiano haya yamebomoka kwa sababu ya kujidhulumu kupitia ubinafsi miongoni mwa wananchi wa kawaida wenyewe. Utengano huu huwa njia ya kutoroka kutoka kwa wadhulumu au kujiunga nao kutokana na kujitakia makuu.

Athari zinazotokana na dhuluma dhidi ya mwananchi wa kawaida zimejikita kwenye mhimili wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Mhimili huu huonyesha hutekelezaji wa matendo kitabaka. Tabaka la chini ambalo linawakilishwa na wananchi wa kawaida lina mahitaji makubwa kiuchumi kwa sababu ya kufanya kazi duni hivyo kuendeleza umaskini. Wananchi wa kawaida pia wameshiriki katika kupinga uongozi usiofaa na kusababisha uhasama kati yao na wenzao wasiowaunga mkono.

Sura itakayofuata italenga kubainisha mikakati anayoweza kuitumia mwananchi wa kawaida kuepukana na dhuluma dhidi yake kwa mujibu wa tamthilia zilizoteuliwa.

SURA YA NNE

4.0 MIKAKATI YA MWANANCHI KATIKA KUZUIA DHULUMA DHIDI YAKE

4.1 UTANGULIZI

Katika sura ya tatu, utafiti umeshughulikia athari zinazotokana na dhuluma dhidi ya mwananchi wa kawaida. Athari zilizobainishwa ni kifo, umaskini na utengano. Kifo kilishughulikiwa kwa kuangazia baadhi ya wananchi wa kawaida waliopoteza maisha yao kutokana na matendo yao kama vile kuwachagua viongozi wasiowajali. Kwa upande mwingine, umaskini ulisawiriwa miongoni mwa wananchi wa kawaida kupitia ukosefu wa chakula miongoni mwa mahitaji mengine ya kimsingi. Mwisho, utengano ulibainishwa kama athari ya dhuluma kupitia kwa mahusiano ya uhasama miongoni mwa wananchi wa kawaida hasa kupitia ukinzani kati ya wananchi waliojiunga na wadhulumu kutokana na ubinafsi na wale waliosimama kidete kupigania haki zao. Katika sura hii, utafiti unapania kuonyesha baadhi ya mikakati anayoweza kuiweka mwananchi wa kawaida ili kuzuia dhuluma dhidi yake. Mikakati hii imefasiliwa kwa mujibu wa nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa ambapo wananchi wananuia kubadilisha hali yao ya maisha. Kutokana na usomaji wa kina uliopendekezwa na watafiti wengine kama vile Gitau (2005) na wa tamthilia teule, zifuatazo ni mbinu zilizopendekezwa kutumiwa na mwananchi wa kawaida ili kukomesha au kupunguza dhuluma dhidi yake:

4.2 KUWACHAGUA VIONGOZI BORA

Kiongozi bora ni yule anayeonyesha jinsi ya kuhusiana na kushiriki na watu wengine katika mazingira yanayoongozwa na taratibu fulani ambazo ni maadili ya uongozi. Uongozi bora ni uongozi unaotumikia wanawake na wanaume, maskini na matajiri na wenye madaraka na wanyonge, ni ule unaoshirikisha watu wote. Uongozi huu hujiepusha na fikira potovu ambazo huwaona baadhi ya watu au baadhi ya tabaka za watu kuwa na haki au mamlaka ya kuzaliwa ya kufanya maamuzi kwa ajili ya watu wengine. Badala yake, uongozi unapaswa kujihusisha na kuleta pamoja na kuyafanyia kazi maoni, vipaji na ujuzi wa watu wengi kadri inavyowezekana na inavyostahili katika sehemu inayohusika. Zaidi ya hayo, ujuzi katika uongozi hauwezi kutenganishwa na ujuzi katika mahusiano na watu kwa vile utendaji mwema na ufanisi wa kiongozi unategemea kiwango cha juu cha ushirikiano alionao kati yake na washirika (Bwenge, 2013). Ili nchi na wananchi waendelee hasa katika viwango vya kiuchumi, sharti wananchi hasa wa kawaida ambao ndio wengi wawachague viongozi bora watakaowashirikisha katika uongozi. Viongozi bora wataweka sera madhubuti za kuinua viwango vya kiuchumi na wataheshimu haki za kibinadamu miongoni mwa mambo mengine ambayo yanatoa msingi bora wa maendeleo. Uongozi bora ambao hutokana na viongozi bora huweka misingi ya maisha bora na kuhakikisha uzalishaji wa nafasi za kazi, chakula, amani na heshima kwa haki za kibinadamu. Kwa kijumla, uongozi bora huboresha maisha ya wananchi katika kila sekta ya maisha yao. Katika kuhakikisha haya, wananchi wana jukumu la kuhakikisha kuwa wanawachagua viongozi wema

ambao wataendeleza azma yao ya maisha mazuri. Hata hivyo, wananchi hasa wa kawaida huwachagua viongozi wabaya hata baada ya viongozi hao kuonyesha dalili za ubaya kabla ya kuchaguliwa. Mwishowe viongozi hawa huwasaliti wananchi kwa kuyafanya maisha yao kuwa mabaya na hivyo kuchangia dhuluma dhidi yao kwa kuwachagua viongozi wabaya inavyobainishwa katika tamthilia teule za *Kilio Cha Haki*, *Mstahiki Meya* na *Amezidi*.

Kwa mfano, katika tamthilia ya *Kilio cha Haki*, wawakilishi wa wafanya kazi waliochaguliwa na wafanya kazi wenyewe ambao ni wananchi wa kawaida hawatekelezi wajibu wao wa kuwatetea wafanya kazi. Kinyume na wao, Lanina amesawiriwa kama mhusika ambaye alistahili kuchaguliwa kuwa mwakilishi bora wa wafanya kazi kwa sababu anaonekana kuyafahamu mahitaji ya wafanya kazi kuliko wawakilishi waliochaguliwa. Japo anakumbwa na vizuizi vingi katika juhudi zake za kuwatetea na kuwahamasisha kuhusu haki zao, hafi moyo. Anadhihirisha kuwa yeye ndiye bora hasa anapobainisha baadhi ya shida zinazowakabili wafanyakazi zikiwemo mshahara duni na mazingira magumu ya kufanyia kazi. Kama kiongozi wa wafanya kazi, Lanina anaelewa shida zinazowakumba wafanyakazi ambao ni wananchi wa kawaida. Hii ni sifa anayostahili kuwa nayo kiongozi bora na mwenye kuheshimu haki za anaowaongoza. Lanina anaonekana kuwa mstari wa mbele katika harakati ya kuwatetea wafanya kazi kama inavyojitokeza katika mazungumzo yafuatayo:

Lanina: (Anamkatiza mwenziwe)
Kwanza kabisa, malalamiko mmeshaletewa
kwa hivyo sioni kwa nini tuyakariri tena hapa.
Pili, sisi sio wawakilishi wa wafanya – kazi wa
shamba hili mjadala wowote juu ya malalamiko
yetu ni lazima ufanywe na watu tuliowawakilisha.
(Delamon anawatazama Zari na Shindo kwa kufadhaika)

Zari: (Kwa hasira kidogo)
Lakini ndio viongozi wao
Nyinyi ndio mnaochochea migomo hapa.
(Anazidisha hasira)
Nyinyi ndio washenzi mnao... mnao... (Mazrui, 1981: 12)

Kutokana na juhudi zake za kuwatetea wafanyakazi wenzake, wasaidizi na hata Delamon wanafadhaishwa na ushujaa wa Lanina. Maelezo ya Lanina yanabainisha kuwa ana busara na uelewa wa shida zinazowakumba. Amewazidi maarifa wasaidizi wa Bwana Delamon ambao wanatumia nguvu katika uongozi wao.

Aidha Wanacheneo katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* (2009) wangeweza kuepuka au kupunguza dhuluma dhidi yao kama vile ukosefu wa dawa, mishahara duni, ufisadi na ukosefu wa chakula kama wangeweka mikakati ya kuwachagua viongozi wema. Ni bayana kuwa hawajaweka mikakati mwafaka ya kuhakikisha kuwa viongozi wanawajibika kwa sababu hata baada ya kumchagua Meya mara tatu, wanakumbwa na shida zinazoweza kutatuliwa kupitia uongozi mwema. Meya anapoelezwa shida zinazowakumba wananchi wa kawaida anaowaongoza haonyeshi huruma badala yake anabainisha kuwa hata asipowasaidia wananchi waliomchagua, bado watamchagua tena. Ndiposa

anamwambia Siki, “Huna habari kuwa walinichagua hao hao watu? Mara ngapi hii kunichagua? Tatu. Hata nikitaka nne, tano na sita bado watanipa.”

Inabainika wazi kuwa, Wanacheneo wanateseka kwa sababu ya kumchagua kiongozi asiyeyajali maslahi yao. Huenda maisha yao yangekuwa afadhali ikiwa wangemchagua kiongozi tofauti kama vile Bwana Kheri katika awamu ya pili baada ya kugundua kuwa Meya aliwasaliti katika awamu ya kwanza. Diwani Kheri anadhihirisha sifa anazostahili kuwa nazo kiongozi yeyote anayeyajali maslahi ya wananchi wa kawaida. Kwa mfano, anawaonya Meya na madiwani wenzake dhidi ya mpango wa kuwapiga wananchi wa kawaida kwa sababu ya kugoma ili kutoa malalamishi yao. Isitoshe, anawaonya dhidi ya kujiongezea mishahara na kutotozwa kodi kwa sababu uchumi utadidimizwa zaidi. Mwisho, Bwana Kheri anaorodhesha baadhi ya mambo muhimu yanayohitaji kushughulikiwa na uongozi wa Meya ili kuinua viwango vya maisha ya Wanacheneo. Hulka ya Diwani wa Tatu ni ithibati tosha kuwa ndiye aliyestahili kuchaguliwa na wananchi wa kawaida lakini wanafanya kinyume na kumchagua kiongozi asiyewajali hivyo kuchangia dhuluma dhidi yao kwa kumchagua kiongozi mbaya.

Ame na Zidi katika *Amezidi* (1995) wanadhihirika kuwa viongozi wabaya kutokana na ubadhirifu wa mali ya umma. Ni viongozi waliochaguliwa na wananchi wa kawaida lakini wanatumia mamlaka yao kujinufaisha na kujifurahisha huku wananchi wa kawaida wakikumbwa na shida nyingi. Ubadhirifu wao unajitokeza katika maandalizi yao ya siku ya kuzaliwa.

Tunaambiwa kuwa mwaka uliotangulia maandalizi yalikuwa makubwa sana na ilidhaniwa kwamba hakuna sherehe ambayo ingeishinda. Lakini mwaka uliofuata, walipanga kutumia mara mbili zaidi ya kiasi cha fedha cha mwaka uliotangulia. Kutokana na wageni wanaowaalika kama vile ndugu zao wa Kiafrika na wanaowapa misaada hasa kutoka Marekani na Uropa, Ame na Zidi ni viongozi wa kisiasa hivyo basi wamechaguliwa na wananchi ambao wengi wao ni wa kawaida. Kinyume ni kuwa, wanatumia pesa nyingi yaani shilingi milioni arobaini katika siku ya kuzaliwa tu ilhali wananchi wa kawaida wanakumbwa na shida kama ukosefu wa chakula na elimu duni miongoni mwa shida nyingine. Uongozi wao mbaya unabainika kwa kutotoa suluhu kwa matatizo yanayowakumba wananchi na kuyapa uzito masuala kama siku ya kuzaliwa ambayo hayana umuhimu wowote. Bila shaka ubadhirifu huu unaosababisha dhuluma dhidi ya wananchi wa kawaida unachangiwa na kuendelezwa na wananchi wenyewe kwa kuwachagua viongozi wasiofaa na hali itabadilika na kuwa nzuri iwapo wananchi wataweka mbinu za kuhakikisha kuwa viongozi waadilifu na wenye kuwajibika watachaguliwa. Mbinu mojawapo ya kuhakikisha kuwa kiongozi ni mwadilifu ni kuweka kifungu katika sheria ambacho kitamhitaji kutaja mali zake na jinsi alivyopata mali hiyo kabla ya kuchaguliwa. Ikiwa itabainika wazi kuwa mali yake ameipata kupitia kwa njia zisizo halali, akose fursa ya kuchaguliwa kuwa kiongozi. Vilevile, akiwa uongozini aweze pia kutaja mali yake baada ya kipindi fulani. Kifungu hiki cha sheria kitawazuia viongozi kujilimbikizia mali na kuwaongoza wananchi katika misingi ya haki na kuwaletea mendeleo.

4.3 KUWEKA JUHUDI

Ili kukabiliana na dhuluma dhidi yao, wanannchi wa kawaida wanahitaji kutia bidii wajiinue hasa kiuchumi. Watakapojiimarisha kiuchumi watajiepusha kuwa wategemezi jambo linalowafanya wachangie dhuluma dhidi yao kwa urahisi. Kwa mfano, baadhi ya wahusika katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki* wanafanya kazi ya aina moja tu. Mshahara wa kazi hii ni duni na kazi yenyewe ni ngumu na hufanywa kwa muda mrefu. Licha ya kasoro hizi, baadhi ya wafanya kazi ambao wanawakilisha wananchi wa kawaida hawaweki juhudi zozote za kupinga dhuluma dhidi yao kutoka kwa waajiri wao. Kwa mfano, Pelekha, Matovu na Tereki wameshindwa kuweka juhudi kutetea haki zao. Wamekata tamaa na kuamua kujiunga na mdhulumu wao ambaye ni Bwana Delamon. Ukosefu wa kuweka juhudi unabainika Tereki anapomwambia Lanina kuwa:

> ... kubwa tunalotaka sasa ni kubadilisha siasa zetu tu za kupigania haki zetu. Nguvu na mizozo haifai. Sasa ni wakati wa busara. Hebu itazame hali yetu sisi Waafrika ... tangu zamani.Tangu tulipokuwa wawili ... watatu ... wachache tu. Idhilali tulivumilia na zaidi. Tukajitosa kwenda kutafuta funguo za hili fumbo, fumbo la hali yetu. Basi kwa nini mpaka sasa jinamizi kutufuata kwa sauti ya mifupa inayosagika na bubujiko la damu inayomwagika? (Mazrui, 1981:53)

Tereki, Pelekha na Matovu wameshindwa kuvumilia shida zinazowakumba na badala ya kutia bidii na kuungana na Lanina kukabiliana na wanaowasababishia shida hizo, wanakata tamaa na kuungana na mdhulumu wao. Ndiposa Delamon anawafanyiza kazi katika mazingira magumu, kwa muda mrefu na kwa mshahara duni kwa sababu anajua kuwa wafanyakazi wametengana na juhudi za kupigania haki zao zimepungua.

Kwa upande mwingine, tamthilia ya *Mstahiki Meya* imebainisha jinsi wananchi wa kawaida wangejiepusha na dhuluma iwapo wangeweka bidii katika sehemu mbalimbali kama ifuatavyo: Mwanzo, hawaweki bidii katika kutafuta kazi mbadala baada ya kugundua kuwa ajira katika baraza la mji haina manufaa kwao. Hii ni kwa sababu mshahara wenyewe ni mdogo, huwa nusu na hauji kwa wakati na zaidi ya yote, hautoshelezi kiwango cha juu cha maisha. Kwa mfano, Dadavuo Kaole ana utapiamlo kwa sababu mamake hawezi kumudu chakula bora ndiposa wanakula chakula kilichokusudiwa kuliwa na mbwa. Isitoshe, chakula chenyewe huwa kiporo kwa sababu ya ukosefu wa pesa ya kununua makaa ya kukitokosa. Mwishowe, Dadavuo anaaga dunia kutokana na kula chakula hiki. Hali hii ngumu inamkumba mamake Dadavuo licha ya kuwa anafanya kazi na baraza la mji. Hata baada ya kugundua upungufu wa kazi anayoifanya, hatii juhudi za kutafuta kazi nyingine ya kumfaa ila kulalamika tu na kuonekana asiyejua la kufanya:

Waridi: Chakula gani hicho hasa ulichochukua ukimpa mtoto?

Mama: Wali na maharage yalolala.

Siki: Wewe hukuyala?

Mama: Sikuyala mie. Yalikuwa machache tu!

Waridi: Wala hukukitokosa chakula hicho tena nyumbani?

Mama: (Akimtazama.) Moto utatoka wapi mwanangu? Makaa siku hizi yamepanda bei tangu sheria ya misitu ishike kasi. Nayo bei ya mafuta taa ndiyo hiyo inapanda kila uchao.

Waridi: Lakini si sasa waona matokeo yake?

Mama: (Kwa upole.) Si nyinyi ndio mjuao wanangu! Mimi sifahamu ila nilikiona afadhali. Siku nyigi tunakula kile walichopimiwa mbwa wa bwana tusipate dhara hata moja. Nashangaa leo hiki chaleta taabu... (Arege, 2009: 4- 5)

Mamake Dadavuo Kaole analalamikia hali ngumu ya maisha na haweki bidii zozote kujinusuru mathalan kwa kujiunga au kuanzisha kikundi cha ushirika kinachojumuisha kazi ya amali. Aidha wananchi wa kawaida wanatumia mbinu hafifu kupinga dhuluma dhidi yao. Wanagoma na kuandamana hadi ofisi ya Meya ilhali kuna askari waliojihami kwa bunduki. Kwa sababu hii, askari wanawatawanya kwa urahisi hivyo kudidimiza juhudi zao za kuyafikisha malalamishi yao kwa Meya. Bila shaka hawakuweka juhudi katika kufikiria kuhusu mbinu ambayo ingefanikisha azma yao. Japo uongozi wa Meya hungewapa nafasi ya kuandamana hata kama ni kwa amani, wangejuza vyombo vya usalama ili wawekewe usalama wasidhulumiwe zaidi inavyobainika wanapofurushwa na askari. Wanakejeliwa na Meya pamoja na wafuasi wake ishara kuwa hawatiliwi maanani inavyobainika katika mazungumzo yafuatayo:

Diwani II: Iwe ni dhiki au raha

Diwani I: Ila dhiki hamna hapa. Mstahiki Meya ndiye awezaye kuchemua na wote wakabanwa na mafua. *(Kwa Meya)* Hawawezi kuchemua wewe upate mafua. Hata kidogo!

Meya: Hawakujua hayo. Waliona mchezo.

Bili: Walivyofyatuka watu, sijawahi kuona!

Diwani II: Kila mtu na mguu wake kumponya. *(Wote anacheka.)* (Arege, 2009: 59)

Dhihaka inayojitokeza kuwahusu wafanyakazi katika mazungumzo ya hapo juu inabainisha matumizi ya mbinu duni katika harakati ya kujikomboa. Ndiposa Diwani wa Kwanza haoni dhiki yoyote katika mgomo wa wafanyakazi kwa sababu wanakabiliana na askari waliojihami kwa bunduki na virungu. Uzembe na ukosefu wa maarifa unabainika katika mbinu yao ambayo inasababisha vurugu na dhuluma zaidi wanapofurushwa na askari. Aidha, watetezi wa wafanya kazi wanatafuta njia ya mkato kusuluhisha shida zinazowakumba. Kwa mfano, Tatu anamwomba Siki awasaidie kupanga miadi na Meya kwa kuwa yeye ni binamu yake. Siki anapomwambia kuwa itakuwa vigumu kwa sababu yeye ni mwajiriwa kama Tatu, anaonekana kukata tamaa. Siki anapomhimiza wasikate tamaa, Tatu anamjibu, "Tunaweza kujaribu tena ingawa hatuoni matumaini." Bila shaka Tatu haoni uwezekano wa kukutana na Meya na kumweleza shida zao. Siki anapomwambia wasikate tamaa, anajaribu kumhimiza waweke juhudi katika mipango ya kukutana na Meya lakini Tatu tayari amevunjika moyo. Ni kama hatua yake na tumaini lake la mwisho lilikuwa kwa Siki. Kama kiongozi wa wafanyakazi, Tatu anatarajiwa kutoa uongozi dhabiti na uliojaa uvumbuzi wa mbinu mbali za kupigania haki zao bila kuchoka na kukata tamaa. Kukata tamaa ni ishara ya uvivu ambao wananchi wa kawaida wanahitaji kuuepuka ili kufanikiwa katika azma yao ya kujikomboa.

Ame na Zidi wakiigiza nafasi ya mwananchi wa kawaida wanabainisha jinsi wanavyochangia dhuluma dhidi yao kwa sababu ya kutoweka juhudi ili

kuimarisha maisha yao. Mathalan, wanatumia muda wao mwingi kulala badala ya kufanya kazi. Hali ya kutopenda kazi inabainika Ame anaposema,

> Ni kwa nini mtu apende kazi? Mungu yupo na ardhi ipo ... na ardhi yenyewe bikra ... Wewe kula tu na kulala! Ah, hata Mungu alifanya kazi siku saba, kisha akapumzika ...(Mohamed, 1995: 7.)

Matokeo ya kutoweka juhudi ni umaskini, njaa na matumizi ya njia za mkato kujinusuru jambo linalozidisha dhuluma. Kwa mfano, Zidi na Ame wanapovamiwa na njaa kutokana na uzembe wao, wanatuma maombi ya msaada kutoka nchi zilizoendelea. Misaada hii inaendeleza uvivu kwa sababu Zidi na Ame kama wananchi wa kawaida hawaoni haja ya kuweka juhudi katika kuzalisha chakula kwa sababu misaada ipo. Isitoshe, baadhi ya misaada kama vile nyama inawasababishia maradhi ya tumbo na mwishowe wanaaga. Aidha, Zidi kama mwalimu hana ufahamu wa kutosha kuhusu anachokifunza. Ndiposa anapoulizwa maswali na wanafunzi anashindwa kuyajibu. Anawahimiza wanafunzi kukariri tu mawazo na hajui umuhimu wa mawazo hayo katika maisha ya baadaye ya mwanafunzi na taifa. Hali hii inatokana na uvivu alionao mwalimu katika kufanya utafiti wa kuelewa na kuona jinsi maarifa anayowapa wanafunzi yanavyoweza kuwa ya manufaa hasa katika uundaji. Kwa sababu elimu ni ya kinadharia tu na maarifa yake hayawezi kutumiwa katika uundaji, wahandisi uagizwa kutoka nje licha ya kuwa kuna wanafunzi waliohitimu. Ni bayana kuwa, ikiwa Ame na Zidi kama wananchi wa kawaida wangeweka juhudi katika kilimo na elimu, bila shaka wangeepuka njaa iliyowasababishia kifo na uchumi wao ungeendelea kutokana na kiwango cha juu cha kiteknolojia hivyo kuyaboresha maisha yao.

4.4. KUWA JASIRI

Japo kuna wahusika wanaowawakilisha wananchi wa kawaida ambao ni jasiri, idadi yao ni ndogo hivyo kushindwa kufanikiwa katika azma yao ya kuleta ukombozi. Wengi wa wananchi wa kawaida katika tamthilia za *Kilio cha Haki*, *Mstahiki Meya* na *Amezidi* ni waoga. Uoga huu huwapa wadhulumu wao fursa ya kutumia mbinu kama vile vitisho, vyombo vya dola na sheria mbaya kuwakandamiza wananchi wa kawaida. Katika tamthilia ya *Kilio Cha haki* (1981) kwa mfano, Lanina, Dewe na Musa ni jasiri lakini ujasiri wao unasalitiwa na wenzao kama Tereki, Pelekha, Matovu, mamake na babake Lanina miongoni mwa wafanyakazi wengine. Ujasiri wao unaambulia patupu kwa sababu Lanina anafungwa naye Musa na Dewe wanakimbilia usalama katika nchi jirani. Kwa hivyo, ili kujiepusha na dhuluma, wafanyakazi wanahitaji kuelezwa umuhimu wa kuwa na ujasiri katika kupigania haki zao. Delamon anapowatuma askari kuwatawanya wafanyakazi wanapogoma katika harakati ya kutetea haki zao wanatoroka. Mgomo na maandamano ni hali inayohitaji ujasiri mkubwa na kujitolea mhanga jambo ambalo halionekani wanapotoroka kwa njia ambayo inamfanya Meya kuwadhihaki. Kutoroka kwao kwa sababu ya uoga kunawapa askari fursa nzuri ya kumkamata Lanina ambaye yupo kwenye mstari wa mbele kuwatetea. Japo walikabiliwa na hatari ya kupigwa risasi, tunataraji kuwaona wengi wakikamatwa bali si Lanina tu. Isitoshe, Tereki ambaye alishikwa pamoja na Lanina anashawishika na kukubali kujiunga na mdhulumu wa wafanyakazi wenzake kwa sababu ya uoga. Hapa ni baada ya Kachero kumwambia kuwa,

> Lakini hutaweza kuzungumza na rafiki zako, maana itabidi tukuweke kizuizini mpaka tuijue jawabu yako. Uhuru wako unategemea jawabu yako. (Mazrui, 1981: 18.)

Badala ya kuwa jasiri na kukataa kata kata kama mwenzake Lanina, anachagua "uhuru" ambao hakuupata kwa sababu japo alikubali kuwa kiongozi, alifanya alivyoamriwa na Bwana Delamon. Tereki alihitaji kuwa jasiri na kukataa mipango ya kushiriki katika kuwadhulumu wenzake ili Delamon akubaliane na matakwa yao kupitia kwa misimamo yao dhabiti na ashindwe kutumia mbinu ya "tenga utawale."

Kwa upande mwingine, Mwengo kama mwananchi wa kawaida anahitaji kuwa jasiri na kutupilia mbali mila potovu. Mila hizi zinamnyima uhuru wa kuwatunza watoto Lanina anapokuwa kizuizini kwa sababu kulingana na mila, kazi ya kuwatunza watoto ni ya mwanamke. Kwa kuegemea kwenye mila, mwanamke kushirikiana na wanaume katika kupigania haki ni upotovu wa maadili kwa sababu huyo mwanamke anataka kuwa mume. Ukosefu huu wa ujasiri wa kuiacha mila inayomfanya Mwengo mtumwa inamnyima nafasi ya kumuunga mke wake katika kupigania haki hivyo kuchangia dhuluma dhidi yao. Aidha, babake na mamake Lanina wanahitaji kuwa jasiri na kuibwaga hii mila ili kumpa Lanina motisha ya kupigania haki zao pammoja na za wafanyakazi. Wanaogopa kuchekwa kuwa binti yao amevunja mila ambazo zinamhitaji awe nyumbani kuitunza familia badala ya kufanya kazi za wanaume. Mzee Seromanga ambaye ni babake Lanina anamtusi na kumchapa Lanina kwa sababu ya kukosa ujasiri wa kukabiliana na kejeli kutoka kwa wanakijiji kuwa mtoto wake ameuasi utamaduni. Japo utamaduni hujenga

kanuni na taratibu za kuishi, si kila jambo linalotokana na utamaduni ni nzuri hasa baada ya mapito ya wakati. Kwa hivyo, ni muhimu watu kama Mzee Seromanga na baadhi ya wanakijiji wafunzwe mambo mazuri katika utamaduni na yale mabaya ili wajue namna ya kuyaepuka mabaya na kuyaendeleza mazuri. Ili kumpa motisha Lanina ambaye yuko mstari wa mbele kupigania haki, Mzee Seromanga anastahili kuwa mkakamavu na kupuuzilia mbali kejeli kutoka kwa watu kuwa mtoto wake amevunja utamaduni.

Ujasiri vilevile unahitajika miongoni mwa wahusika wanaowawakilisha wananchi wa kawaida katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* ili kujiepusha na dhuluma. Kwa mfano, Dida anahitaji ujasiri wa kumwambia Meya kuwa ni mlafi na mbinafsi ndio maana anajichoma kwa chai na kumsingizia Dida. Badala ya Dida kuwa mkakamavu na kumwambia ukweli, anaogopa na kunyenyekea ilhali hana kosa lolote. Unyeyekevu wake unampatia Meya kiburi ambaye anamdunisha kwa kumtusi. Pia, Waridi anahitaji ujasiri ili kutafuta ukweli kuhusu zilipo dawa ambazo baada ya siku tatu, hazikuwa zimefika zahanatini. Lakini baada ya kugundua kuwa alidanganywa na mazingira ya kufanyia kazi yanaendelea kuwa magumu, anaiacha kazi yake ya utabibu. Hali hii inatokana na uoga wa kumkabili Meya na kuhakikisha kuwa dawa zimewasili na mazingira ya kufanyia kazi yameboreshwa. Hivyo basi, Waridi alihitaji kuwa jasiri ili kuhakikisha kuwa dawa zimeletwa na mazingira ya kufanyia kazi yameboreshwa.

Mhubiri kama mwananchi wa kawaida anahitaji ujasiri ili kumwambia Meya kasoro alizonazo katika uongozi wake kwa sababu kanisa ina jukumu la kueleza ukweli jinsi ulivyo. Mhubiri ana ushawishi mkubwa na uwezo wa kutangaza uozo wa uongozi wa Meya hadharani ikiwa hatazingatia ushauri wake. Ni kutokana na kigezo hiki ambapo tunatarajia Meya aongoze kwa maadili kwa kuwa hangependa mbinu zake za uongozi mbaya zijulikane na umma. Lakini kutokana na ubinafsi na uoga, anampa Meya sifa nzuri na kuupongeza uongozi wake. Hiki ni kinaya kwa sababu Wanacheneo wanakosa huduma muhimu kama vile chakula bora na maji safi chini ya uongozi wa Mstahiki Meya. Aidha, Wanacheneo wanahitaji ujasiri wa kuwania uongozi ili kuutumia kuboresha maisha yao. Lakini wanaogopa kuingia katika siasa kwa sababu siasa ni mchezo mchafu na hawangependa kuhusishwa na uchafu wa siasa. Kwa sababu hii, wanawachagua viongozi wale wale ambao hawayabadilishi maisha yao. Kwa mfano, wamemchagua Mstahiki Meya mara tatu licha ya kuwa amewadhulumu katika awamu hizo zote. Kwa hivyo, wanataaluma kama vile Siki ambao wanaelewa shida za wananchi wa kawaida wanachangia katika shida zinazowakumba wenzao kwa kutowania nyadhifa za uongozi na kwa kutoungana na wananchi wenzake ili kuweka sheria za uchaguzi za kuhakikisha kuwa viongozi wanawajibika na hatua zitakazochukuliwa ikiwa wataenda kinyume.

Katika tamthilia ya *Amezidi*, ujasiri kama njia mojawapo ya kukabiliana na dhuluma unahitajika katika mkutano wa Bosi, Msaidizi wake na wafanyakazi.

Katika mkutano huu, Bosi baada ya kupanga njama ya kuiba mali ya umma, anasingizia wafanyakazi. Anawaambia kuwa atakayepatikana atafutwa kazi na kupelekwa mahakamani. Mmoja wa wafanyakazi anajaporibu kudadisi suala hilo, anamnyamazisha na badala ya wafanyakazi wenzake kumuunga mkono na kumpa motisha ya kuuliza swali jinsi wanavyohusika katika wizi huo, wanaogopa na kutawanyika walivyoamriwa. Japo wanahitajika kutii amri kutoka kwa wakubwa wao, si kila amri inafaa kufuatwa hasa inayolenga kukandamiza haki zao. Ni muhimu wawe na umoja ili kushinikiza wapewe fursa ya kutoa maoni kuhusu masuala yanayowalenga. Kujumuisha kwao katika mchakato wa kutoa uamuzi utawapa ujasiri wa kudadisi tuhuma za wizi wanazosingiziwa. Wanapokosa umoja ambao utawapa ujasiri, inawawia vigumu kumwambia Bosi ukweli kuwa hawahusiki kwa vyovyote katika unyakuzi wa mali ya umma ili wazime mbinu zake za wizi. Upungufu huu unawafanya wafanyakazi ambao ni wawakilishi wa wananchi wa kawaida kuchangia dhuluma dhidi yao. Vilevile, wanafunzi wanahitaji kuwa jasiri ili kumkosoa mwalimu ambaye haelewi taaluma yake. Ujasiri huu utapatikana ikiwa wanafunzi watapewa nafasi katika kuchangia masuala yanayowahusu katika harakati ya kujipatia elimu. Kwa sababu hawana fursa hii, wanakosa ujasiri wa kumwambia mwalimu ukweli kuwa yeye ni mjinga na anawapotosha katika majibu yake kwa maswali wanayomuuliza hivyo basi kuchangia dhuluma dhidi yao kielimu. Lakini wanaogopa kumwambia ukweli kuwa yeye ni mjinga na anawapotosha katika majibu yake kwa maswali wanayomuuliza. Vilevile, kuhusishwa katika masuala ya elimu kutawapa

ujasiri katika kukosoa mfumo wa elimu ambao ni wa kinadharia usiowawezesha kuunda.

4.5 KUFAHAMU HAKI

Haki ni wazo dhahania ambalo mtu anastahili au anatakiwa kulifurahia, iwe kwa njia ya desturi, sheria au utamaduni. Inamaanisha kuwa kila mtu ana fursa sawa ya kufurahia haki kulingana na tabia za kimaumbile, maadili na sheria (Eguren, 2012). Ili kujikomboa kutoka kwa dhuluma, wananchi wa kawaida wanahitaji kufunzwa kuhusu haki zao zinazokiukwa kama vile haki ya kuishi, uhuru na usawa mbele ya sheria. Mafunzo yanapaswa kutolewa na baadhi ya wananchi wa kawaida ambao wanazifahamu haki zinazokiukwa. Wananchi wengi wa kawaida wakishahamasishwa kuhusu haki zao, watapata mwamko wa kupanga na kutetea maslahi yao ipasavyo. Kwa mfano, katika tamthilia ya *Kilio Cha Haki* wanahitaji kujua kuwa wananchi kama wafanyakazi, wanafaa kulipwa mshahara mzuri na kufanya kazi kwa muda unaostahili. Haki hii haijulikani na wengi kama vile Mfanya Kazi ambaye haoni haja ya kugoma kwa sababu amepata nyongeza ya mshahara. Lakini hana ufahamu kuwa, japo amepewa nyongeza, muda wa kufanya kazi nao umeongezwa. Kuongezwa huku kwa muda wa kufanya kazi kunawanyima fursa ya malipo ya ziada waliyokuwa wakiyapata baada ya kufanya kazi zaidi ya muda uliowekwa. Kwa hivyo Mfanya Kazi angefahamu haki zake barabara na jinsi zilivyokiukwa, angejiunga na wenzake kuzipigania. Isitoshe, Tereki, Pelekha na Matovu wanahitaji kufahamu kuwa kupigania maslahi mema ni haki yao. Lakini kwa

sababu hawana ufahamu huu, wanaingia kwa mtego wa Bwana Delamon wa kuwafanya viongozi wa chama ambacho amekianzisha. Njama ya Delamon ilikuwa kuiua ari ya wafanyakazi ya kupigania haki zao lakini Tereki, Pelekha na Matovu walidhani wanafanyiwa hisani. Kile ambacho hawakufahamu ni kuwa walikuwa na haki ya nyongeza ya mshahara na uhuru wa kukiongoza chama cha wafanyakazi kidemokrasia. Kukosa kufahamu haki zao kunawafanya wachangie dhuluma dhidi yao na wenzao kwa kutopata mshahara mzuri na kufanya kiwango cha kazi kinachostahili. Mtu wa Nne naye anadhihirisha kuwa anahitaji kufahamu haki zake kama mwananchi wa kawaida ili ajiepushe na dhuluma. Anamkashifu Lanina anapowaambia kuwa wanahitaji kuungana ili kupinga dhuluma dhidi yao. Anamwambia,

> "Sasa ! Wewe mwanamke umesimama na umeanza kutuchochea wewe! Sasa tukifukuzwa kazini je! Wewe una shamba? Wewe... wewe utatupatia kazi tukifukuzwa? Upuuzi tu! Porojo tu! Kwanza hata nyinyi wanawake mnatunyonya sisi wanaume!... (Mazrui, 1981: 63)

Mtu wa Nne haoni haja ya kukomesha kunyonywa kwa sababu hiyo itamaanisha kufukuzwa kazini. Kwa hivyo, hafahamu kuwa ana haki ya kulipwa vizuri. Lanina angemhamasisha kwanza kuwa haki yake ya kulipwa vizuri imekiukwa, angejiunga na wenzake kupinga unyonyaji. Hangejali kufukuzwa kazini kwa sababu umuhimu wa maisha bora hapo baadaye ungempa ari ya kupigania haki zake liwe liwalo. Ni hakika kuwa ufahamu wa haki zako ndio mwanzo wa kujiepusha na dhuluma.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* (2009), Dida ambaye anawakilisha mwananchi wa kawaida alihitaji kufahamu haki zake ili kujiepusha dhidi ya

matusi na dharau kutoka kwa mstahiki Meya. Dida ana haki ya kuheshimiwa na si vyema Meya kumdunisha kwa matusi na dharau. Lakini Dida hafahamu hili na anapodunishwa, anaomba msamaha kwa makosa ambayo hakuyafanya. Ni kama Dida hajui kuwa ana umuhimu katika kumsaidia Meya kutekeleza majukumu yake na kwa sababu hiyo anastahili heshima. Kwa hivyo, angekuwa na ufahamu wa haki zake, angepinga dhuluma dhidi yake kutoka kwa Meya na kumbainishia umuhimu wake katika maisha ya Meya na ya baraza la mji wa Cheneo kwa jumla. Vilevile, Waridi kama mfanyakazi na mwananchi wa kawaida anahitaji kufahamu kuwa ana haki ya kujua ukweli kuhusu ukosefu wa dawa zahanatini. Kwa mfano, baada ya Waridi kugundua kwamba alidanganywa kuwa dawa zingefika baada ya siku tatu, angekashifu kitendo hicho na kumshinikisha Meya kuwajibikia vifo vya wananchi kutokana na ukosefu wa dawa. Lakini ni kama Waridi hakuwa na ufahamu kuwa kuambiwa ukweli kuhusu hali halisi ilikuwa ni haki yake ndiposa anajiuzulu baada ya kushindwa kuwahudumia wagonjwa kutokana na ukosefu wa dawa na mazingira mabaya ya kufanyia kazi.

Ukosefu wa ufahamu wa haki miongoni mwa wananchi wa kawaida vilevile unabainika katika tamthilia ya *Amezidi* (1995). Ame ambaye anaigiza nafasi ya mwanafunzi hafahamu kuwa elimu bora ni haki yake. Anawakilisha wanafunzi ambao hawana uwezo wa kujitetea dhidi ya mifumo ya elimu ambayo haiwanufaishi baada ya kuhitimu. Hali hii hutokana na ukosefu wa ufahamu kuhusu umuhimu wa elimu bora wakiwa shuleni kwa sababu ya kuelekezwa

vibaya na walimu na wazazi au kwa kukosa kuelekezwa kabisa. Isitoshe, mwalimu wake ambaye ni Zidi hana ujuzi wa taaluma yake ya ualimu na ni mzembe. Kwa hivyo, haki yake ya kupata elimu bora inakiukwa kupitia mfumo mbaya wa elimu pamoja na mwalimu ambaye hana uelewa wa anachokifunza. Kwa hivyo, Ame na wanafunzi wengine walihitaji kufahamu kuwa elimu bora ni haki yao na baada ya kugundua kuwa ilikuwa na kasoro waikatae. Lakini hata baada ya kugundua kasoro zake hawakuikataa kwa sababu hawakuona elimu kama haki yao muhimu. Kutokana na kutoifahamu haki hii, baada ya kuhitimu wanashindwa kuunda mashine ya kuchemsha maji ya moto, friji na simu licha ya kuwa wamehitimu kama wahandisi kutoka chuo kikuu.

4.6 HITIMISHO

Sura hii imebainisha lengo la mikakati anayoweza kuiweka mwananchi wa kawaida ili kuzuia au kupunguza dhuluma dhidi yake. Mikakati iliyobainishwa ni uchaguzi wa viongozi bora, kuweka juhudi, kuwa jasiri na kufahamu haki zao. Umuhimu wa kuwachagua viongozi bora umeonyeshwa kupitia kwa matendo mabaya ya viongozi dhidi ya wananchi wa kawaida waliowachagua. Matendo hayo ni kama ufisadi ambao unaharibu uchumi wa nchi na kuwanyima wananchi wengi mahitaji ya kimsingi kama vile chakula. Kwa hivyo, mikakati ya kuwachagua viongozi walio bora ikiwekwa, wananchi wa kawaida watayaboresha maisha yao kwa kuwachagua viongozi wanaowajali. Kwa upande mwingine, kuweka juhudi kumesawiriwa kwa kuangazia dhuluma

wanazokumbana nazo wananchi wa kawaida kwa kulaza damu. Kwa mfano, kulala kwa siku nyingi na kupokea misaada iliyoharibika wakati wa njaa. Ujasiri nao kama njia muhimu ya kujikomboa ulibainishwa kwa kuangazia uoga wa wananchi wa kawaida. Uoga huu uliwafanya wananchi wa kawaida kushindwa kupinga dhuluma dhidi yao kwa sababu pingamizi yoyote ingesababisha kufutwa kazi au kufungwa gerezani. Mwisho, wananchi wa kawaida wanafaa kufahamu haki zao ili wazipiganie ipasavyo. Ufahamu wa haki kama mbinu ya kujiepusha na dhuluma umebainishwa kupitia jinsi baadhi ya wananchi wa kawaida wanavyoziona shida wanazokumbuna nazo kuwa jambo la kawaida. Kwa mfano, baadhi ya wananchi wa kawaida hawaoni haja ya kupigania nyongeza ya mshahara kwani kulingana nao tayari wamefanyiwa hisani kupewa kazi na hawangependa kufutwa. Sura inayofuata itashughulikia muhtasari, matokeo ya utafiti kulingana na malengo, mchango wa utafiti na mapendekezo ya tafiti za baadaye.

SURA YA TANO

5.0 HITIMISHO

5.1 UTANGULIZI

Katika sura ya nne, tumeeleza mikakati mbalimbali anayoweza kuitumia mwananchi wa kawaida ili kujiepusha na dhuluma dhidi yake. Mikakati iliyopendekezwa ni pamoja na: kuwachagua viongozi bora, kuweka juhudi katika azma yao ya kujikomboa, kuwa jasiri na kufahamu haki zao. Uchaguzi wa viongozi ulibainishwa kwa kuangazia ukosefu wa mahitaji ya kimsigi miongoni mwa wananchi hali ambayo ingesuluhishwa na viongozi waliochaguliwa. Lakini kwa sababu viongozi hawa hawakuwa na sera madhubuti na wamejazwa na ubinafsi, hawayazingatii maslahi ya wananchi waliowachagua. Kwa upande mwingine, kuweka juhudi kumeangaziwa kwa kurejelea uzembe na udhaifu miongoni mwa wananchi wa kawaida katika harakati ya kupigania haki zao na kujiinua kiuchumi. Hivyo basi matakwa yao hayatiliwi maanani na wanaowadhulumu kwa sababu ya kubainika wazi kuwa hawajaweka juhudi zozote. Ujasiri nao uliangaziwa kupitia kwa uoga walioudhihirisha wananchi wa kawaida katika kupigania haki zao. Uoga ulikuwa kikwazo kikubwa na baada ya wadhulumu kugundua hivyo, wakatumia mbinu ya ‘tenga utawale’ kuendeleza udhalimu wao. Mwisho, mbinu ya kufahamu haki zinazokiukwa ni muhimu katika kuwapa motisha kuyaboresha maslahi yao. Hii ni baada ya kubainika kuwa baadhi ya wananchi wa kawaida wanachangia dhuluma dhidi yao kwa sababu ya kutofahamu haki

zao. Katika sura hii, tutahitimisha tasnifu na kutoa mapendekezo kwa utafiti zaidi

5.2 MUHTASARI WA UTAFITI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza jinsi mwananchi wa kawaida anavyochangia dhuluma dhidi yake alivyosawiriwa katika tamthilia za *Kilio cha Haki* (1981), *Amezidi* (1995) na *Mstahiki Meya* (2009). Tamthilia hizi ziliteuliwa kwa ktumia mbinu kusudio ambayo ilifanikisha kuafiki malengo ya utafiti. Kwa kutumia wahusika mbalimbali, utafiti ulipania kuonyesha jinsi mwananchi wa kawaida hasa katika nchi zinazoendelea, anavyochangia dhuluma dhidi yake kupitia kwa matendo na maamuzi yake katika kipindi cha ukoloni na baada ya ukoloni. Aidha, utafiti ulilenga kubainisha athari zinazotokana na dhuluma dhidi ya mwananchi wa kawaida na mbinu anazoweza kuzitumia ili kujiepusha na dhuluma mbalimbali.

Nadharia mbili zilizoteuliwa kuhimili kazi hii ni nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa na nadharia ya Udenguzi. Mihimili ya nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa ambayo iliongoza kazi hii ni pamoja na mhimili wa wahusika wa kimaendeleo ambao hunuia kuipindua na kubadilisha hali yao ya maisha. Mhimili huu ulionekana kuwa muhimu katika kusaidia kuchunguza mbinu mbalimbali wanazoweza kuzitumia wananchi wa kawaida katika kujinua kiuchumi. Mhimili wa pili ulisawiri matukio kihistoria na kuonyesha jinsi wahusika hutekeleza matendo ya kitabaka. Mhimili huu ulisaidia katika kuonyesha mbinu zinazotumiwa na tabaka linalokandamiza katika kuendeleza

ukandamizaji na yale matendo ya tabaka linalokandamizwa ambayo yanaendeleza ukandamizaji. Nao mhimili wa tatu ulikuwa kuhusu wahusika ambao hutumiwa kama vipasa sauti vya watunzi ambao hupuliziwa uhai na huwa wanadamu wa kawaida. Mhimili huu ni muhimu katika kuonyesha jinsi mhusika kipasa sauti anavyowahamasisha wananchi wa kawaida kuhusu dhuluma wanazokumbana nazo na njia za kujikomboa kutokana na dhuluma hizo.

Kulingana na nadharia ya Udenguzi, mtazamo ambao umekubalika kuhusu ulimwengu na lugha ukichunguzwa kwa kuangazia matumizi ya ishara tunazozifahamu, taswira itakayojitokeza ni tofauti na yale tunayoyafahamu. Mihimili iliyoongoza utafiti huu ni ile ya kutokuwepo kwa toleo la mwisho la kazi ya fasihi na kazi ya fasihi kuwa na maana ya ndani ikifasiriwa kwa makini. Mhimili wa kutokuwepo kwa toleo la mwisho la kazi ya fasihi ulilenga kuonyesha kinaya katika madai ya baadhi ya waandishi kuwa mwananchi wa kawaida anadhulumiwa na walio na mamlaka pekee na kuwa hachangii dhuluma dhidi yake kwa kuwa yeye ni mnyonge. Lakini ukweli ni kuwa kwa kiwango fulani mwananchi wa kawaida huchangia dhuluma dhidi yake. Mhimili wa kazi ya fasihi kuwa na maana ya ndani ikifasiriwa kwa makini ni muhimu katika kubaini kiishara matendo wayatendayo wananchi ili kuchangia dhuluma dhidi yao.

Tasnifu hii imegawanywa katika sura tano: sura ya kwanza imeshughulikia usuli wa mada ya utafiti, suala la utafiti, maswali ya utafiti, sababu za

kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia pamoja na mbinu za utafiti.

Sura ya pili ilichunguza jinsi mwananchi wa kawaida alivyochangia dhuluma dhidi yake. Baadhi ya mambo anayoyashiriki na yanayomsababishia dhuluma ni kushikilia itikadi zilizopitwa na wakati, kutojiinua kiuchumi, kurusha cheche za matusi na kushiriki ufisadi. Ilibainishwa kuwa wananchi wa kawaida hawakuwa na ufahamu kuwa walikuwa wanachangia dhuluma dhidi yao kutokana na matendo yao.

Nayo sura ya tatu ilichunguza athari za dhuluma dhidi ya mwananchi wa kawaida. Athari zilizobainishwa ni kifo, umaskini na utengano wa kijamii. Athari hizi ziliwapa wananchi wa kawaida mwamko mpya wa kukabiliana na dhuluma.

Katika sura ya nne, utafiti ulichunguza mbinu anazoweza kutumia mwananchi wa kawaida ili kujiepusha na dhuluma dhidi yake. Mbinu zilizorejelewa ni kama vile uchaguzi wa viongozi bora, kuweka juhudi katika harakati ya kujikomboa, kuwa jasiri katika kukabiliana na wadhulumu na kufahamu haki zao ili wawe na ari ya kuzipigania.

Sura ya tano ni hitimisho la tasnifu. Hitimisho hilo limetoa utangulizi na muhtasari wa kila sura. Maelezo yametolewa kulingana na malengo ya utafiti. Mwisho sura hii imeeleza matokeo na mapendekezo ya tafiti ambazo zinaweza kufanywa katika siku za baadaye.

5.3 MATOKEO YA UTAFITI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza jinsi mwananchi wa kawaida alivyochangia dhuluma dhidi yake kwa kurejelea wahusika katika tamthilia za *Kilio Cha Haki* (1981), *Amezidi* (1995) na *Mstahiki Meya* (2009). Uchunguzi wa tamthilia zilizoteuliwa umeonyesha kuwa wananchi wa kawaida wamekuwa wakichangia dhuluma dhidi yao huku wakiwaona viongozi wao pekee kuwa chanzo cha shida zinazowakumba. Utafiti huu ulilenga kubadili mtazamo kuwa wananchi wa kawaida wanadhulumiwa na viongozi tu na kuonyesha jinsi wananchi wenyewe wanavyochangia dhuluma zinazowakumba. Wanachangia dhuluma dhidi yao kwa kuwachagua viongozi wabaya katika kila msimu wa uchaguzi licha ya kuwa kuna viongozi wazuri wanaostahili kuchaguliwa. Isitoshe, wananchi wa kawaida wanashikilia tamaduni zinazochangia dhuluma na hawataki kuziacha kwa sababu hawataki kuonekana watumwa. Aidha wananchi wenyewe wanavunjana mioyo ya kujikomboa kutoka kwa dhuluma kwa kudharauliana na kutusiana. Hali hii huwapa wadhulumu mazingira mwafaka ya kwendelea dhuluma dhidi ya wananchi wa kawaida.

Vilevile, utafiti umeonyesha athari mbalimbali zinazotokana na dhuluma dhidi ya mwananchi wa kawaida. Athari ya kwanza ni kifo ambacho kinaleta huzuni miongoni mwa wananchi wa kawaida na kuwavunja moyo. Wanaona kuwa hawathaminiwi na viongozi na walio na uwezo wa kiuchumi hali inayosababisha baadhi waanze kupigania haki zao. Hata hivyo, uchunguzi wa kidenguzi ulibainisha kuwa wananchi wenyewe walichangia vifo kupitia kwa matendo yao.

Aidha utafiti umebainisha athari ya umaskini inayotokana na wananchi wa kawaida kujidhulumu wenyewe. Wanachangia umaskini kwa kuwachagua viongozi wabaya na kutoweka juhudi katika kutafuta riziki ili kujiinua kiuchumi. Umaskini unaonekana kupitia ukosefu wa hela za kugharamia matibabu, chakula na hata karo ya watoto wao. Hali hii inawafanya wananchi wa kawaida kuwa na uhitaji mkubwa hivyo kushawishika kwa urahisi. Badala ya kuweka juhudi ili kujikomboa kiuchumi, baadhi ya wananchi wanajiunga na wadhulumu wao wanapotishwa kuwa watafutwa.

Athari nyingine iliyobainishwa ni utengano wa kijamii. Athari hii imetokana na uhasama miongoni mwa wananchi wa kawaida kati ya wanaopinga dhuluma na wanaoungana na wanaokisiwa kuwa wadhulumu. Ubinafsi na uhitaji mkubwa unawafanya baadhi ya wananchi kushawishika kwa urahisi na kujiunga na wadhulumu wao. Wananchi wa kawaida wanaoasi huchukiwa na wenzao kufikia hata kiwango cha kupigwa. Wao hudhani wanafanyiwa hisani wanapopewa kazi hata kama mshahara ni mdogo na mazingira ya kufanyia kazi ni duni. Kutokana na mtazamo huu, wao huwatetea waajiri wao na kuwapuuza wananchi wenzao licha ya kuwa wanadhulumiwa na mwajiri wanayemtetea. Wasichokifahamu ni kuwa mwajiri hutumia mbinu ya ‘tenga utawale’ ili kuuvunja umoja wao na hakika anafaulu panapotokea uhasama baina ya wananchi wa kawaida inavyojitokeza katika tamthilia teule.

Aidha, utafiti umeonyesha jinsi ambavyo mwananchi wa kawaida anavyoweza kujiepusha kutokana na dhuluma. Mwanzo, wanahitaji kuweka mikakati ya kubainisha na kuwachagua viongozi bora. Hawa ni wale viongozi ambao

wanayajali maslahi ya watu wote wakiwemo wananchi wa kawaida. Ni viongozi walio na utu na sera nzuri za kuimarisha sekta mbalimbali za kiuchumi. Uongozi wao utahakikisha kuwa kuna chakula cha kutosha, nafasi nyingi za kazi, mazingira salama ya kufanyia kazi, afya bora miongoni mwa huduma nyingine muhimu. Viongozi na uongozi unapokuwa mbaya ilivyobainishwa na utafiti, wananchi hasa wa kawaida hunyimwa huduma za kimsingi au huduma zenyewe huwa mbaya kutokana na ubinafsi wa viongozi waliochaguliwa.

Pili, utafiti umeonyesha kuwa wananchi wa kawaida wanahitaji kuweka juhudi katika harakati za kujikomboa kwa kutotegemea kazi za ajira tu ili kujiimarisha. Wanaweza kujiajiri kupitia biashara na kutia juhudi katika kazi nyinginezo kama kilimo. Kwa mfano, baadhi ya wananchi wanalaza damu kwa kulala badala ya kurauka mapema na kwenda shambani kulima. Mwishowe wanaangamia kutokana na njaa. Vilevile, wengine wanalalamika kuwa kazi waliyopewa na mwajiri wao ni mbaya kwa kuwa haina mshahara wa kutosha lakini hawaweki juhudi za kutafuta kazi iliyo nafuu ya kuwafanya wajitegemee. Wanaendelea kuwa maskini licha ya kufanya kazi hivyo kushindwa kugharamia mahitaji ya kimsingi kama vile afya na chakula bora. Na wengine hawaweki juhudi katika kujikomboa, badala yake wanakata tamaa na baadhi kutumia njia ya mkato kwa kujiunga na wadhalimu wao kutokana na ubinafsi na hofu kuwa huenda wasifue dafu katika azma yao ya kujikomboa.

Utafiti vilevile umeonyesha kuwa wananchi wanaweza kujiepusha na dhuluma dhidi yao kutokana na umoja miongoni mwao ambao utawapa ujasiri wa

kuwakemea wadhalimu licha ya kuwepo kwa vitisho. Bila shaka wadhalimu wanatumia askari, jela na vishawishi vya kuwanufaisha wachache katika mbinu ya ‘tenga utawale’ lakini wananchi wakiwa na ujasiri utakaotokana na umoja miongoni mwao, watastahimili yote na mwishowe kumshinda mdhulumu kutokana na nguvu za umoja wao.

Mwisho, utafiti umebainisha kwamba ili mwananchi kujiepusha na dhuluma, ni muhimu afahamu haki zake. Ni muhimu aelewa kuwa kupata mshahara mzuri na kufanyia kazi katika mazingira salama ni haki yake. Aidha, anahitaji kuthaminiwa na kupewa heshima kama mlipa ushuru na mshirika katika uchaguzi wa viongozi. Kwa hivyo ana haki ya kupata huduma bora ya afya na elimu na ufahamu wa haki hizi utampa mwananchi wa kawaida ari ya kuzipigania ili kuyaboresha maslahi yake.

5.4 MCHANGO WA UTAFITI

Kutokana na utafiti huu, imebainika kuwa mwananchi wa kawaida ana wajibu mkubwa katika kupunguza au kumaliza dhuluma dhidi yake. Ana uwezo wa kuhakikisha kuwa viongozi wanaongoza kwa njia inayojali maslahi ya wote wakiwemo wananchi wa kawaida.

Utafiti huu utachangia katika kuondoa imani kuwa wanaowadhulumu wananchi wa kawaida ni viongozi pekee. Mtazamo huu umeondolewa baada ya utafiti kuonyesha jinsi mbalimbali anazozitumia mwananchi wa kawaida kuchangia dhuluma dhidi yake kwa kujua au kutojua. Aidha, utafiti huu utachangia katika kuwahamasisha wananchi wa kawaida hasa katika Bara la

Afrika kwamba wana uwezo mkubwa katika kupambana na dhuluma dhidi yao na dhana kuwa wananchi wa kawaida hudhulumiwa na viongozi pekee si ya kweli.

Vilevile utafiti huu utachangia katika kuwapatia wananchi wa kawaida motisha ya kutetea haki zao kupitia mbinu zilizobainishwa katika sehemu ya matokeo ya utafiti kama vile kuwachagua viongozi bora, kuweka juhudi, kuwa jasiri na kufahamu haki zao. Pia utatumiwa kuwahimiza baadhi ya wananchi wa kawaida ambao hawana msimamo dhabiti umuhimu wa kupigania haki zao ili wajiepushe na dhuluma.

Utafiti huu utachangia kuwahamasisha viongozi hasa wa Kiafrika kuhusu umuhimu wa wananchi wa kawaida katika kufanikisha uongozi wao ili waweze kuwaheshimu na kuyazingatia maslahi yao. Utafiti huu pia utakuwa onyo kwa viongozi wanaondeleza uongozi mbaya kubadilisha njia zao za kuwaongoza wananchi wa kawaida kwa sababu wana uwezo wa kuwatoa uongozini.

Mwisho, utafiti huu utatumiwa kama changamoto kwa wananchi wa kawaida wanaowatukuza na kuwaenzi viongozi wabaya kutokana na ubinafsi na kigezo cha kuhusiana kwa njia moja au nyingine. Tabia hii hudidimiza juhudi za kujiepusha na dhuluma fauka ya kusababisha uhasama miongoni mwa wananchi wa kawaida wenyewe.

5.5 MAPENDEKEZO

Utafiti huu ulishughulikia suala la mwananchi wa kawaida kama mdhulumu wa maslahi yake katika tamthilia za *Kilio Cha Haki* (1981), *Amezidi* (1995) na *Mstahiki Meya* (2009). Tulionyesha jinsi mbalimbali mwananchi wa kawaida anavyochangia dhuluma, athari zinazotokana na dhuluma dhidi ya mwananchi wa kawaida na mbinu anazoweza kuzitumia kujiepusha na dhuluma. Mbali na kuangalia jinsi wananchi wa kawaida wanavyochangia dhuluma, kuna haja ya kufanya utafiti zaidi ili kubainisha jinsi mwananchi wa kawaida kama mdhulumu wa maslahi yake alivyoshughulikiwa katika fasihi simulizi. Utafiti unaweza kufanywa katika jamii tofauti kwa kuwa fasihi simulizi ni tofauti kutoka jamii moja hadi nyingine.

Aidha, utafiti zaidi unawezwa kufanywa ili kuchunguza jinsi nyimbo pendwa zilivyoshughulikia suala la mwananchi wa kawaida kama mdhulumu wa maslahi yake. Nyimbo hizi zinaweza kuangaliwa kwa kuchunguza ujumbe unaopitishwa kuhusu dhuluma.

Utafiti zaidi unaweza kufanywa ili kuchunguza jinsi mwananchi wa kawaida anavyosawiriwa kama mdhulumu wa maslahi yake katika riwaya za Kiswahili. Usawiri huu wa mwananchi wa kawaida unaweza kuchunguzwa kwa kulinganisha na kulinganua riwaya za kisasa na za kale ili kubainisha tofauti na kufanana kwa mbinu mbalimbali anazozitumia mwananchi wa kawaida kujidhulumu.

Vilevile, kuna haja ya kufanya utafiti zaidi katika tamthilia nyingine za Kiswahili ili kuchunguza jinsi suala la wananchi wa kawaida kama wadhulumu

wa maslahi yao lilivyoshughulikiwa. Ni muhimu pia kuchunguza viwango vya athari ya dhuluma kwa kuzingatia jinsia moja. Kwa mfano, kuangazia jinsia iliyoathiriwa zaidi na dhuluma na mchango wa kila jinsia katika kusababisha na kukabiliana na dhuluma dhidi yake. Utafiti huu utakuwa na mchango katika kuonyesha kuwa hakika tanzu zote za fasihi zina nafasi kubwa katika kukabiliana na dhuluma dhidi ya mwananchi wa kawaida katika jamii.

MAREJELEO

Abdilatif Abdalla (1973). *Sauti ya Dhiki*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Abdulla, M. (2014). "Dialectical Materialism." *Ecyclopedia Britannica* https://www.britannica.com. Ilipakuliwa 20. 06.2015

Arege, T. (2009). *Mstahiki Meya*. Nairobi: Vide~ Muwa Publishers.

Arvon, H. (1973). *Marxism and Esthetics*. London: Cornell University Press.

Bottomore, T. (ed) (1983). *A Dictionary of Marxist Thought*. Cambridge: Mass Harvard University Press.

Burgess, (1979). *Child Abuse: A situational Analysis in Advances in Clinical Child Psychology* (vol. 2). New York: Plenum Press.

Burman, E na Magie, M. (2005). *Deconstruction as a Method of Research*. New Delhi: Vistaar Publications.

Bwenge, C. (ed) (2003). *Uongozi Bora*. Montgomery: Women's Learning Partnership for Rights Development, and Peace

Chacha, N. (1986). *Mwongozo wa Ukame*. Nairobi: Heinemann Kenya Limited.

Chinua Achebe. (1975). *Morning Yet On Creation Day: Essays*. London: Heinemann Publishers.

Critchley, S. (1992). *The Ethics of Deconstruction*. Indiana: Purdue University Press.

Culler, J. (1982). *On Deconstruction: Theory and Criticism After Structuralism*. New York: Cornell University Press.

Derrida, J. (1976). *Of Grammatology. Trans. Gayatri Spivak*. Baltimore: Johns Hopkins.

Eagleton, T. (1976). *Marxism and Literary Criticism*. London: Methuen.

Eagleton, T. (1991). *Ideology: An Introduction.* London: Verso

Eguren, E. na Caraj, M. (2012). *Mwongozo Mpya wa Ulinzi kwa Watetezi Wa Haki Za Binadamu.* Brussels: Protection International.

Engels, F. (1975). *The Origin of the Family Private Property and the State*. New York: Pathfinders Press Inc.

Escholz, P. (1982). *Language Awareness.* New York: Martin's Press.

Gasche, R. (1986). *The Tain of the Mirror: Derrida and the Philosophy of Reflection.* Cambridge: Harvard University Press.

Gibbe, A. (1978). *Fasihi na Jamii: Washairi wa Kiswahili 1960- 1977*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi ya Kiswahili.

Gitau, E. (2005). "Unyanyasaji Dhidi ya Wanaume katika Fasihi Andishi ya Kiswahili." Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Gisele, L. Alyson, M. na Cindi, L. (2005). *Take Action Against Bulling (2nd Edition)* Guadalajara: Bully B'Ware Productions.

Gorki, M. (1975). *On Literature*. Washinton: University of Washington Press.

Hegel, F. (1818). *Introduction to Aesthetics*. Oxford: Clarendon.

Kamuf, P. (1991). *A Derrida Reader: Between the Blinds*. New York: Columbia University Press

Kareithi, P.M. (1969). *Kaburi Bila Msalaba*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Kezilahabi, E. (2008). *Dhifa*. Nairobi: Vide~ Muwa Publishers.

Khaemba, S. (1999). "Ulinganishi wa Maudhui ya Mapinduzi katika *Dunia Mti Mkavu* na *Kiza katika Nuru*." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Kimani, C.W. (2003). "Swala la Dhuluma Dhidi ya Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili." Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Kithaka, M. (2007). *Msimu wa Tisa*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Laititi, S. (2004). *Retrenchment and Domestic Violence: A cause Effect Analysis in Disasters.* Volume 4. Nairobi: Disaster Kenya Consult.

Lukacs, Georg (1979). *The Meaning of Contemporary Realism*. London: Merlin.

Lynch, M. na Roberts, J. (1982). *Consequences of Child Abuse*. London: Academic Press Inc. Ltd.

Mahero, J. (1992). " Maono ya Jamii katika Tamthilia za Chacha Nyaigoti Chacha: Swala la Uongozi." Tasnifu ya M. A Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Mavisi, R. (2007). "Usawiri wa Wahusika wa Kike katika kazi za Zainabu Burhani." Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Mazrui, A. (1981). *Kilio cha Haki.* Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Mohamed, S. A. (1980). *Sikate Tamaa*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mohamed, S. A. (2001). *Mwongozo wa Kilio cha Haki*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Mohamed, S. A. (1995). *Amezidi*. Nairobi: East African Publishrrs Ltd.

Momanyi, C. (1998). "Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili kama ilivyobainika katika Ushairi wa Kiswahili." Tasnifu ya Phd, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors.

Muindi, A. (1990). “Usawiri wa Wahusika Makahaba katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed.” Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Nangira, E. na Rapando, M. (2005). *Mwongozo wa Kifo Kisimani*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Ndungo, C. (1985). “Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria.” Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).

Ng’etich, D. (2011). “Dini kama Chombo cha Kuwadhulumu Waumini: Mifano kutoka Fasihi ya Kiswahili.” Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Ngugi wa Thiong’o. (1972). *Homecoming.* London: Heinmann Publishers.

Ngugi wa Thiong’o. (1981). *Writers in Politics.*Nairobi: East African Publishers.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

TUKI. (1980). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Senkoro, F. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Shaaban Robert (2003). *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Wafula, R.M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, W. K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.